# ATHARI ZA *SHENG'* KWA KISWAHILI SANIFU: UCHUNGUZI WA KAMUSI YA *SHENG'*.

**JOTHAM MUYUMBA**

**C50/CE/26142/2014**

**TASNIFU HII INAWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

**MEI, 2023**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi____________________________ Tarehe______________________________

**Muyumba Jotham**

**C50/CE/26142/2014**

## MSIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahihi____________________________ Tarehe______________________________

**Dkt. David Kihara**

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

## TABARUKU

Kwa watoto wangu wapendwa, Emannuel Feva na Oliver Sami. Walinisisimua kwa kudadisi nilichokuwa nikisoma. Kwa bibi yangu mpendwa Irene Nato kwa kuwa mvumilivu katika safari hii ya usomi. Kwa babangu Samuel Muyumba kwa jitihada zake za kunitia moyo na kuniombea katika safari za usomi. Dai lake kuwa “mnyonge hufarijika” lilinitia moyo.

## SHUKRANI

Namshukuru mwenyezi Mungu kwa kunifanikisha nikawa na uwezo wa kutamatisha kazi hii. Ni kweli kuwa kwa imani na jitihada, chochote chawezakana. Shukrani zangu za dhati zimwendee msimamizi wangu Dr. David Kihara. Ama kweli alinitoa mbali. Aliniokota jangwani, akanishika bega na kunipa mwelekeo. Akanijaza tumaini wakati nilipokuwa nimekata tamaa. Hekima na busara akanijaza hadi tulipofika tamatini. Daktari Mungu akubariki. Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahilii katika chuo kikuu cha Kenyatta kwa kunipa motisha katika kazi hii, hususan Dkt.Onyango. Sitasahau mchango wake katika kuisisimua na kupiga msasa mada tangulizi ya kazi hii.  Aidha, ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu, Barasa Wafula na James Matseshe kwa mchango wao masomoni ulionifaa sana.

# YALIYOMO

**IKIRARI………..........................................................................................ii**
**TABARUKU….........................................................................................iii**
**SHUKRANI……......................................................................................iv**
**YALIYOMO…..........................................................................................v**
**ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO ............................................................x**
**ORODHA YA MAJEDWALI .....................................................................xi**
**MAELEZO YA ISTILAHI........................................................................xiii**
**IKISIRI………… ......................................................................................xiv**
**ABSTRACT………….................................................................................xv**
**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI……...........................................................1**
1.1 Usuli wa Mada........................................................................................1
1.2 Suala la Utafiti........................................................................................4
1.3 Malengo ya Utafiti...................................................................................5
1.4 Maswali ya Utafiti ...................................................................................5
1.5 Sababu ya kuchagua mada .........................................................................6
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti..........................................................................8
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada .......................................................................9
1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu ukuaji wa Sheng’ ...................................................12
1.7.2 Uundaji wa maneno katika Sheng’ ...........................................................32
1.7.3 Fonolojia ya Sheng’ ..............................................................................36
1.8 Misingi ya nadharia ...................................................................................39
1.8.1 Mihimili ya nadharia fonolojia boreshi........................................................41
1.8.1.1 Umajumui...........................................................................................41
1.8.1.2 Ukiukwaji ...........................................................................................42
1.8.1.3 Upangiliaji...........................................................................................43
1.8.1.4 Usambamba ........................................................................................43
1.8.2 Utumikizi wa Nadharia ya Fonolojia Boreshi katika utafiti huu .................47
1.9 Mbinu za Utafiti .......................................................................................50
1.9.1 Muundo wa Utafiti ..................................................................................51

1.9.2 Mahali pa Utafiti ..... 51
1.9.3 Jumuiya ya utafiti ..... 52
1.9.4 Uteuzi wa sampuli ..... 52
1.9.5 Ukusanyaji wa data ..... 52
1.9.6 Uchanganuzi wa data ..... 53
1.9.7 Uwasilishaji wa data ..... 53
1.10 Hitimisho ..... 53
**SURA YA PILI: MANENO KATIKA S.E.D AMBAYO HUTUMIKA KATIKA KISWAHILI SANIFU.** ..... 54
2.1 Utangulizi ..... 54
2.2 Maneno katika Sheng'- English Dictionary yanayotumika katika Kiswahili sanifu. ..... 54
2.2.1 Nomino katika S.E.D ..... 55
2.2.2 Vitenzi katika S.E.D ..... 57
2.2.3 Vivumishi katika S.E.D ..... 59
2.3 Sifa za kisemantiki za maneno katika S.E.D. ..... 66
2.3.1 Uhamishaji wa maana ..... 66
2.3.2 Polisemi ..... 68
2.3.3 Sinonimu ..... 69
2.3.3.1 Sinonimu jozi ..... 70
2.3.3.2 Sinonimu utatu ..... 71
2.3.3.3 Sinonimu unne ..... 72
2.4 Maneno ya S.E.D yanayojitokeza katika miktadha mbalimbali. ..... 73
2.4.1 Sheng' katika vyombo vya habari ..... 74
2.4.2 Sheng' katika magazeti. ..... 75
2.4.3 Sheng' katika mitandao ya kijamii ..... 76
2.4.4 Sheng' katika sekta ya Jua Kali ..... 77
2.4.5 Sheng' katika matangazo ya Biashara ..... 78
2.4.6 Sheng' ughaibuni ..... 81
2.4.7 Sheng' katika muziki wa reggae ..... 82
2.4.8 Sheng' katika usafiri wa matatu ..... 83

2.5 Hitimisho .......... 84

**SURA YA TATU: MUUNDO WA KIFONOLOJIA WA MANENO YA SHENG' .......... 86**

3.1 Utangulizi .......... 86

3.2 Fonolojia ya Sheng' .......... 86

3.2.1 Fonimu za Sheng' .......... 87

3.2.2 Vokali za Sheng' katika leksimu za S.E.D .......... 89

3.2.2.1 Fonimu /ɛ/ katika Sheng' .......... 96

3.2.2.2 Fonimu /ɔ/ katika Sheng' .......... 97

3.2.2.3 Vokali /i/ na /e/ katika Sheng' .......... 98

3.2.2.4 Vokali ndefu katika Sheng'. .......... 100

3.2.3 Konsonanti za Sheng' .......... 101

3.3 Silabi za Sheng' .......... 103

3.3.1 Miundo ya silabi za Sheng' .......... 107

3.3.1.1 Miundo ya silabi za nomino za sheng'. .......... 108

3.3.1.2 Silabi za vitenzi vya Sheng' .......... 111

3.3.1.3 Silabi za vivumishi vya sheng' .......... 114

3.3.1.4 Silabi za vielezi katika Sheng' .......... 115

3.3.3 Dhana ya ukanushi katika Sheng' .......... 116

3.3.4 Nyakati na hali katika Sheng' .......... 117

3.4. Mifanyiko ya kifonolojia katika Sheng' .......... 119

3.4.1 Kudhoofika kwa fonimu .......... 119

3.4.2 Usilimishwaji wa fonimu .......... 120

3.4.3 Udondoshaji wa silabi katika maneno ya S.E.D. .......... 122

3.4.4 Tangamano la irabu katika Sheng' .......... 122

3.5 Sifa za arudhi za Sheng' .......... 123

3.5.1 Jinsi shadda inavyojitokeza katika Sheng'. .......... 123

3.5.2 Kiimbo katika Sheng'. .......... 125

3.5.2.1 Kiimbo cha kauli au maelezo. .......... 125

3.5.2.2 Kiimbo cha maulizo .......... 126

3.5.2.3Kiimbo cha amri .......... 126

3.5.2.4Kiimbo cha mshangao ..................................................................... 126
3.5.3 Toni katika Sheng' ........................................................................... 126
3.6 Hitimisho ........................................................................................... 128
**SURA YA NNE:SABABU ZA TOFAUTI ZA KIMUUNDO KATIKA MATUMIZI YA SHENG' NA KISWAHILI SANIFU. ........... 131**
4.1 Utangulizi ......................................................................................... 131
4.2 Sababu zinazochangia kuwepo kwa tofauti kati ya Sheng' na KS .................. 131
4.2.1 Kuficha siri katika Sheng' ................................................................. 131
4.2.2 Athari za Lugha changizi. .................................................................. 134
4.2.2.1 Athari za lugha changizi kwa irabu za Sheng' ............................... 135
4.2.2.2 Athari za lugha changizi kwa toni ya Sheng' ................................. 137
4.2.2.3 Athari za lugha changizi katika unyambuzi wa vitenzi. ................. 138
4.2.3 Ubunifu wa wazungumzaji .................................................................. 140
4.2.4 Mienendo ya kisasa ............................................................................ 142
4.2.5 Hali ya maisha na uchumi ................................................................... 143
4.2.6 Kurahisisha mawasiliano .................................................................... 145
4.2.7 Sheng' hutumika kama lugha tenganishi. ............................................ 147
4.2.8 Sababu za tasfida ................................................................................ 149
4.3 Hitimisho ........................................................................................... 151
**SURA YA TANO: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI** ........................................................................ 153
5.1 Utangulizi .......................................................................................... 153
5.2 Muhtasari wa tasnifu. ......................................................................... 153
5.3 Matokeo ya Utafiti .............................................................................. 156
5.3.1 Ubainishaji wa maneno katika S.E.D .................................................. 156
5.3.2 Muundo wa kifonolojia wa maneno ya Sheng' ..................................... 159
5.3.3 Sababu za tofauti za kimuundo katika matumizi ya Sheng' na Kiswahili sanifu. ........................................................................................ 164
5.4 Changamoto za utafiti. ........................................................................ 167
5.5 Mapendekezo ya utafiti zaidi ............................................................... 168
**MAREJELEO**……. ................................................................................. 169

**VIAMBATISHO**……………………………………………………………………173
**Kiambatisho A: Data Iliyotumika Katika Utafiti Huu.** ....................................... 173
**Kiambatisho B: Kibali cha Utafiti cha Chuo Kikuu cha Kenyatta.** .................... 187
**Kiambatisho C : Leseni ya Utafiti ya Nacosti.** .................................................... 188
**Kiambatisho D : Kibali cha Utafiti cha Kaunti Ndogo ya Kakamega Kaskazini.** ............................................................................................ 189
**Kiambatisho E : Kibali cha Utafiti cha Kaunti ya Kakamega.** ........................... 190
**Kiambatisho F: Ripoti ya Uzuiaji Wizi wa Kiakademia** ..................................... 191

# ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ø** | **Mofu kapa** |
| * | Sio sahihi |
| $ | Mpaka baina ya silabi |
| # | Mpaka wa silabi |
| > | Yakatokea |
| { } | Alama za kuonyesha mofu |
| < --- > | Kuwepo kwa mfanyiko wa kimofofonolojia. |
| ⟶ | Mawimbi ya kiimbo. |
| Ɵ | Mofu kappa. |
| E | Kielezi |
| H | Kihusishi |
| K | Konsonanti |
| KS | Kiswahili sanifu |
| N | Nomino |
| T | Kitenzi |
| S.E.D | *Sheng'* - English Dictionary |
| V | Kivumishi |

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali la 1: Msamiati katika sajili ya matatu: Kihara (2006)........................... 19
Jedwali la 2: Vokali za Sheng’ (Mwihaki, 2007) ............................................. 37
Jedwali 3: Mfumo wa Kifonetiki wa *Sheng’* (Ferrari, 2014) ............................ 38
Jedwali 4: Mfano wa Umbotokeo katika *Sheng’* ............................................... 46
Jedwali 5: Namna mashartizuizi huamua umbotokeo katika maneno ya *Sheng’* ........................................................................................... 50
Jedwali 6: Orodha ya nomino katika S.E.D zinazojitokeza katika Kiswahili Sanifu ........................................................................................... 56
Jedwali 7: Orodha ya vitenzi katika S.E.D vinavyojitokeza katika Kiswahili Sanifu ........................................................................... 58
Jedwali 8: Orodha ya vivumishi katika S.E.D vinavyojitokeza katika Kiswahili Sanifu ........................................................................... 59
Jedwali 9: Orodha ya vihusishi katika S.E.D vinavyojitokeza katika Kiswahili Sanifu ........................................................................... 61
Jedwali 10: Vielezi katika S.E.D vinavyojitokeza katika Kiswahili Sanifu ....... 61
Jedwali 11: Idadi ya maneno yakipangwa kiabjadi .......................................... 63
Jedwali 12: Idadi ya maneno kiorodha kuanzia idadi nyingi hadi chache.......... 64
Jedwali 13: Kuhamisha maana katika S.E.D.................................................... 68
Jedwali 14: Polisemi katika S.E.D.................................................................. 69
Jedwali la 15: Sinonimu jozi katika S.E.D....................................................... 71
Jedwali la 16: Sinonimu utatu katika S.E.D.................................................... 71
Jedwali la 17: Sinonimu unne katika S.E.D. .................................................... 72
Jedwali 18: Maneno ya S.E.D yanayotumika katika kipindi cha Kizazi Kipya katika *Redio Citizen*................................................................ 74
Jedwali 19: Maneno ya *Sheng’* katika gazeti (Taifa Leo, Juni 22, 2022)........... 76
Jedwali 20: Matumizi ya *Sheng’* katika mitandao ya kijamii ............................ 77
Jedwali 21: Maneno ya S.E.D katika matangazo ya biashara ............................ 79
Jedwali la 22: Matumizi ya *Sheng’* miongoni mwa wanafunzi katika shule za mashambani (Githiora 2018). ...................................................... 80

Jedwali 23: Maneno ya S.E.D katika sekta ya matatu ..................................... 83
Jedwali la 24: Vokali za *Sheng'* (Mugambi 2007) ........................................... 90
Jedwali 25: Maneno yanayotokana na vokali za *Sheng'* katika S.E.D............... 95
Jedwali 26: Fonimu /ɛ/ katika *Sheng'* ............................................................ 96
Jedwali 27: Fonimu /ɔ/ katika *Sheng'* ............................................................ 97
. Jedwali 28: Maneno mkopo ya *Sheng'* katika S.E.D..................................... 99
Jedwali 29: Konsonanti za *Sheng'* (Mwihaki 2007)...................................... 101
Jedwali 30. Konsonanti za *Sheng'*: Githinji (2022)...................................... 102
Jedwali 31: Konsonanti za *Sheng'* katika S.E.D ambazo hazipatikani katika KS ........................................................................... 103
Jedwali 32: Silabi funge na silabi wazi katika S.E.D .................................... 105
Jedwali 33: Miundo ya silabi za *Sheng'* ....................................................... 105
Jedwali 34: Silabi funge za *Sheng'* katika S.E.D .......................................... 106
Jedwali 35: Nomino zenye muundo wa konsonanti pekee kwenye silabi. ....... 109
Jedwali 37: Silabi #*nga*# ya ukanushi katika S.E.D. ...................................... 113
Jedwali 38: Vivumishi katika S.E.D............................................................. 114
Jedwali 39: Muundo wa vielezi katika *Sheng'* ............................................... 115
Jedwali 40: Ukanushi katika *Sheng'* ............................................................ 116
Jedwali 41: Hali ya mazoea katika *Sheng'* ..................................................... 118
Jedwali 42: Fonimu za udogo katika maneno ya S.E.D ................................. 119
Jedwali 43: Umbo la wingi la nomino katika S.E.D ...................................... 121
Jedwali 44: Shadda katika maneno ya *Sheng'* .............................................. 124
Jedwali 45: Shadda katika silabi tamati katika *Sheng'* .................................. 124
Jedwali 46: Kiimbo katika maneno ya S.E.D................................................ 125
Jedwali 47: Maneno yenye toni katika S.E.D ................................................ 128
Jedwali 48: Kutambua vokali za Ekegusii (Makini,2015).............................. 135
Jedwali 49: Matumizi ya kiambishi #*nga*# katika vitenzi vya *Sheng'* ............. 139
Jedwali 50: Maneno ya S.E.D yanayoonyesha ubunifu................................. 141
Jedwali 51: Udogo katika *Sheng'* ................................................................ 146
Jedwali 52: Maneno ya tasfida katika S.E.D................................................. 150

# MAELEZO YA ISTILAHI

**Lugha changizi** Lugha ambayo hutoa maneno ili yakubalike katika lugha ya pili.

**Lugha pokezi** Lugha inayopokea maneno ya mkopo kutoka lugha changizi.

**Mashartizuizi** Vizuizi vinavyofanya neno fulani likubalike au lisikubalike katika lugha pokezi.

**Umbotokeo** Neno lenye umboghafi ambalo halijaboreshwa na kukubalika katika lugha pokezi.

**Umboghafi** … Neno ghafi ambalo halijapitia vizuizi vya lugha kabla ya kukubalika katika lugha sanifu.

***Sheng'*** Msimbo wa lugha ya Kiswahili ambao asili yake ni mchanganyiko wa maneno ya Kiswahili, Kiingereza na lugha za kienyeji na ambao chimbuko lake ni mitaa ya mabanda jijini Nairobi.

## IKISIRI

Utafiti huu ulidhamiria kutathmini athari za kamusi ya *Sheng' – English Dictionary* kwa Kiswahili sanifu. Kamusi ya *Sheng' –English Dictionary* (2003) iliteuliwa kama msingi wa uchunguzi huu kwa sababu ndio kamusi ya kwanza ya *Sheng'* kuwahi kuchapishwa. Licha ya kamusi hii kuchapishwa katika lugha ya Kiingereza ina leksimu za *Sheng'* ambazo yafaa kuchunguzwa namna zinavyoathiri Kiswahili sanifu kwa wakati wa sasa. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kubainisha maneno yaliyomo katika *Sheng'*- *English Dictionary* na katika Kiswahili sanifu. Kadhalika, utafiti huu ulinuia kueleza muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* na jinsi yanavyotofautiana na Kiswahili sanifu. Mwisho, utafiti huu ulidhamiria kueleza sababu za utofauti wa muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* na kueleza athari zake kwa Kiswahili sanifu. Nadharia ya utafiti ilikuwa Nadharia ya Fonolojia Boreshi ambayo inapatikana katika mtazamo mpana wa Nadharia Boreshi iliyoasisiwa na Alan Prince na Paul Smolensky (1991). Hii ni nadharia inayochunguza hatua za ukuaji wa msamiati kutoka hali ghafi hadi ukubalifu wake kupitia kwa vizuizi tofauti. Mahali pa utafiti palikuwa maktabani na mtandaoni. Mbinu ya uchunguzi ikawa kupitia kusikiliza wazungumzaji wa *Sheng'* na kusoma makala mbalimbali kuhusu mada hii. Data ilikusanywa kupitia kwa kuchunguza maneno na vidahizo vya maneno kutoka kamusi ya *Sheng' – English Dictionary* (2003). Iliaminika kuwa kamusi hii ingetoa sampuli ya maneno mahsusi ya *Sheng'* ambayo muundo wake huathiri matumizi katika Kiswahili sanifu kwenye jamii ya kisasa. Uchanganuzi wa maelezo ulitegemea mtazamo wa Fonolojia Boreshi katika nadharia ya fonolojia inayoangazia sarufi zalishi. Katika mtazamo huu, uambishaji wa maneno uliangaziwa na jinsi uundaji huo hutawaliwa na vizuizi mbalimbali na sheria za fonolojia. Kadhalika nadharia ya Fonolojia Boreshi ilitumika kueleza michakato ya namna wazungumzaji wa *Sheng'* hubuni leksimu mbalimbali katika mawasiliano. Uwasilishaji wa data ulikuwa kupitia kwa maelezo ya kina, michoro na jedwali. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa: maneno yanayopatikana katika *Sheng' – English Dictionary* na Kiswahili sanifu yalibainishwa. Pia, muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* na namna yanavyotofautiana na Kiswahili sanifu ulielezwa. Kadhalika, sababu zinazochangia utofauti wa muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu zilielezwa. Uchunguzi huu ulidhamiria kuchangia usomi wa Kiswahili kwa kuweka wazi athari za *Sheng'* katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili kimsamiati. Kadhalika, utafiti huu utawasaidia wanafunzi kuweka mipaka bayana kati ya msimbo wa *Sheng'* na lugha ya Kiswahili sanifu.

## ABSTRACT

This study was meant to assess the impact of *Sheng'-English Dictionary* (2003) on Standard Swahili. The *Sheng'- English Dictionary* (2003) was selected as the basis of this research since it was the first *Sheng'* dictionary to be published. Though the dictionary was published in English, it has *Sheng'* lexemes that need to be studied to assess their impact on the current Standard Swahili. Objectives of the research were to identify *Sheng'* words in *Sheng'-English Dictionary* that also exist in Standard Swahili. It also aimed at explaining phonological structure of *Sheng'* words and how they differ with Standard Swahili words. Furthermore, the research was meant to explain reasons for the phonological structural difference of *Sheng'* words and their impacts on Standard Swahili equivalent. These difference could clearly point out how they affect Standard Swahili usage. The theory of the study was Phonological Optimality Theory that is anchored on the main Optimality Theory that was introduced by Alan Prince and Paul Smolensky (1991). The core tenets of this theory was that words pass through series of violable constraints before being incorporated in a given language. Methods of research entailed listening to *Sheng'* speakers and content analysis. Data was collected by analyzing *Sheng'* words derived from *Sheng' – English Dictionary* (2003). Descriptive data analysis method was used basing on Phonological Optimality Theory. The major findings of this study was that: *Sheng'* words in *Sheng'-English Dictionary* that also exist in Standard Swahili were identified. Likewise, phonological structure of *Sheng'* words and how they differ with Standard Swahili words were explained. Furthemore, reasons for the phonological structural difference of *Sheng'* words and their Standard Swahili equivalent were explained. This research will contribute to academic growth of Kiswahili through ascertaining the phonological effects of *Sheng'* to standard Swahili. Moreover, the research will assist learners in drawing clear disparities between *Sheng'* and standard Swahili.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

*Sheng'* ni msimbo wa lugha ya Kiswahili ambao asili yake ni mchanganyiko wa maneno ya Kiswahili, Kiingereza na lugha za kienyeji. Kwa muijibu wa Githinji (2022), msimbo huu huchukuliwa kuwa wa lugha ya Kiswahili na wala sio lugha nyinginezo kwa sababu mfumo wake wa kisarufi kimofofonolojia huwiana na Kiswahili sanifu. Chimbuko lake ni mitaa ya mabanda mashariki mwa mji wa Nairobi. Mitaa hiyo kwa mujibu wa Githiora (2018) ni; Eastleigh, Mathare, Ngara, Pangani na Kaloleni. Utafiti huu ulidhamiria kubainisha athari za chapisho la *Sheng' English Dictionary* (S.E.D) kwa Kiswahili sanifu (KS). Msimbo wa *Sheng'* umeimarika na kusambaa tangu kubuniwa kwake katika mitaa ya mabanda jijini Nairobi. Hadi sasa msimbo huu umepata umaarufu mkubwa sana miongoni mwa vijana sio tu katika sehemu za mijini bali hata katika maeneo ya mashambani. Umaarufu huu kimatumizi ulifikiriwa kuwa huenda ukawa na athari anuai kwa KS. Tafiti nyingi zimefanywa awali kuchunguza athari hizi. Hata hivyo, kulikuwa na haja ya kufanya uchunguzi zaidi namna chapisho la S.E.D (2003) lilivyoathiri ukuaji wa *Sheng'* kwa upande mmoja, na kupungua kwa matumizi ya msamiati kifonolojia kwa KS kwa upande mwingine.

Iraki (2004), adokeza kuwa msimbo wa *Sheng'* ulizuka katika miaka ya 60 mashariki mwa jiji la Nairobi. Dai hili linaungwa mkono na Ferrari (2014) anayesema kuwa

msimbo wa *Sheng'* huenda ulizuka mnamo miaka ya 60 jijini Nairobi. Naye Salome' (2020), akadai kuwa msimbo huu ulizuka katika maeneo ya mabanda mashariki mwa Nairobi mnamo miaka ya 1970. Muaka (2011) alisema kuwa *Sheng'* ni mchanganyiko wa lugha inayozungumzwa na vijana katika sehemu za mijini. Madai haya yaliungwa mkono na Mbaabu na Kipande (2003) kwa kudai kuwa, mwanzoni *Sheng'* ilichukuliwa kuwa mchanganyiko wa lugha kati ya Kiswahili na Kiingereza.

Ni kutokana na lugha hizi mbili; Kiswahili na Kiingereza ndiko kulizuka neno *Sheng'*. Kiswahili (*Sh*) na Kiingereza (*Eng*) na kuzua *Sheng'*. Msimbo huu ulianza kukua na kuimarika kwa kupata msamiati mpana kutoka lugha zingine za kienyeji nchini Kenya. Ukuaji huu ukaanza kuwa tishio kwa umaarufu wa KS. Dai hili lilichochea haja ya kufanya utafiti kutathmini ikiwa kuna uwezekano wa KS kuathirika kifonolojia kutokana na matumizi mapana ya leksimu za *Sheng'* hasa baada ya chapisho la kamusi ya S.E.D (2003). Kwa mujibu wa utafiti huu, athari hizi zinachangia kupungua kwa matumizi ya baadhi ya leksimu za KS. Msimbo huu umeenea kutoka mijini hadi sehemu za mashambani.

Sarufi ya *Sheng'* ina uwiano mkubwa sana na Kiswahili sanifu (Githiora, 2018). Yaaminika chimbuko lake ni sehemu za mabanda mashariki mwa jiji la Nairobi. Mwanzoni watu wengi walikuwa na hisia hasi kuhusu *Sheng'*. Walihusisha *Sheng'* na watu wahuni, majangili na utingo wa matatu. Kwa mujibu wa Githiora (2018), *Sheng'* imevuka mipaka ya kijiografia na kijamii na kutumika na watu wengi hasa vijana kote nchini. Umaarufu wa matumizi haya ulichunguzwa katika utafiti huu na namna

unavyoathiri KS. Kuchapishwa kwa kamusi ya *Sheng'- English Dictionary* (2003), kulisisimua mwamko mpya wa kutathmini ukuaji wa msimbo wa *Sheng'* na athari zake katika lugha sanifu ya Kiswahili. Awali, kulikuwa na dhana kuwa msimbo wa *Sheng'* ni wa vijana wa mtaani na ambao hauwezi kudumu. Lugha hii imeendelea kukua na kupata nafasi katika machapisho ya kisasa na hata kwenye vyombo vya habari, (Ferrari, 2014). Dhana hii ilifaa kutathminiwa kubainisha ikiwa kuendelea kukua kwa *Sheng'* kunaathiri KS.

Wataalam wamefanya utafiti kuhusu ukuaji wa *Sheng'* na mwingiliano wake na lugha ya Kiswahili. Mekonge (2016), alifanya utafiti kuhusu athari za *Sheng'* katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili za Gusii Highlights na Daraja Mbili mjini Kisii. Katika utafiti wake, alijaribu kuonyesha namna *Sheng'* inavyosababisha matokeo duni kwa wanafunzi wa shule za upili.

Naye Mwenesi (2022), akafanya utafiti kuhusu namna dhana ya umaratokezi wa msamiati wa *Sheng* katika upokezi lugha wa Kiswahili miongoni mwa Wanadaraja la Awali katika shule za msingi mjini Mbale, kaunti ya Vihiga, Kenya. Hata hivyo, utafiti wao haukuonyesha namna maneno ya S.E.D yalivyojitokeza na kupenyeka katika Kiswahili sanifu kifonolojia. Kamusi ya *Sheng' –English Dictionary* (2003) iliteuliwa kama msingi wa uchunguzi huu kwa sababu ndio kamusi ya kwanza ya *Sheng'* kuwahi kuchapishwa. Isitoshe, utafiti wa awali kuhusu kamusi hii ulibaini kuwa kuna data ya kutosha itakayowezesha kufanya uchunguzi kuhusu maneno ya *Sheng'*.

Yamkini chapisho la kamusi kwa lugha yoyote ni dhihirisho tosha kuwa lugha hiyo inaanza kupata umaarufu. Utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa S.E.D kifonolojia kwa KS. Kadhalika, ulidhamiria kuangazia aina za maneno katika S.E.D ambayo yalijitokeza katika KS. Vilevile, utafiti huu ulilenga kubaini namna kuchipuka kwa msamiati wa *Sheng'* kunavyosababisha kupungua kwa matumizi ya leksimu za KS. Utafiti huu ulidhamiria kuweka wazi dhana kuwa matumizi ya maneno katika S.E.D yanaweza kuwa yamejipenyeza katika Kiswahili Sanifu. Kuna baadhi ya misamiati ya Kiswahili Sanifu iliyoweza kupungua kimatumizi kwa sababu ya matumizi mapana ya maneno ya *Sheng'*. Huenda leksimu za KS zikafifia au kupotea kabisa kwa kupata leksimu mbadala kutoka kwa *Sheng'*. Uchunguzi huu ulikusudia kuchangia usomi wa Kiswahili kwa kuweka wazi athari za *Sheng'* katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili kifonolojia. Kadhalika, utafiti huu utawasaidia wanafunzi wa lugha ya Kiswahili kuweka mipaka bayana kati ya msimbo wa *Sheng'* na lugha ya Kiswahili sanifu.

### 1.2 Suala la Utafiti

Msimbo wa *Sheng'* umesambaa sana kimatumizi. Tafiti nyingi zimewahi fanywa awali kuchunguza chimbuko, ukuaji na athari zake katika Kiswahili sanifu. Ingawa uchunguzi wa awali uligusia maswala ya athari za *Sheng'*, hamna ushahidi wa kutosha kitaaluma kudhihirisha athari za S.E.D kifonolojia katika KS.

Kwa mfano, Bosire (2014) alihusika zaidi kueleza kwa kina ukuaji wa *Sheng'* kihistoria na kijamii, na vile vile miundo yake kifonolojia na kimofolojia kwa upana sana. Utafiti wake ulitufaidi zaidi kwa kuonyesha namna *Sheng'* ilivyokua na akatoa

maelezo kwa kina kuhusu miundo yake changamano ya kifonolojia na kimofolojia. Hata hivyo uchunguzi wa Bosire (2014), haukuchunguza kwa kina namna leksimu kutoka S.E.D zinavyoathiri KS. Kwa hivyo, ni kusudi la utafiti huu kujikita katika kuchunguza iwapo kuna uwezekano wa matumizi ya maneno ya S.E.D yanayoweza kuwa yamejipenyeza kwa Kiswahili sanifu. Kuna uwezekano kuwa msamiati wa Kiswahili sanifu waweza kupungua kimatumizi kwa sababu ya athari za *Sheng'*. Sababu mojawapo yaweza kutokana na matumizi ya maneno mbadala kutoka kwa S.E.D.

**1.3 Malengo ya Utafiti**

Malengo ya utafiti huu yalikuwa:

i. Kubainisha maneno yaliyomo katika *Sheng'- English Dictionary* na katika Kiswahili sanifu.
ii. Kueleza muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* na jinsi unavyotofautiana na wa Kiswahili sanifu.
iii. Kueleza sababu za tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na kueleza athari zake kwa Kiswahili sanifu.

**1.4 Maswali ya Utafiti**

i. Ni maneno yapi yaliyojitokeza katika *Sheng'*-English Dictionary na ambayo yapo katika Kiswahili sanifu?
ii. Muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* unatofautiana vipi na wa Kiswahili sanifu?

iii. Ni sababu zipi za kimuundo zinazoleta tofauti katika matumizi ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu na zina athari zipi kwa Kiswahili sanifu.

**1.5 Sababu ya kuchagua mada**

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza athari za msimbo wa *Sheng'* kwa Kiswahili sanifu. Madai ya wataalamu kama vile Warambo (2017), Salome' (2020), Konnor. na Hinter. (2021) na Githinji (2022) kuwa sarufi na miundo ya maneno kimofofonojia ya *Sheng'* yanawiana na Kiswahili sanifu yafaa kuchunguzwa. Hii ni kwa sababu kukaribiana huku kunaweza kuchangia katika kupungua kwa matumizi ya baadhi ya leksimu za Kiswahili sanifu na mahali pake pakachukuliwa na msimbo wa *Sheng'*. Mada hii ilichaguliwa kwa sababu tangu kuchapishwa kwa kamusi ya *Sheng'- English Dictionary (2003)*, suala la athari za kamusi hii kifonolojia kwa Kiswahili sanifu lilifaa kuchunguzwa na wataalamu. Kulikuwa na uwezekano kuwa, tangu kuchapishwa kwa kamusi hii matumizi ya Kiswahili Sanifu yameathirika. Leksimu za *Sheng'* katika S.E.D huenda zimepenyezwa kwa Kiswahili sanifu. Muda mrefu uliopo tangu chapisha la S.E.D. (zaidi ya miaka 17) unafaa zaidi katika kuchunguza matumizi ya leksimu za lugha katika jamii. Leksimu hizi zilifaa kuchunguzwa ili kubaini iwapo zilichangia kuathirika kwa baadhi ya maneno katika Kiswahili Sanifu.

Kamusi za *Sheng'* zilizochapishwa hivi karibuni hazikuchaguliwa kwa sababu leksimu nyingi zinazobuniwa upya huchukuwa muda mwingi kabla ya kupata uzoefu wa kimatumizi katika mawasiliano; Iraki (2004). Mugambi (2007) alifanya utafiti kuhusu utohozi wa maana katika maneno ya *Sheng'*. Uchunguzi wake ulitoa mwanya wa jinsi msimbo wa *Sheng'* unavyokua kwa kupata msamiati mpya kupitia kwa njia ya

utohozi. Hata hivyo, utafiti huo haukubainisha mchango wa kifonolojia wa kamusi ya S.E.D. katika Kiswahili sanifu. Iraki (2004), alieleza kuwa kuna ushindani mkubwa sana wa matumizi ya *Sheng'*, lugha za kienyeji, Kiingerea na KS miongoni mwa vijana. Hali hii hupelekea kubuni aina nyingi za leksimu kuafiki dhana na matakwa mbalimbali ya mawasiliano.  Aidha, hali hii yaweza kuzua hatari ya kupuuza au kutupilia mbali baadhi ya leksimu za lugha hizi mbadala. Kando na mawasiliano, *Sheng'* hutumika na vijana kama lugha ya utangamano na ya kujitambulisha.

Kwa kuangazia sababu zinazochangia kuwepo kwa tofauti kati ya muundo wa leksimu za *Sheng'* na za Kiswahili sanifu, mtafiti aliweza kutathmini namna *Sheng'* hupenyezwa katika Kiswahili sanifu.  Iwapo matumizi haya yaweza kuendelea kuimarika, yaweza kuwa tishio kubwa linaloweza kuathiri KS kwa kusambaratika au kupungua kwa matumizi ya baadhi ya leksimu za KS. Dhana hii ndio iliupa utafiti huu msukumo wa kuchunguza namna *Sheng'* ilivyoathiri ukuaji wa KS. Lilikuwa kusudi la utafiti huu kuweka wazi athari za S.E.D. kifonolojia kwa Kiswahili sanifu tukirejelea kamusi ya S.E.D. Kamusi hii ilichaguliwa kimakusudi kwa sababu uchapishaji wake ulichangia kuonyesha leksimu za *Sheng'*. Kama anavyodai Mbaabu (1996), Kiswahili kama zilivyo lugha zingine huwa na uwezo wa kukopa msamiati kutoka kwa lugha zingine. Ukopaji ndio huimarisha ukuaji wa lugha. Madai ya Ferrari (2014) kuwa sarufi ya *Sheng'* inakaribiana sana na KS, yanaweza kuzua hofu kuwa ni rahisi leksimu za *Sheng'* kupenyezwa katika KS.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kutathmini ikiwa maneno ya *Sheng'* yalijitokeza katika Kiswahili Sanifu. Kamusi ya S.E.D iliteuliwa makusudi kwa sababu ni kamusi ya kwanza kuchapisha katika msimbo wa *Sheng'*. Kuna kamusi zingine za *Sheng'* ambazo zimechapishwa hivi karibuni. Kamusi hizo hazikushughulikiwa katika utafiti huu kwa sababu kipindi kirefu kilichopo baada ya chapisho la S.E. D (2003) kinatoa nafasi bora ya kutathmini namna leksimu za *Sheng'* zinavyokua na kuathiri Kiswahili sanifu. Maneno na vidahizo vya maneno katika kamusi ya S.E.D (2003) yalitumiwa kama msingi wa uchunguzi. Msamiati ulioibuliwa katika kamusi ya S.E.D ulifuatiliwa kwa makini ili upate kutathminiwa iwapo ulijitokeza katika matumizi ya kisasa. Hakukuwa na jaribio la kurejelea machapisho mengine ya *Sheng'* kwa sababu lengo la utafiti lilikuwa kubaini mchango wa leksimu unaotokana na S.E.D kwenye Kiswahili Sanifu. Kwa hivyo mtafiti aliamini kuwa kamusi ya S.E.D. ingetoa data toshelevu ya kuchunguza.

Aina zote za maneno zilichunguzwa bila kujali kama ni nomino, vivumishi, vielezi na vitenzi. Uchunguzi huu ulijikita tu katika kutafiti muundo wa kifonolojia wa maneno jinsi ulivyodhihirika kimatumizi kutokana na athari za S.E.D. Hata hivyo, kubainisha kategoria ya maneno katika sampuli mahsusi kwa misingi ya semantiki kulitumika. Yamkini, huenda kulikuwa na maneno mapya katika Kiswahili sanifu ambayo chimbuko lake sio S.E.D.  Uchunguzi huu haukulenga maneno hayo ingawa umeyabainisha katika baadhi ya maelezo. Kadhalika, maneno katika S.E.D ambayo hayakujitokeza katika mawasiliano ya kisasa ya Kiswahili sanifu yalichukuliwa kuwa

hayana athari kwa Kiswahili. Kwa hivyo, yalipuuzwa na sababu za kutojitokeza kwake kuelezwa. Sababu za utofauti wa kimuundo kwa matumizi ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu zilijadiliwa. Kulikuwa na umuhimu wa kufanya hivyo ili kubaini hatua za mabadiliko hayo tukirejelea uwezekano wa leksemu za S.E.D kuchipuka katika Kiswahili sanifu. Utafiti huu haukuchunguza matumizi ya *Sheng'* nyanjani bali ulijikta katika machapisho mbalimbali. Msingi wa machapisho hayo ulikuwa katika kamusi za Kiswahili sanifu. Kamusi hizo ni: *Kamusi Teule ya Kiswahili* (2013) na *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (2016). Iliaminika kuwa data inayojitokeza katika machapisho hayo ni toshelevu katika kuchanganua malengo ya utafiti huu.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Katika sehemu hii, mtafiti alijikita katika kutalii waandishi ambao walichangia pakubwa katika kueleza chimbuko la *Sheng'*, ukuaji wake, na muundo wa kifonolojia wa leksimu zake. Kadhalika, mtafiti aliweza kutalii wachunguzi waliohusika na sifa bainifu za leksimu za *Sheng'*. Utaratibu wa uchunguzi huu umechukua mwelekeo wa kimatukio. Waandishi walioshughulikia kipengele chenye sifa moja bainifu kuhusu *Sheng'* wamejadiliwa kwa pamoja. Hali hii yamkinika, itamrahisishia msomaji kuelewa vipengele mbalimbali vya *Sheng'* kiutaratibu hatua kwa hatua.

Utafiti ulianza kwa kerejelea waandishi wa awali kabla ya kuegemea waandishi wa hivi karibuni. Tafiti nyingi zimefanywa kutathmini ukuaji wa lugha na sababu za ukuaji wake. Hata hivyo, tafiti hizi hazijachunguza kwa kina chapisho la Mbaabu na Kipande (2003) la S.E.D jinsi chapisho hilo lilivyoathiri Kiswahili sanifu. Bwenge (1995) anasema kuwa, faida ya kamusi ni kutoa taarifa muhimu kuhusu lugha au

msamiati wa lugha tayari katika mpangilio maalum. Mabadiliko katika lugha huwa si makubwa wala ya haraka sana kusababisha kamusi iliyotangulia kutupiliwa mbali. Kwa msingi huo, chapisho la S.E.D lilifaa kuchunguzwa ili kutathmini athari zake kwa Kiswahili sanifu. Msimbo wa *Sheng'* awali ulichukuliwa kama waweza kuwa tishio kwa Kiswahili sanifu, (Chimera 2000). Hili ni jambo lililofaa kuchunguzwa hasa baada ya chapisho la S.E.D.

Lugha yaweza kuimarika au kupungua kwa matumizi kutegemea mwelekeo wa wazungumzaji wake. Uchunguzi huu ulikusudia kubainisha athari za *Sheng'* kwa KS kifonolojia kwa kuonyesha iwapo baadhi ya maneno ya S.E.D yalijitokeza katika KS na ikiwa kujitokeza huku kunaweza kuchangia kupungua kwa matumizi ya maneno ya KS kimatumizi. Iliaminika kuwa uchunguzi wa leksimu katika S.E.D ungetoa mwanya wa kukadiria kiwango cha kuathirika huku kwa KS. Wairungu (2010), ana mtazamo kuwa kuwepo kwa kamusi katika lugha fulani huipa hiyo lugha uhalali wa ukuaji. Sababu kuu ni kuwa, taasisi nyingi za elimu kama shule hutathmini sana lugha iliyoandikwa kuliko inayozungumzwa. Njia hakika ya kuchunguza ukuaji ama kupungua kwa matumizi ya maneno katika lugha ni kutathmini kamusi zilizochapishwa katika lugha husika. Jambo hili ndilo lililotupa mshawasha wa kuchunguza athari za S.E.D kwa KS.

Michieka (2012), alifanya uchunguzi kuhusu matumizi ya lugha mbalimbali katika mawasiliano ya simu miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Kulingana na uchunguzi huo wa Michieka (2012), ni kweli kuwa umaarufu wa msimbo wa *Sheng'* miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu ni kubwa sana.  Alibaini asilimia 17.1 ya

wanafunzi wanaotumia *Sheng'*, ikilinganishwa na wanaotumia Kiswahili sanifu ambayo ilikuwa asilimia 2.1. Hali hii ilitoa msukumo wa kuchunguza iwapo ukuaji wa *Sheng'* uliweza kuathiri KS kifonolojia.

Kihara (2006) alichambua matini ili kubaini matumizi ya lugha katika sajili ya matatu. Alichunguza namna lugha inavyotumika katika vituo vya magari na vile vile barabarani katika sekta ya uchukuzi. Baadhi ya data ambazo alichambua ni namna sajili hii ya matatu inavyotumia msimbo maalum katika mawasiliano. Alibaini aina mbili za msimbo katika sajili hii: msimbo wa maana dhanishi na msimbo wa maana dhahiri. Katika msimbo wa maana dhanishi, maneno yanapata maana mpya tofauti na yalivyo katika lugha changizi. Neno *kunyonga* la KS lilipewa maana mpya ya *kusitisha safari*. Neno hili katika KS humaanisha *kuua kwa kukaba koo*. Kadhalika, neno *toa* ambalo kawaida humaanisha *ondoa* lilipata maana nyingine tofauti ya *kushukisha kwa abiria*. Kihara (2006) alizidi kutoa mifano zaidi ya maneno mengine kama *kanyanga* na *zuia* ambayo vile vile huchukua maana mpya katika sajili ya uchukuzi wa matatu. Uchunguzi huu ulifaidi utafiti huu kwa sababu data ya maneno yaliyochunguzwa katika utafiti wake ni yale pia yaliyojitokeza katika msimbo wa *Sheng'*. Hata hivyo, kulikuwa na haja ya kuthibitisha iwapo maneno hayo yalichangia kutupilia mbali au kupungua kwa matumizi ya leksimu za KS katika sajili ya matatu. Katika msimbo wa maana dhahiri, Kihara (2006) alibaini namna wahudumu wa matatu hutumia msamiati maalum kuelezea maana ya vitu dhahiri na mahali mahsusi pa kazi.

Maneno ya kawaida kama vile *hewa* yanapewa maana ya *muziki* ilhali katika KS hewa ni *upepo*. Neno *gate* la Kiingereza linapata maana mpya ya *mlango wa gari* na wala

sio *lango la kuingia katika boma*. Kadhalika, neno *nganya* lamaanisha *matatu maridadi* na *rwambi* ni *sarafu ya shilingi mia mbili.* Haya ni baadhi ya maneno ambayo yalihitaji kuchunguzwa iwapo matumizi yake yaweza kuchangia katika kupungua kwa matumizi ya KS.

### 1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu ukuaji wa *Sheng'*

Katika sehemu hii mtafiti alijikita kurejelea maoni ya wataalam mbalimbali jinsi walivyo husika kueleza dhana tofauti kuhusu msimbo wa *Sheng'*. Wale waliozungumzia kuhusu swala fulani na kuwa na maoni ya pamoja, madai yao yamejadiliwa kwa pamoja bila kujali nyakati zao za uchunguzi. Mtafiti alifanya hivyo ili kurahisha utiririko wa mawazo na kumfanya msomaji kuwa na uelewa zaidi kuhusu vipengele mbalimbali vinavyochangia ukuaji wa msimbo wa *Sheng'*

Iraki (2004), alifafanua *Sheng'* kama mfumo wa lugha ya Kiswahili ambao huzungumzwa na vijana katika mitaa ya mabanda ya Nairobi. Maelezo haya yanawiana na Chimera (2000), Mbaabu na Kipande (2003), Githinji (2006), Ogechi (2005), Ferrari (2014) na Githiora (2018). Hata hivyo, aonya kuwa si rahisi kubaini wakati mahsusi wa chimbuko lake lakini kuna makisio kuwa huenda *Sheng'* ilizuka mnamo miaka ya 1960. Ogechi (2005) naye anaona kuwa, msimbo wa *Sheng'* ulizuka miaka ya 1970.

Iraki (2004) anazidi kueleza sifa bainifu za msimbo wa *Sheng*. Kwanza, *Sheng'* hukua kwa kukopa maneno mengi kutoka kwa lugha ya Kiingereza, KS na lugha za kienyeji nchini Kenya. Baada ya kuyakopa maneno, muundo wa maneno hubadilika ili kuafiki

taratibu za sauti na muundo wa silabi za *Sheng'*. Kauli hii iliungwa mkono na Ogechi (2005) anayesema kuwa, maumbo mengi ya mofimu za *Sheng'* huchukua muundo wa KS na msamiati wake huendelea kubadilika badilika. Kigezo hiki ndicho kilichovutia utafiti huu kutathmini namna maneno hubadilika kifonolojia na iwapo kulikuwa na uwezekano wa kuathiri KS.

Iraki (2004) anaendelea kueleza kuwa, vidahizo vya kileksia vya lugha huwa na uwezo wa kukua ama kupungua kwa matumizi baada ya matumizi ya muda fulani. Anakadiria kuwa, leksimu za *Sheng'* huweza kubadilika baada ya muda wa miaka mitano. Kwa mfano, neno linalorejelea noti ya shilingi 100 lilianza na *hando* (miaka ya 70), *masai* (miaka ya 80), *red* (miaka ya 90) na hatimaye *soo* la nyakati za sasa. Nalo neno *kula* likabadilika kwa kuanzia *minya*, *dishi* na baadaye *dema*.

Maelezo ya Ogechi (2005) yanaafikiana na haya ya Iraki (2004). Ogechi (2005) na Githiora (2002) wanahoji kuwa, *Sheng'* hupata leksimu zake kutoka kwa aina tofauti za lugha. Leksimu hizi zinapokopwa hubadilishwa ili kuwiana na muundo wa kipekee wa *Sheng'*. Sifa hii ya kubadilika kwa maneno ya *Sheng'* kulishawishi uchunguzi zaidi ili kubaini hatua za kubadilika huku. Mbaabu na Kipande (2003) wanasistiza hoja hii kwa kueleza kuwa, leksimu za *Sheng'* hubadilika ili kuficha siri. Sifa hii ya kubadilika kwa leksimu za *Sheng'* iliupa utafiti huu msukumo wa kufanya uchunguzi ili kubainisha iwapo mabadiliko haya huathiri KS.

Maelezo ya Iraki (2004) yanatoa muhtasari wa sifa bainifu za *Sheng'*. Kwanza, kuna maneno ambayo hufupishwa kwa kudondosha baadhi ya silabi. Anatoa mfano wa maneno kama: *Basketball* (mpira wa vikapu). Neno hili linabadilika na kuwa *bake*, *zamani* (kitambo) linakuwa *zamo* na *barabara* (njia kuu) linakuwa *baro*. Aidha, muundo wa *Sheng'* wa ngeli si kamilifu, dai linalopingwa na Bosire (2014). Hii ni kwa sababu *Sheng'* huegemea zaidi muundo wa neno kama ilivyo kutoka lugha iliyokopwa. Kwa mfano, kiambishi cha hali timilifu #***me***# hudondoshwa na #***sha***# hutumika kama kiambishi mbadala. *A**me**kuja* – *A**sha**kuja*. Hali hii hutokea ili kurahisha mawasiliano. Maelezo haya ya Iraki (2004) yalitupa mwanya wa kutathmini namna muundo wa maneno ya *Sheng'* ulivyojitokeza kifonolojia. Kadhalika, ilifaa kuchunguza iwapo miundo hii ya maneno ya *Sheng'* yanaweza kupenyeka katika KS. Maelezo haya yalifaa utafiti huu kwa sababu yalitumika kama kiunzi cha uchanganuzi wa fonolojia ya *Sheng'*.

Githinji (2006) aliangazia namna wazungumzaji wa *Sheng'* kutoka jamii tofauti huathiriana katika mawasiliano. Licha ya kuwa makundi haya huwa na lugha zao asili tofauti, mwingiliano huu huendelea kuzua lugha ya kuwajumuisha pamoja. Lugha hiyo kwa muktadha huu ni *Sheng'*. Vijana hutumia msimbo wa *Sheng'* ili kujitambulisha. Wageni wanaojiunga na kundi la vijana walio ndani hujibidiisha kumilisi msimbo wa *Sheng'* ili wapate kutambulika kundini. Kwa mujibu wa maelezo yake, *Sheng'* ni lugha ya utambuzi miongoni mwa vijana. Uchunguzi wa Githinji (2006) unatoa msisitizo kuwa, vijana hujitahidi kutumia *Sheng'* hali ambayo yaweza kuchangia kupungua kwa

matumizi ya leksimu za KS. Dhana hii ndio ilifaa kuchunguzwa kupitia kwa utafiti huu.

Kihara na Schröder (2012) walifanya uchunguzi kuhusu namna tanzu ya *Mchongoano* hutumia *Sheng'* kufanikisha mawasiliano. Walifafanua mchongoano kama usemi unaotumia mchezo wa maneno kuzua utani kwa kundi pinzani, familia, marafiki au hadhira maalum. Utanzu huu ni maarufu sana miongoni mwa vijana na lugha inayotumika pakubwa ni *Sheng'*. Lugha hii hufumbwa kwa namna ya kipekee kwa kutumia chuku, isitiara au kinaya ili kuzua utani unaoweza kusisimua au kuchekesha hadhira. Licha ya kuwa uchunguzi wao ulijikita tu katika namna lugha inavyotumika kuzua utani, matumizi mapana ya leksimu za *Sheng'* katika mchongoano yanadhihirisha namna *Sheng'* inavyozidi kuimarika. Mifano ya maneno yaliyojitokeza ni kama; *fala* (mjinga), *ulinishow* (uliniambia), *jam* (msongamano wa magari barabarani) na *mgreedy* (mlafi). Huenda matumizi mapana ya leksimu za *Sheng'* yalichangia kupungua kwa matumizi ya KS katika tanzu ya *mchongoano*.

Bosire (2014) alieleza *Sheng'* kama mfumo wa lugha ambao umezuka na kuimarika. Kuimarika huku kunafanya *Sheng'* kutumiwa kama lugha ya kwanza miongoni mwa vijana wa mijini nchini Kenya. Hata katika sehemu za mashambani, vijana wengi pamoja na idadi kiasi ya watu wazima, hutumia *Sheng'* katika mawasiliano. Vyombo vya habari havijaachwa nyuma. Hali hii inazua haja ya kuchunguza iwapo umaarufu wa *Sheng'* unapunguza matumizi ya baadhi ya leksimu za KS. Bosire (2006) anaeleza namna *Sheng'* hutumika pakubwa katika vyombo vya habari. Hadhira lengwa kwa

vyombo hivi vya habari huwa vijana. Matumizi haya mapana ya *Sheng'* katika vyombo vya habari huenda yalichangia kupungua kwa matumizi ya KS.

Bosire (2006) alihusika zaidi kueleza kwa kina ukuaji wa *Sheng'* kihistoria na kijamii, na vile vile miundo ya kifonolojia na kimofolojia ya *Sheng'* kwa upana. Anaeleza namna ukuaji wa *Sheng'* waweza kuwa ulitokana na harakati za ukoloni. Inadaiwa kuwa Waafrika waliohusika katika ujenzi wa reli kutoka Mombasa hadi Uganda katika maeneo ya Jinja, walikuwa na lugha zao za asili. Mazungumzo kati ya haya makundi yakawa kizungumkuti. Ikabidi lugha nyepesi iteuliwe kuafiki majukumu ya kimawasiliano kati ya makundi haya. Huu ndio mwanzo wa kuzuka kwa *Sheng'* kama pijini na hatimaye ikawa kirioli. Hata hivyo, Bosire (2006) anapinga dhana kuwa *Sheng'* ni pijini au kirioli. *Sheng'* ilizuka baada ya kuwepo kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza. Aidha, madai kuwa *Sheng'* ni kirioli hayana mashiko. Kirioli ni pijini iliyoimarika kwa kupata wazawa wake. Vijana wanaotumia *Sheng'* tayari wana lugha zao za kienyeji au wengi wana umilisi mpana wa lugha za Kiswahili sanifu na Kiingereza. Bosire (2006) alihitimisha kuwa *Sheng'* ni msimbo wa lugha ambao ni badilifu. Muundo wake wa leksimu licha ya kuwa una uwiano na KS, huendelea kuimarika na kubadilika. Hali hii hutokea kwa kuchanganya lugha za Kiingereza, Kiswahili na lugha za Kiafrika kuelezea dhana mbalimbali.

Kando na *Sheng'*, kuna misimbo mingine ya lugha katika sehemu zingine za bara la Afrika ambazo zina sifa sawia na *Sheng'*. Kuna *Lingala* katika Zaire, *Sango* katika Afrika ya Kati, *Indoubil* katika Afrika ya Kusini (Bosire 2006). Dhana kuwa muundo

wa *Sheng'* unazidi kukua na kuimarika inahalalisha utafiti huu kuchunguza ikiwa kukua huku kunaathiri KS. Bosire (2006) azidi kueleza kuwa, sifa kuu bainifu ya misimbo hii ya lugha ni kuwa zote zilizalika kutoka mabanda ya miji yenye vijana walio na sifa za ujangili. Lugha hizi zilizuka mijini baada ya jamii kusheheni mabadiliko ya kijamii na kisiasa baada ya uhuru. Mtagusano huu ndio uliozua haja ya jamii nyingi za kimji kubuni lugha ya kisasa inayoweza kuhalisi hali hii. Vijana walijipata katika mtanziko wa aina mbili. Ulimwengu wa zamani uliosheni tamaduni za Kiafrika na ulimwengu wa sasa.

Ikabidi pawe na haja ya kubuni msimbo mpya wa lugha ambao unaweza kuafiki matakwa ya kisasa ya ubunifu, ukengeushi, ujasiri na ufahamu mpana wa matukio ya kisasa. Msimbo wa lugha ulio na uwezo wa kusetiri hali hii ukawa ni *Sheng'*. Matumizi mapana ya *Sheng'* miongoni mwa vijana katika maeneo hayo yaweza kuathiri KS. Ikabidi utafiti huu ufanywe ili kuchugnguza ikiwa kuna athari zozote kwa KS. Utafiti wake Bosire (2006), ulitufaidi zaidi kwa kueleza namna *Sheng'* ilivyokua na miundo yake changamano ya kifonolojia na kimofolojia. Uchangamano huu ulitokana na dhana kuwa ukuaji wa *Sheng'* ulitokana na ukopaji wa leksimu kutoka kwa aina nyingi za lugha za kienyeji pamoja na Kiingereza. Lugha hizi kimsingi huwa na miundo tofauti ya lugha. Ingawa Bosire (2006) aliweza kueleza ukuaji wa *Sheng'* kihistoria, na miundo yake ya kifonolojia na kisemantiki, kulikuwa na haja ya utafiti zaidi kufanywa kuhusu leksimu mahsusi za S.E.D zinavyoweza kuathiri ukuaji ama kupungua kwa matumizi ya leksimu za KS.

Utafiti wa Kihara (2016) ulihusu matumizi ya *Sheng'* katika biashara ya matatu nchini Kenya. Utafiti huo ulizama zaidi kueleza namna *Sheng'* inavyounda leksimu zake. Dhana hii ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa iliweza kutoa mchango kwa kueleza namna leksimu za *Sheng'* zilivyoundwa ambapo miundo ya fonolojia ya *Sheng'* bila shaka ilijitokeza. Aidha, Kihara (2016) alitathmini namna leksimu za *Sheng'* zinavyonasibishwa na kuunda msamiati katika taasisi za uchukuzi wa matatu.

Alidhamiria kubaini namna leksimu hizi zinavyonasibishwa au kutupilia mbali katika sekta ya matatu. Alifafanua jinsi mbinu ya uchopekaji hutumika. Kihara (2006) alitoa mfano wa neno la *Sheng' roundaa*. Neno hili ni utohozi wa neno la Kiingereza *round-about* ambalo limefupishwa na kisha kuchukua viambishi tamati /***aa/***. Maneno mengine ya *Sheng'* yaliyobainika katika uchunguzi huu ni kama *mamii* (mama), *antii* (shangazi) lakini katika *Sheng'* likawa ni *dada*. Mifano zaidi inadokezwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 1: Msamiati katika sajili ya matatu: Kihara (2006)**

| **Data** | **Maana** |
|---|---|
| Wadhii | Wasafiri. |
| Tao | Mji. |
| Chapaa | Pesa |
| Selasa | Thelathini |
| Mbao | Shilingi ishirini. |
| Kidy | Shilingi kumi. |
| Kondaa | Kondakta. |
| Deree | Dereva. |
| Kalao | Polisi. |
| Dubai, soo | Sarafu mpya, mia moja. |
| Mosmos | Polepole |
| Nganya | Matatu yenye maridadi |

Uchunguzi huu wa Kihara (2006) ulifaa katika utafiti huu. Kunasibishwa huku kwa msamiati wa *Sheng'* katika uchukuzi wa matatu huenda kulichangia katika kupungua kwa matumizi ya KS miongoni mwa washikadau wa sekta ya matatu. Wakahiari kutumia msamiati wa *Sheng'* badala ya msamiati wa KS. Hata hivyo, utafiti huo haukuangazia S.E.D na kueleza namna inavyoweza kuathiri sekta ya matatu.

Mwangi na Mukhwana (2011), waona *Sheng'* kama lugha ya msimbo au kipindi. Mwelekeo wao ulikisia *Sheng'* kuwa pijini. Iwapo *Sheng'* yaweza kuchukuliwa kama pijini basi uchunguzi wao ungechukua mwelekeo wa Romaine (1994) aliyegawa Pijini katika hatua mbalimbali za ukuaji. Kulingana na Romaine (1994), lugha ya pijini huwa na hatua kuu muhimu za ukuaji tangu kuwa lugha sahili hadi lugha komavu. Aona lugha kama mfumo wa tabia zinazorithishwa kutoka lugha zalishi hadi lugha zaliwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Lugha ya kawaida huwa inapokezwa kupitia kwa watoto wa jamii husika wanaoitumia kama lugha ya kwanza. Kudumu kwa lugha hutegemea jinsi lugha hiyo inavyozidi kutumika na wazawa wa lugha.

Mtazamo huu huenda ukawa mwafaka katika uchunguzi wa *Sheng'*. Ukuaji wa *Sheng'* na umaarufu wake waweza kuwa ni kwa sababu ya kupata wazawa wake. Ukuaji huu wa *Sheng'* ndio ulioupa utafiti huu msukumo wa kutaka kubaini iwapo unachangia katik kupungua kwa matumizi ya KS.

Romaine (1994), aorodhesha vipindi vifuatavyo vya ukuaji wa lugha: Kwanza kuna kipindi cha mtagusano hafifu. Huu ni wakati ambapo lugha ya pijini imeanza kuzalika kutoka kwa mgongano kati ya lugha mbili au zaidi. Mgongano huo huzalisha lugha ya tatu yenye maneno sahili. Sarufi yake ni chapwa na haina uchangamano wa kisarufi. Matumizi yake huwa katika mazingira finyu mahsusi kama vile mahali pa biashara, na kuelekeza wafanyikazi viwandani. Huenda hii ikawa hatua ya kwanza ya matumizi ya *Sheng'* jijini Nairobi kama alivyodokeza Chimera (2000). Madai haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwani yaliweka wazi hatua mbalimbali ambazo *Sheng'* inapitia katika ukuaji wake. Dhana kuwa *Sheng'* hutumika katika mazingira finyu huenda yasiwe na mashiko. Hii ni kwa sababu chapisho la S.E.D ni thibitisho tosha kuwa *Sheng'* imeendelea kukua hadi kupata nafasi katika machapisho ya kisasa. Ukuaji huu ulifaa kuchunguzwa namna unavyoathiri KS.

Kipindi cha pili kwa mujibu wa Romaine (1994), ni kipindi cha umilisi wa lugha. Lugha huwa na sentensi sahili na sentensi chache changamano lakini hutumika tu kwa ajili ya uhusiano wa kijamii na kutafuta maafikiano katika mawasiliano. Kwa hivyo, hutumika tu katika muktadha binafsi wa mtu na hudhamiria kutafuta uthibiti wa kijamii miongoni mwa watu wanaoitumia. Romaine (1994), anatoa mfano wa lugha ya Russenorsk (Russo- Norwegian). Hii ni pijini iliyokuwa ikitumika kati ya

wafanyibiashara wa Kirusi na wavuvi kutoka Norway. Dhana hii inaweza kuafiki *Sheng'* kwa sababu matumizi yake hualisi miktadha ya kibinafsi ya wahusika. Hata hivyo uimarikaji wa *Sheng'* ya kisasa umepita kiwango hiki cha matumizi. Kuwepo kwa kamusi ya *Sheng'* na matumizi katika vyombo vya habari ni dhihirisho tosha kuwa dai hili la Romaine (1994) laweza kupuuzwa.

Kipindi cha tatu cha ukuaji wa lugha ni kipindi cha pijini sambazwa. Lugha huanza kuwa na sarufi changamano, na kuwa na muundo maalum wa kuzalisha msamiati mpya. Watumizi huanza kuwasiliana kwa mwendo wa kasi kuliko ilivyokuwa awali. Kigezo hiki chaweza kuafiki msimbo wa *Sheng'* kwa namna ilivyokua. Inaonyesha jinsi *Sheng'* inavyokuwa na sarufi changamano na kuwa na uwezo wa kuzalisha misamiati tofauti ya kuafiki hali tofauti. Maelezo haya yaliweza kunufaisha utafiti huu kwa kuonyesha hatua mbalimbali za ukuaji wa lugha. Lugha huanza kutumika katika hali zote za maisha, kujieleza, katika mchezo wa maneno, machapisho na huwa kiungo muhimu cha utangamano kati ya jamii mbalimbali. Mfano mzuri ni pijini inayotumika katika nchi za Afrika magharibi. Dhana hii huenda ikaafiki *Sheng'* ambayo kuna chapisho la kamusi, hutumika na baadhi ya vituo vya redio kama vile kituo cha Redio cha Ghetto (Githiora, 2018). Matumizi haya mapana huenda yaliathiri KS kwa kuchangia katika kupungua kwa matumizi ya baadhi ya leksimu. Hata hivyo, haya ni maelezo yaliyopingwa vikali kupitia kwa uchunguzi wa Bosire (2006) kama ilivyoangaziwa pale juu.

Githiora (2018) adai kuwa *Sheng'* sio Kirioli wala Pijini. Sarufi ya *Sheng'* ina uwiano mkubwa sana na sarufi ya KS. *Sheng'* haionyeshi kiwango sahili au duni cha kisarufi kama ilivyo katika Kirioli na Pijini. Pijini huzalika ili kutosheleza majukumu machache ya mawasiliano miongoni mwa watu ambao hawana lugha moja ya kuwaunganisha. Wazungumzaji wa *Sheng'* tayari wana lugha zao asili. Ni kwa ajili ya umaarufu huu wa *Sheng'* ndipo kulikuwa na haja kutathmini iwapo *Sheng'* ni tishio kwa KS. Pijini haina wazawa wake. Huwa ni lugha ya msimu na ambayo huenda ikatoweka ikiwa mazingira ya uzalishaji wake yatabadilika. *Sheng'* haikuzalika ili kutosheleza majukumu au pengo la mawasiliano miongoni mwa wakaaji wa Nairobi. Wakaaji wa Nairobi walikuwa na lugha zao za asili, Kiingereza na KS. Kadhalika, matumizi ya *Sheng'* hayajaonyesha uwezekano wa kupungua kwa matumizi hivi karibuni.

Ferrari (2014) anapinga dhana kuwa *Sheng'* yaweza kuwa Pijini. Anaona *Sheng'* kuwa lugha ya kimji iliyopata udhabiti mkubwa kwa kuwa na mfumo mahsusi wa kimofolojia na kisintaksia. Apendekeza *Sheng'* kujumuishwa kuwa kiwango sawa na lugha za kienyeji. Udhabiti huo ulidhihirika wazi kupitia kwa utafiti huu kwa kuchunguza jinsi *Sheng'* ilivyoathiri KS. Hata hivyo, wataalam hawa hawakuchunguza chapisho la S.E.D.

Chimera (2000) aliona kuwa, ukuaji wa *Sheng'* waweza kuwa tishio katika mfumo rasmi wa Kiswahili sanifu. Kwa wakati huo (mwaka wa 2000), Chimera aliona *Sheng'* kama Pijini ya Kiswahili ambayo ni tishio kwa KS jijini Nairobi. Hakujua kuwa

msimbo huu ungekuja kusambaa kote nchini miongoni mwa vijana. Chimera (2000) na Mbaabu na Kipande (2003) wanaamini kuwa neno *Sheng'* latokana na maneno mawili ya Swahili na English. Viambishi ***sh*** na ***eng*** vikaungwa pamoja na kuunda neno *Sheng'*. Licha ya kuwa *Sheng'* ina mfumo wa kisarufi unaofanana na wa Kiswahili, Chimera (2000) amebaini kuwa idadi ya maneno yaliyokopwa kutoka Kiingereza yanakaribia kiwango sawa na Kiswahili. Kuna baadhi ya maneno mengine ambayo yamekopwa kutoka lugha zingine kama vile Kiluhya, Gikuyu, Kamba na Kiluo (Githiora 2018). Hata hivyo, maneno mkopo hutamkwa visivyo kiasi kwamba si bayana kubainisha usuli wake. Ukopaji huu wa maneno huenda ukapenyezwa pakubwa katika KS na kwa hivyo kufanya baadhi ya leksimu za KS kupungua kimatumizi au kutupiliwa mbali.

Hali kadhalika, muktadha wa baadhi ya maneno ya *Sheng'* huzua maana mpya kinyume na maana asili katika lugha changizi. Mchango wa Chimera (2000) katika utafiti huu ni kuwa; alieleza usuli wa msamiati wa *Sheng'*. Kama kilivyo Kiswahili sanifu, *Sheng'* hupata msamiati wake kupitia kwa utohozi na ukopaji wa maneno kutoka lugha zingine. Yamkini maneno haya huathirika kifonolojia kabla ya kukubaliwa katika lugha pokezi. Hili ndilo swala lililofaa kuchunguzwa kwa kuangazia namna maneno yaliyo kwenye S.E.D yalivyoathirika kifonolojia yakiingizwa katika KS.

Vyombo vya habari pia vimechangia pakubwa katika maenezi ya *Sheng'*. Baadhi ya vipindi kwenye redio na runinga vinatumia msimbo wa *Sheng'* hali inayochangia

maenezi yake miongoni mwa vijana. Kivutio kikubwa kinachoonekana kusisimua vijana kutumia *Sheng'* ni kuzuka kwa miziki ya kizazi kipya aina ya mafoka (*Swahili Rap Music*), ambayo wasanii wake hutumia lugha hii katika nyimbo zao. Hata katika ulingo wa kisiasa, nyimbo hizi zimesikika zikichezwa katika shughuli za kampeni na wanasiasa ili kuwavutia na kuwasisimua vijana. Mazingira kama haya yamefanya baadhi ya watu waliokuwa na mtizamo hasi kuihusu *Sheng'* kuanza kuichangamkia.

Utafiti huu ulilenga kutathmini hali hiyo kwa kubaini kiwango cha athari ya lugha hii katika lugha sanifu ya Kiswahili kwa kujikita katika chapisho la S.E.D. Madai haya yanaungwa mkono na Githiora (2018). Chombo cha habari kinachovuma nchini Kenya kwa upeperushaji wa matangazo katika *Sheng'* ni kituo cha redio cha Ghetto Fm. Hii ni idhaa ya redio iliyozinduliwa mwaka wa 2007. Kusudi la kituo hiki ni kuafiki na kudhihirisha ukwasi mkubwa wa maisha na tabia za vijana katika sehemu za mabanda jijini Nairobi. Licha ya kupasha habari na burudani kwa vijana, kituo hiki pia hupeperusha matangazo ya biashara katika msimbo wa *Sheng'*. Umaarufu wa matumizi ya *Sheng'* katika vipindi hivi yaliupa utafiti huu mshawasha wa kufanya uchunguzi ili kutathmini ikiwa unachangia katika kupungua kwa matumizi ya leksimu za KS.

Madai ya Mwangi na Mukhwana (2011) kuwa *Sheng'* ni lugha ya mpito yalifaa kuchunguzwa. Kulingana nao, hii ni lugha ya msimu au mpito kwa kuwa haidumu. Ni lugha ambayo msamiati wake hupungua kimatumizi namna kipindi au misimu inavyobadilika kiwakati. Wanathibitisha kwa kudai kuwa, msamiati wa *Sheng*'

huendelea kubadilika badilika. Wanatoa mfano wa neno *msichana*. Vijana walianza kutumia neno *manzi*, kisha *mshi, demu*, *chikidee*, *chile, msupuu* na hatimaye *chiki*. Mabadiliko haya ya maneno yalichunguzwa katika utafiti huu ili kuthibitisha iwapo yalijitokeza katika Kiswahili sanifu.

Mwangi na Mukhwana (2011) wanakubaliana na Muaka (2011) kuwa msimbo wa *Sheng'* ulizuka kutoka maeneo ya mashariki mwa Nairobi ukitumika miongoni mwa vijana na umesambaa kwa haraka hadi sehemu zingine za nchi. Watu wa matabaka mbalimbali wanatumia *Sheng'*, hutumika kwenye magari ya umma na hata katika vyombo vya habari. Matumizi haya yamefanya *Sheng'* kupata umaarufu mkubwa sana miongoni mwa vijana. Matangazo ya biashara ya kuwahimiza vijana kutahadhari na ugonjwa wa ukimwi, msimbo wa *Sheng'* ulitumika. Maneno kama *kuchill* na *tuliza boli* ni ya asili ya *Sheng'*. Ni jukumu la utafiti huu kuthibitisha iwapo matumizi haya yanaathiri KS. Msimbo huu wa lugha ya Kiswahili, unavuma sana sio tu kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa vijana, bali pia katika kufahamisha, kuelimisha na kuburudisha kiasi cha kutumika katika redio na runinga. Hali hii husababisha utangamano na kujitambulisha miongoni mwa vijana.

Kwa hivyo, dai la Mwangi na Mukhwana (2011) kuwa *Sheng'* inaupa uhai msamiati wa Kiswahili sanifu na kubuni maana mpya lilichunguzwa katika utafiti huu. Huenda uundaji huu wa msamiati huzua maneno mbadala ya matumizi katika mawasiliano. Hali hii yaweza kuchangia kutupiliwa mbali au kupuuza matumizi ya msamiati wa KS. Wanatoa mfano wa neno '*sasa'* na '*poa'* katika salamu. Maneno haya yanapewa

maana mpya kinyume na yalivyo katika Kiswahili sanifu. Kuzuka kwa maneno mbadala kama haya katika mazungumzo ndiyo yaliyochochea utafiti huu kujaribu kubaini iwapo kuzuka kwa maneno mengi mapya katika *Sheng'* yanaweza kuchangia katika kupungua kwa matumizi ya msamiati katika KS.

*Sheng'* pia husababisha kutoelewana kati ya vijana wenyewe, kati ya wanafunzi na walimu, na kati ya watoto na wazazi. Hii ni kwa sababu kila kuchao, kuna msamiati mpya ambao huibuliwa. Kigezo hiki ndicho hufanya *Sheng'* kuwa na usiri mkubwa sana (Mwangi na Mukhwana, 2011). Kadhalika, kuna dhana kuwa vijana wanaotumia *Sheng'*, hudharauliwa na makundi mengine ya watu.

Huenda dhana hii ikawa kweli kwa sababu chimbuko la *Sheng'* ni mitaa ya mabanda Nairobi yenye wakaazi wahuni, walevi, utingo wa magari ambao husheheni fujo nyingi. Kutoelewana huku huenda ni kwa sababu ya vijana kumilisi na kuanza kutumia msamiati mbadala wa *Sheng'* badala ya KS. Uzoefu mwingi wa matumizi ya maneno kuwasilisha dhana fulani huenda ukafanya watumizi kusahau au kutozingatia matumizi ya maneno halisi katika lugha asilia. Tishio hili lilifaa kuchunguzwa kubaini iwapo kuna upungufu wa matumizi ya maneno fulani kwa sababu ya mchipuko wa msamiati mpya wa *Sheng'*.

Licha ya wataalamu wengi kuwa na mtazamo hasi kuihusu *Sheng'*, huu msimbo unazidi kupata umaarufu. Ithibati zifuatazo zinadhihirisha dhana hii. Mwangi na Mukhwana (2011), walisistiza kuwa *Sheng'* ni lugha ya vijana na kwa sababu vijana ni

wengi, basi umaarufu wake utazidi kukua. Pili, msimbo huu una nafasi kubwa katika vyombo vya habari. Vipindi vingi vya redio na runinga vyatumia msimbo wa *Sheng'*. Katika kituo cha redio cha Ghetto FM, matangazo yote yanapeperushwa kwa kutumia msimbo wa *Sheng'*. Muziki wa kizazi kipya almaarufu *Bongo Fleva* unatumia *Sheng'*. Wasanii kama Nonini, Diamond, Alkiba na Chege hutumia *Sheng'* katika nyimbo zao. Itakumbukwa kuwa muziki ni njia bora na ya haraka sana ya kueneza lugha (Mbaabu, 1996).

Namna aina hizi za nyimbo zianvyopata umaarufu miongoni mwa vijana, ndivyo kunavyozuka hofu kuwa umaarufu huu waweza kuchangia kupungua kwa matumizi ya leksimu za KS. Mukhwana (2015) ana maoni ya kutia moyo kuhusu ukuaji wa *Sheng'*. Kulingana na utafiti wake, watu wazima walionekana kuwa na mtazamo hasi kuhusu matumizi ya *Sheng'*. Hata hivyo, anaona kuwa ukuaji wa *Sheng'* utaendelea kuimarika kwa misingi mitatu mikuu. Kwanza, *Sheng'* haiambatanishwi na kabila lolote kwa hivyo ni kiungo muhimu cha kuunganisha wananchi. Watu kutoka jamii na kabila tofauti hutumia *Sheng'* bila kujali tofauti zao. Pili, *Sheng'* huzuka na kuimarika bila kuwa na mpangilio wowote. Msamiati na sarufi yake huzuka tu kinasibu kuafiki matakwa ya kimuktadha ya watumizi. Hali hii ndio huvutia mno watumizi wengi wa *Sheng'* hata wale wasio na umilisi mwafaka wa sarufi ya KS. Tatu, licha ya kupigwa vita katika taasisi za elimu, msimbo wa *Sheng'* hutumiwa kama kiungo muhimu cha mawasiliano kati ya walimu na wanafunzi. Hali hii huenda ikachangia pakubwa kuenea kwa matumizi makubwa ya leksimu za *Sheng'* badala ya KS.

Kauli hizi zinaungwa mkono na Githiora (2018), ambaye anaona *Sheng'* kama matokeo ya mfumo wa kiisimu ambao unaonyesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyooendelea kukua na kubadilika. *Sheng'* haswa inahusishwa na kizazi kipya kinachoathiriwa na miingiliano au miigo ya tamaduni na tabia za watu weusi wanaoishi ughaibuni. Kadhalika, inahusishwa na jamii ya watu weusi wanaoishi nje ya bara la Afrika. Athari hizi hujitokeza katika mitandao ya kijamii, muziki wa mafoka (hip hop) na *reggae*.

Nchini Kenya, *Sheng'* imepata umaarufu kwa kujipenyeza katika vyombo vya habari, kampeni za kisiasa na matangazo ya biashara ya kampuni kubwa kubwa. Githiora (2018) anasistiza kuwa msimbo huu umekua kutoka kuwa lugha finyu na wa watu wachache na kuwa lugha kuu. Umesambaa nje ya mji wa Nairobi na kupata wafuasi wengi. Kadhalika, ni msimbo unaotishia kuwa kitambulisho cha kitaifa. Maoni haya ya Githiora (2018), yaliupa nguvu utafiti huu kwa kuweka wazi hoja kuwa *Sheng'* imepata umaarufu katika kizazi cha sasa. Kwa hivyo, kukawa na haja ya kubaini iwapo msimbo huu umepata nafasi katika Kiswahili sanifu na kutishia kupungua kwa matumizi ya leksimu za KS katika jamii.

Munuku (2005) katika tasnifu yake ya uzamili, alichunguza miundo ya lugha inavyofumbwa na kubadilika katika nyimbo za mafoka (rap). Uchunguzi wake ulitenga Kiswahili sanifu kama lugha kuu kwa upande mmoja huku Kiingereza na *Sheng'* zikawa lugha mbadala katika utafiti wake. Dhamira kuu ya uchunguzi wake

ilikuwa kubaini namna wasanii wa Mafoka wanavyochukua maneno ya kawaida ya KS na kuyafumba kwa kutumia *Sheng'*.

Umaarufu wa nyimbo hizi miongoni mwa vijana waweza kuwavutia ili kuanza kutumia maneno ya *Sheng'* badala ya KS katika mawasiliano yao. Hili ndilo jambo ambalo lilichunguzwa na utafiti huu ukiwa na kusudi la kubaini ikiwa leksimu za KS zilipungua kimatumizi na nafasi zake kuchukuliwa na *Sheng'*. Nyimbo hizi hutumia lugha ya mafumbo kutegemea hali ilivyo au kutegemea kigezo cha mofolojia. Kwa mfano, matini hubadilishwa na kuingizwa *Sheng'* ili kuficha dhana zinazotaja mambo kama askari, ngono na mapenzi. Matumizi haya huchukuliwa kama lugha ya tasfida kwa sababu makali ya lugha hufichwa kwa kutumia lugha ya upole.

Kwa mujibu wa Munuku (2005), vijana huwa na uwezo wa kuelewa maana iliyofumbwa katika lugha kwa kutumia tasfida. Vijana hutumia tasfida katika *Sheng'* kuwasilisha mambo ya kimapenzi kwa njia inayoeleweka miongoni mwao wazi. Katika KS neno *kuchumbiana* likitumika hadharani huweza kuibua uozo wa maadili miongoni mwa wazungumzaji. Lakini katika *Sheng'* neno *kukatiana* linatumika kwa maana ile ile kwa kuficha makali ya *kuchumbiana*. Hali hii hudhamiria kuwatenga watu wengine wa 'nje' kuelewa kilichokusudiwa. Hata hivyo, mazoea ya matumizi ya neno *kukatiana* huenda yakazoeleka na kisha yakachangia kupungua kwa matumizi ya neno *kuchumbiana*.

Mwihaki (2007) alieleza *Sheng'* kama mfumo mbadala wa isimu ya lugha ya Kiswahili. Alikuwa na dhana kuwa, wazungumzaji wa *Sheng'* huwa na umaarufu mkubwa kijamii unaowatenganisha na watu wengine wasiotumia *Sheng'*. Msimbo huu hutumiwa na vijana kujitambulisha kimakundi, kutafuta umaarufu wa kibinafsi na kuunda uhusiano. *Sheng'* hupendwa na vijana kwa sababu ni lugha legezi lakini kamilifu katika mawasiliano ya kibinafsi. Hali hii huchangia kuzuka kwa vikundi vidogo katika jamii pana kimawasiliano. Mwihaki (2007) anataja kigezo hiki kama lahaja ya kijamii. Matumizi haya mbadala ya lugha ndio huzua mianyo ya kuzuka vikundi vya kijamii. Maelezo haya ya Mwihaki (2007), yalichochea utafiti huu kuchunguza namna umaarufu wa *Sheng'* unavyoathiri KS.

Ogechi (2005) alichunguza namna leksimu za *Sheng'* huzuka na kuchukua maana mbalimbali. Licha ya kukubaliana na Iraki (2004) kuwa muundo wa maneno ya *Sheng'* huwiana na KS, anatofautiana naye kwa kudai kuwa kuna miundo mingine ya leksimu za *Sheng'* ambayo ni tofauti mno na KS. Aidha, miundo hiyo huwa geni sana na wakati mwingine huchangia katika kuibua kwa leksimu za *Sheng'*. Kutokana na madai haya, kutokea kwa miundo migeni ya leksimu za *Sheng'* hufanya watu kushindwa kufuatilia mawasiliano ya *Sheng'*. Hata kwa wale ambao wana umilisi mzuri wa KS hutatizika. Ogechi (2005) alibaini kuwa, kigezo cha kisaikolojia na kijamii huwa kichocheo kikuu katika muundo wa kileksia wa *Sheng'*. Kwa mfano neno *teke* humaanisha msichana mrembo katika *Sheng'*. Katika Kiswahili sanifu, *teke* humaanisha *pigo la mguu*. Matumizi haya yanatokana na taswira inayodhihirika kisaikolojia ya msichana mrembo kuwa na umbo la miguu na wala sio *kupiga mateke*.

Mfano huu unathibitisha dhana kuwa, matumizi ya *Sheng'* miongoni mwa vijana ni kwa sababu ya kujitambulisha na kujinasibisha katika makundi fulani. Kimsingi, vijana hawahitaji *Sheng'* katika mawasiliano kwa sababu wana uwezo wa kujieleza ipasavyo kupitia kwa Kiswahili sanifu, Kiingereza au kupitia kwa lugha za Kiafrika. Kwa mujibu wa maelezo haya, ni vyema kuelewa lugha pana ya Kiswahili, sifa zake na miundo yake kimatumizi kabla ya kujikita katika uchunguzi wa *Sheng'*.

Kulingana na (Echessa 1990, Chimera 1998, Ogechi 2005) *Sheng'* huchukuliwa kama mfumo tofauti wa lugha ya Kiswahili unaokopa maneno kutoka lugha za Kiafrika na za kigeni. Kwa hivyo, *Sheng'* ni jina linalotumiwa kuelezea msimbo tofauti wa lugha ya Kiswahili. Msimbo huu hufuata muundo wa kisarufi wa Kiswahili sanifu na lugha za kibantu, ambao huwiana vilivyo katika viwango vyote vya lugha: kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, na kisemantiki (Mwihaki 2007). Kwa hivyo, wataalamu hawa wanakubaliana kuwa *Sheng'* inazidi kukua na kuimarika miongoni mwa vijana.

Hali hii ndiyo iliyochangia kuwepo kwa msukumo wa kufanya utafiti kuhusu athari zake hasa kifonolojia kwa Kiswahili sanifu. Kamusi huwa chapisho mahsusi la kutathmini ukwasi wa lugha fulani (Muaka, 2011). Ikiwa kuna athari zozote kifonolojia kwa Kiswahili sanifu, yamkini athari hizi zitajitokeza katika kamusi. Kimsingi, *Sheng'* hutumika kuzua maana inayoafiki vijana. Huonekana kama chaguo asili la mawasiliano ya kujinasibisha kimakundi. Uamuzi wa kubadilisha mkondo wa mawasiliano hadi *Sheng'* na vijana, ni wa kimakusudi. Hudhamiria kutekeleza malengo fulani ya kimatumizi kijamii. Ni kupitia hali hii ndipo maneno ya mkopo

kutoka Kiswahili sanifu na lugha zingine hutoholewa ili kuafiki mfumo wa *Sheng'*. Kigezo hiki ndicho kilitupa msukumo wa kutathmini namna maneno haya ya mkopo hutoholewa hadi kuwa msamiati kubalifu katika msimbo wa *Sheng'* kupitia kwa nadharia ya Fonolojia Boreshi.

### 1.7.2 Uundaji wa maneno katika Sheng'

Warambo (2017) alieleza njia kadhaa za uundaji wa maneno katika msimbo wa *Sheng'*. Licha ya wataalamu kuona *Sheng'* kuwa lugha ya mpito, kuna ukweli kuwa muundo wake wa maneno una udhabiti.

**a) Utohozi**

Utohozi ni hali ambapo maneno au vishazi vya maneno hukopwa kutoka lugha moja hadi nyingine na kufinyangwa ili kuafiki muundo wa kisarufi wa lugha pokezi. Warambo (2017) alitoa mfano wa maneno kama *mwasi*- *msichana* kutoka kwa lugha ya Lingala; *buda* – *baba* kutoka kwa lugha ya Gujarati na *nyora-kojoa* kutoka kwa Kisii. Mbinu ya utohozi ilifaa sana katika utafiti huu kwa sababu kuna maneno mengi katika S.E.D ambayo msingi wake ni utohozi. Ukopaji huu pia umeungwa mkono na Mekonge (2016) aliyetoa mifano ifuatayo. *Masa*- *Mama* kutoka lugha ya Kiingereza, *fomu-mpango* kutoka Kiingereza na *githaa* - *wakati* kutoka lugha ya Kigikuyu. Githinji (2006) anatoa mfano wa *gothie-kuenda* ambalo limetoholewa kutoka kwa Gikuyu *g*û*thii*.

Echessa (1990) adokeza mfano wa neno *basi* kutoka kwa *bus* la Kiingereza. Katika utafiti huu maneno yaliyobainika kama ya utohozi ni kama *brandi* – mpya, *kampu* – kampuni; yote kutoka Kiingereza.

**b) Udondoshaji**

Ni hali ya kufupisha neno kwa kuondoa baadhi ya herufi au silabi. Udondoshaji huu waweza kutokea kwa viambishi awali au tamati. Warambo (2017) anatoa mfano wa neno la Kiingereza *Saturday* ambalo hudondoshwa katika *Sheng'* na kuwa *Sato*. Kauli hii iliungwa mkono na Iraki (2004), ambaye anatoa mifano ifuatayo: *basketball – bake, zamani – zamo, Nairobi – Nai, na safari – safo.* Mekonge (2016), anatoa mifano zaidi katika *Sheng'*: juu – *ju, hadi – adi, kama – ka, hiyo – io.* Naye Githinji (2006) alichangia *Dago – Dagoretti*.

**c) Unyambuaji**

Ni hali ya kuongeza viambishi kwenye mzizi wa neno ili kutoa maana tofauti. Viambishi hivi vyaweza kupachikwa mwanzoni au tamati mwa neno. Hata hivyo, meneno mengi ya *Sheng'* huchukua viambishi awali kwa wingi. Herufi ***/m/*** hutumika kama kiambishi awali kwa baadhi ya maneno yanayorejelea viumbe.

*Supa-* ***m****supa, shii-****m****shii, ngoso-* ***m****ngoso.* Iraki (2004) anaonyesha namna kiambishi awali ***ku*** hupachikwa kwa mizizi ya vitenzi baada ya kukopwa; ***ku****dedi*, ***ku****zubaa*, na ***ku****ng'etha*. Maoni haya yalifaa sana katika utafiti huu kwa sababu maneno kama; ***ku****jidu*, ***ku****jishoo*, na ***ku****jiseti* yanayojitokeza katika S.E.D yaliundwa kwa msingi huu.

**d) Uundaji upya wa maneno**

Ogechi (2005) anaeleza kuwa, uundaji upya wa maneno ni hali ambapo neno huundwa kidhahania bila kupata maana kutoka kwa neno lingine. Maneno haya huwa na maana mahsusi. Maneno kama *burungo* (vitu), *kerende* (umati wa watu), *nyagu* (nyama), *njeve* (baridi), *mboch* (yaya) na *rasa* (makalio) yaliundwa kupitia mbinu hii. Mifano hii ni maneno halisi ya *Sheng'* ambayo yalijitokeza katika kamusi ya S.E.D.

**e) Mofolojia ya maneno ya *Sheng'***

Iraki (2004) anaonyesha jinsi baadhi ya maneno ya *Sheng'* huundwa. Maneno mengi huishia kwa herufi ***–i*** na ***–e*** hasa yale yaliyokopwa kutoka Kiingereza na kuswahilishwa. Kwa mfano, *dedi* (kufa) linatokana na neno la Kiingereza -*die*, *noki* (kuchanganyikiwa) kutoka *crazy*, *seti* (mpangilio) kutoka kwa *set* na *cheki* (kuangalia) likatoholewa kutoka kwa *check.* Aidha, maneno mengi huchukua kiambishi awali na tamati cha irabu ***o*** au ***a*.** Hali hii hujitokeza katika nomino za kipekee za kurejelea mahali na watu mahsusi. Maoni haya yalithibitishwa na Ferrari (2014). Neno *uwanja* (uga wa michezo) linakuwa ***o****wanjo* na *duka* (jumba la kuuzia bidhaa) linakuwa ***o****duka*. Mifano hii inawiana na baadhi ya maneno yaliyobainishwa katika S.E.D kama ***o****dijo*- mwalimu, ***O****kuyu* – Mgikuyu, na ***o****karo* – kipande cha karatasi.

**f) Kuvuta kwa silabi ya irabu**

Githiora (2018) ana mtazamo kuwa baadhi ya irabu za *Sheng'* zinapotokea kama kiambishi tamati hutamkwa kwa mvuto. Neno *vijana* litakuwa *vijanaa*

(watu wachanga katika umri wa ubaleghe) na *chapa* (pesa) likawa *chapaa*. Hata hivyo, sio maneno yote ya *Sheng'* huchukua mwelekeo huu.

Kihara (2006) alitoa mfano wa *raundaa* (mzunguko wa barabara) lililotokana na neno la Kiingereza *round-about*. Katika S.E.D maneno kama vile *zamoo* (zamani), *ziboo* (kutulia) na *bohoo* (mtu mjinga) yaliangaziwa.

**g) Ubadilishaji wa silabi**

Kwa mujibu wa Ogechi (2005), neno hukopwa kutoka lugha changizi. Muundo wa nje wa neno hilo hubadilishwa ili kufanya umbo linalojitokeza kuwa tofauti sana. Neno *dika* (kipande cha karatasi) limekopwa kutoka Kiingereza *card*. Baadaye linapata umbo la Kibantu *kadi* kisha silabi zake zinabadilishana nafasi hadi kuwa *dika*. Neno *jake* (nyumba) limeundwa kutoka kwa *Sheng' keja* lililotokana na neno la Kiingereza *cage*.

**h) Onomatopia**

Onomatopia ni mbinu ambapo maneno huundwa kwa kuiga tabia, sauti au mlio wa kitu (Mekonge, 2016). Mifano ya maneno haya katika *Sheng'* ni kama *nyoi* – kinyozi. Limetokana na dhana ya kunyoa. Ogechi (2005) anatoa mfano wa neno *blingbling* lenye maana ya vito vya mapambo.

**i) Urudiaji**

Ni hali ambayo sehemu ya neno au neno nzima hurudiwa. Kulingana na Echessa (1990), kurudiwa huku hukusudia kutoa dhana ya mtawanyiko, wingi, ukubwa, au ongezeko la hali au kauli. Maneno ya *Sheng'* kama *mosmos* (polepole) na *chapchap* (haraka) yameundwa kupitia kwa kigezo hiki.

**j) Polisemi**

Ni mbinu ambayo maneno huwakilisha maana zaidi ya moja (Ogechi, 2005). Warambo (2017), alitoa mfano wa neno *washa*. Neno hili katika Kiswahili sanifu lina maana ya kufanya kitu kiwake. Hata hivyo, katika *Sheng'* neno hili linapata maana kadhaa. Laweza maanisha kunywa maji, pombe, kutafuna miraa, au kukasirika kwa sababu ya kuchokozwa. Katika data ya utafiti huu, neno *wahi* katika KS humaanisha *kufika mahali*. Katika *Sheng'* neno hili linapata maana mpya ya *kudhibiti*. Neno *mbao* linalomaanisha *kipande cha mti* katika KS, katika *Sheng'* linapata maana ya *shilingi ishirini.*

### 1.7.3 Fonolojia ya *Sheng'*

Mwihaki (2007) anaeleza kuwa, mtazamo wa isimu boreshi katika fonolojia huzua seti za vizuizi bia vinavyotawala mifumo ya sauti. Hata hivyo, mifumo hii ya sauti huwa na uamilifu tofauti kutegemea na lugha pokezi. Misingi ya kifonolojia kama vile muundo wa silabi huzua vizuizi vya fonimu katika lugha pokezi. Mwihaki (2007) afafanua fonimu kama kipashio cha kimsingi cha kifonolojia ambacho hutumika kutofautisha maneno tofauti katika lugha moja. Kauli hii ilifaa katika uchunguzi huu kwa sababu iligunduliwa kuwa, fonimu ni kigezo cha kutathmini tofauti zinazozuka kati ya Kiswahili sanifu na *Sheng'*. *Sheng'* hutawaliwa na sauti saba za irabu ambazo ni: (i, e, ɛ, a, u, o, ʊ). Mwihaki (2007) alizigawa irabu hizi kwa kutumia jedwali lifuatalo.

**Jedwali la 2: Vokali za Sheng’ (Mwihaki, 2007)**

| **Mwinuko wa ulimi** | **Sehemu ya ulimi** | | |
|---|---|---|---|
| | **Mbele** | **Kati** | **Nyuma** |
| Juu | i | | u |
| Kati - juu | e | | o |
| Kati - chini | ɛ | | ʊ |
| Chini | | a | |

Mgao huu ulifaa sana katika uchanganuzi wa data za maneno katika utafiti huu kwa kuegemea mihimili ya nadharia ya Fonolojia Boreshi. Sauti za irabu za maneno ya *Sheng’* zilichunguzwa na nyingi zikawa zinaafiki miundo hii kama mashartizuizi. Maneno kama *ng**o**s**o***, ***i**na*, na ***o**lolo* yana irabu **/o**/, **/i/,** na **/a/** mtawalia. Maneno haya yanajitokeza katika S.E.D. Kadhalika, Mugambi (2007) alibaini baadhi ya konsonanti za *Sheng’* kama ifuatavyo *(p, b, f, v, mb, m, θ, t, d, s, z, nd, n, l, r, č, ǰ, ʃ,* j, *k, g, w, h)*. Konsonanti hizi zilifaa sana katika utafiti huu kwa sababu zilitumika kama baadhi ya msingi wa mashartizuizi kwa mujibu wa Nadharia ya Fonolojia Boreshi.

Hata hivyo, Mwihaki (2007) anapendekeza uchunguzi zaidi ufanywe kuhusu konsonanti nazali /***nz***/ katika neno *ma**nzi*** (msichana) na/***ndh*/** katika neno *ndhom* (bhangi). Kwa mujibu wa Mwihaki (2007), fonimu huathiriana kifonetiki katika kuunda silabi. Kwa mfano, silabi ***/o/*** yaweza kuwa umbo la msingi la fonetiki ambalo laweza kutumika kuunda silabi ya konsonanti na irabu. Kadhalika, kipashio hiki chaweza kujitokeza kama fonimu kamili katika silabi. Silabi za *Sheng’* hujitokeza katika maumbo sita makuu: KI, KIK, I, N, IK, na KKI (Mwihaki, 2007)

Ferrari (2014) alifanya uchunguzi kuhusu fonolojia ya *Sheng'*. Alibaini kuwa tofauti iliyopo kati ya *Sheng'* na KS ni finyu sana. Baadhi ya tofauti hutokana na udondoshaji wa sauti ***/gh/*** na /***kh***/ za asili ya Kiarabu na mahali pake kuchukuliwa na sauti ***/g/*** na /***k***/. Kadhalika, sauti ***/h/*** hudondoshwa kwa baadhi ya maneno na mahali pake kuchukuliwa na irabu /***a***/ hasa katika ukanushi wa nafsi ya pili umoja. Sauti ***/a/*** yaweza pia kutumika kama kiambishi awali, katika nafsi ya pili kanushi. Mfano;

Kiswahili Sanifu: yakinishi: *una*; kanushi: *huna*

*Sheng'*: yakinishi: *uko na/ una*; kanushi: *auko na / auna*

**Jedwali 3: Mfumo wa Kifonetiki wa *Sheng'* (Ferrari, 2014)**

| | Midomo | Meno na midomo | Meno | Ufizi | Ukingo wa ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vizuio pasuo | p b | | | t d | tʃ dʒ | | k g |
| Vikwamizo | | f v | ð θ | s z | ʃ | | |
| Vizuio kwamizo | w | | | r l | | J | |
| nazali | m | | | n | | | n |

Uchunguzi huu wa Ferrari (2014), ulifaa sana katika utafiti huu kwa sababu ulionyesha sauti za konsonanti za *Sheng'*. Konsonanti hizi ndizo zilitumiwa kama vigezo vya kimsingi katika kueleza sifa bainifu za fonolojia ya *Sheng'*. Mfano mzuri unatokana na uchunguzi wa Kihara (2006), alipoeleza namna neno *wadhii* la *Sheng'* lilivyotoholewa kutoka kwa *wathii* (kuenda) la Gikuyu. Sauti ya kikwamizo /***th/*** inabadilika na kuwa /***dh***/. Sauti kama hizi ziliweza kutumika kama msingi wa uchanganuzi wa miundo mbalimbali ya maneno ya *Sheng'* kifonolojia.

Sehemu hii ya mapitio ya maandishi imefaa zaidi katika utafiti huu. Mtafiti ameweza kufanikiwa kueleza hatua kwa hatua mchango bainifu wa wataalamu tofauti kuhusu msimbo wa *Sheng'*. Amefanya hivyo kwa kuweka pamoja maoni ya waandishi wanaojadili kipengele kimoja katika *Sheng'*. Mtafiti alifanya hivyo kwa kusudi la kurahisisishia msomaji kuweza kuelewa vipengele tofauti vya msimbo wa *Sheng'*. Alianza kwa kuangazia maoni ya wataalam kuhusu chimbuko la *Sheng'*, kisha akaeleza sifa za *Sheng'* ikiwa ni lugha ya mpito au pijini, mwisho akaeleza sifa bainifu za miundo ya *Sheng'* na sarufi zake kwa ujumla. Kwa kufanya hivyo, ameweza kufanikisha kurahisisha msomaji wa utafiti huu kuwa na uelewa wa kina kuhusu msimbo wa *Sheng'*.

## 1.8 Misingi ya nadharia

Utafiti huu ulitumia nadharia ya *Fonolojia Boreshi*. Nadharia hii iliasisiwa na Alan Prince na Paul Smolensky (1991). Kulingana na nadharia hii, maneno katika lugha huzalika kutokana na mwelekeo wa mkinzano kati ya taratibu za lugha. Taratibu hizi hujitokeza katika jamii kupitia kwa mashartizuizi yaliyopo. Madai yao yamekitwa kwa imani kuwa, tofauti zinazojitokeza katika lugha zote za binadamu huthaminiwa na mashartizuizi yanayohusu mpangilio wa sauti, maneno na virai.

Kager (1999), anaeleza kuwa nadharia ya fonolojia boreshi ni mfumo wa kiisimu ambapo maneno ya lugha huzalika kutokana na mwingiliano kati ya maneno na mashartizuizi tofauti yanavyopishana. Nadharia hii ni tofauti na nadharia za awali

kama vile; nadharia *Fonolojia Zalishi ya Awali*, *Nadharia Mizanishi* na *nadharia Finyizi*. Hii nadharia haizingatii sheria zinazotawala vipashio vya lugha, bali huzingatia mwingiliano kati ya vizuizi mbalimbali vya lugha. Mfumo huu waweza kutumika vyema katika kufafanua uzalishaji wa aina mbalimbali za maneno kama vile nomino, vivumishi, vitenzi na vielezi katika *Sheng'*.  Nadharia hii ilifaa zaidi katika utafiti huu kwa sababu iliweza kutumiwa kuonyesha namna maneno hubuniwa katika *Sheng'* kabla ya kukubaliwa kimatumizi katika jamii.

Kuzalika kwa aina tofauti ya maneno kukawa umboghafi na matumizi yake yakawa umbotokeo. Aidha katika KS, Nadharia ya Fonolojia Boreshi ilifaa katika uchunguzi huu kwa sababu hatua za uzalishaji wa maneno kutoka msimbo wa *Sheng'* na kuingizwa kwa KS zilichunguzwa. Maneno hayo yalichunguzwa jinsi yanavyokabiliwa na mashartizuizi mbalimbali ya lugha. Sababu za ukubalifu wa maneno hayo ama kukataliwa zilijadiliwa. Mawazo ya kimsingi kuhusu Nadharia ya Fonolojia Boreshi ni kuwa, huchukua umboghafi kama umbo lenye vizuizi na masharti mahsusi ya mpangilio ambayo huamua umbotokeo. Umboghafi katika lugha huwa na vipengele vingi. Vipengele hivi vikipitishwa katika mashartizuizi mbalimbali, huzalisha umbotokeo moja tu. Kwa mfano neno la *Sheng' kuchill* limetokana na neno la Kiingereza *chill*. Umboghafi laweza kuwa *chill*, *chili*, *chily au chilli*. Baada ya kupitia vizuizi vinavyotokana na mashartizuizi ya Kiswahili sanifu, umbotokeo litakuwa *kuchili*.

Mfumo huu huchagua umboghafi moja la neno kutokana na maumbo ghafi mengi kutegemea na vizuizi vilivyopitiwa. Umboghafi hilo likitokea kuwa neno lenye maana kamili inayokubalika kwa misingi ya sarufi ya lugha pokezi, basi huwa umbotokeo. Kwa mfano, sauti /***kh***/ na /***gh***/, ***/q/*** na ***/g/*** au ***/k/*** hukinzana katika matamshi ya Kiswahili. Maneno haya hupitia mashartizuizi ya kifonetiki ambayo huondoa sauti zisizotakiwa za ***/kh/***na ***/q/***. Hali hii huzalisha maneno ya asili yenye sauti ambayo huchukua umbo mpya kama; *lugha* badala ya *lukha* au Kurani badala ya *Quran*.

Nadharia hii hudhihirisha kuwa, viungo hivi vya mashartizuizi huwa na sifa bia. Kila mfumo wa isimu ulimwenguni huwa na viwango tofauti vya mashartizuizi. Uwezo wa mzawa lugha kuwa na umilisi wa lugha hutegemea jinsi ambavyo mzawa huyo humudu mashartizuizi haya ya lugha. Madai haya yanaungwa mkono na Kager (1999), anaposema kuwa kila aina ya lugha huwa na vigezo viwili; cha kutathmini mashartizuizi na kisichotathmini mashartizuizi katika lugha. Vigezo ambavyo havitathmini mashartizuizi huwa vinakubalika katika takriban lugha zote. Lakini vile ambavyo huathirika huwa vinaepukwa na hutumika na wanasarufi kwa ajili ya ulinganuzi.

### 1.8.1 Mihimili ya nadharia fonolojia boreshi.

#### 1.8.1.1 Umajumui

Mhimili wa umajumui huchunguza sifa za kijumla zinazotawala lugha zote za binadamu ulimwenguni (Makini, 2015). Lugha ni mfumo wa mwingiliano kati ya nguvu bia za lugha. Nguvu bia ni sheria zinazotawala mfumo wa lugha kote ulimwenguni. Nguvu bia ni mfumo na utaratibu unaotawala sarufi za lugha fulani.

Hali hii hujitokeza katika lugha nyingi duniani. Hizi nguvu huzalisha vizuizi ambavyo huathiri mfumo tokeo wa vipande vya lugha. Vizuizi hivi huwa vinakinzana na kimoja hufanya kingine kuathirika.

Kwa sababu hakuna mfumo ambao waweza kuridhisha kila shartizuizi, basi ni lazima kuwe na mbinu za kuchagua vipengele ambavyo havitaathiriwa na mashartizuizi hayo pakubwa. Kwa mujibu wa Mugambi (2007), silabi ya *Sheng'* huwa na maumbo matano. Vokali pekee (V), konsonanti(K) pekee, konsonanti konsonanti vokali(KKV), konsonanti vokali konsonanti(KVK), na nazali pekee (N). Maneno yanayokiuka mpangilio huu wa silabi katika *Sheng'* huchukuliwa kama umboghafi. Kwa hivyo, lazima yapitie katika mashartizuizi mbalimbali ili yapate umbo linaloweza kukubalika katika *Sheng'* kama umbotokeo. Maneno ya *Sheng'* yanayoishia kwa konsonanti kama *chill*, *gwan* na *mboch* yalichunguzwa namna yanavyoingizwa katika KS.

**1.8.1.2 Ukiukwaji**

Ni hali ambayo hufanya mashartizuizi kukubalika au kukiukwa katika uundaji wa maneno. Ukiukwaji huu hutegemea lugha husika (Makini, 2015). Lazima pawepo umboghafi na umbotokeo. Kila mfumo wa umbotokeo wa kiisimu hujitokeza kwa sababu hauathiriwi sana na mashartizuizi yanayokinzana. Katika aina yoyote ya umbotokeo, sarufi huzalisha viumbotokeo vingi.

Kati ya hivi viunzi, kuna kimoja ambacho huchaguliwa, na ambacho huwa umbotokeo. Kutokea huku kwa umbotokeo hupitia katika mfumo wa mashartizuizi uliopangwa

mahsusi. Vizuizi hivi, huondoa vipengele fulani vya umboghafi hadi wakati ambao, umboghafi moja tu ndilo hubaki.

**1.8.1.3 Upangiliaji**

Ni hali ambapo mashartizuizi ya lugha hupangwa kwa utaratibu msonge kutoka kwa mashartizuizi makuu hadi yale ya hadhi ya chini ambayo yaweza kuvumilika (Mekonge, 2016). Ukiukwaji wa mashartzuizi makuu mengi humaanisha kuwa neno litakalozalika halitakubalika. Mashartizuizi huwa na athari zake. Mahartizuizi ni umbo hitajika ambalo laweza kurithishwa au kuharibiwa katika mfumo wa umbotokeo. Kulingana na Kager (1999), mfumo huu hurithisha mashartizuizi fulani iwapo utaafikiana na mahitaji ya kizuizi haribifu.

**1.8.1.4 Usambamba**

Ni mfumo wa utoshelezi wa kimpangilio wa mashartizuizi na namna mpangilio huo huathiri umbotokeo (Makini, 2015). Katika mpangilio huu, kuna dhana kuwa kila lugha ina uwezo wa kupokea aina yoyote ya umboghafi. Hakuna ukomo au masharti katika kupokea aina nyingi za maumboghafi. Kwa mfano neno la *Sheng' brandi*, limetokana na neno la Kiingereza *brand*. Huenda baadhi ya maumboghafi yakawa *brandi*, *brandy*, *brand* au *brande*. Mfumo wa sarufi wa *Sheng'* hukaribiana sana na wa KS (Githinji, 2006). Basi, neno *brandi* linajitokeza kwa kuvunja mashartizuizi machache ya *Sheng'*. Baadhi ya mashartizuizi haya ni yale yaliyodokezwa na Mugambi (2007) kwamba mpangilio wa silabi za *Sheng'* uchukue umbo la KI, KKI, I, II, au IK. Aidha, silabi ya *Sheng'* lazima huishia kwa irabu. Nadharia Boreshi hujikita katika misingi mikuu ifuatayo.

**a) Msingi wa uzalishi.**

Hiki ni kipengele ambacho huzalisha maumbotokeo mbalimbali katika lugha. Haya ni maumbo tofauti ya neno moja yanayowakilisha dhana moja na huwa na ushindani. Lile umbo ambalo hupata ukubalifu wa kimatumizi basi huwa ni umbotokeo. Umbotokeo hujitokeza baada ya maumbo mengine shindani kuzuiliwa na mashartizuizi ya lugha husika. Kwa mujibu wa Makini (2015), umbo la neno linalokiuka mashartizuizi hayo basi hujitokeza kama umbotokeo. Umbotokeo laweza hata kuwa limevunja mashartizuizi kadhaa ambayo yalikuwa ya hadhi ya chini.

Mashartizuizi ya chini ni yale ambayo hukiuka utaratibu wa lugha lakini yaweza kuvumilika. Kuvumilika huku ni kwa sababu maneno husika yanaweza kueleweka katika muktadha wa mazungumzo. Neno *bako* (mchezo wa mpira wa vikapu), linatokana na neno la Kiingereza *basket ball*. Kwa mujibu wa mhimili huu, neno hili laweza kupitia vizuizi mbalimbali vinavyoathiri maumbotokeo tofauti. Baadhi ya maumbo huenda yakawa *basketi*, *basketi boli*, au *basko* kabla ya kutupiliwa mbali na kubakisha *bako*. Hata hivyo, *basket boli* laweza kuvumilika kwa sababu laweza kueleweka.

**b) Msingi wa mashartizuizi.**

Hivi ni vigezo vya masharti katika uvunjaji wa maneno ambavyo vyaweza kuvunjwa au kutovunjwa. Ni vigezo ambavyo hutumiwa kuamua ni umbo lipi la neno linalofikia hali ya ukubalifu kwa mujibu wa mashartizuizi ya lugha husika. Kwa mfano katika KS, konsonanti halisi haziwezi kufuatana mara tatu au zaidi kwa mfululizo. Neno kama *mktaba* haliwezi kukubalika kwa sababu

sharti hili haliwezi kuvunjwa. Hata hivyo likiandikwa *makitaba* laweza kuvumilika kwa sababu maana kusudiwa inaeleweka. Hata hivyo, umbotokeo halisi yafaa liwe *maktaba*. Neno la *Sheng' konda* linatokana na *conduc**t**or* la Kiingereza lenye maana ya makanga.

Huenda mfuatano wa konsontanti ***/c/*** na ***/t/*** huwa shartizuizi kwa hivyo zikadondoshwa.

c) **Msingi wa utathmini.**

Hiki ni kipengele kinachoamua ni umbo lipi kati ya maumbotokeo yaliyopo limefikia hali ya ukubalifu. Huamua ni kiunzi kipi kati ya seti nyingi za maumbo tofauti ya neno, huvunjwa masharti muhimu mengi, machache au yale ya chini zaidi, kiasi kwamba yanaweza kuvumilika. Msingi wa vizuizi vya utathmini huhakikisha kuwa umbotokeo lolote lazima liafiki matarajio ya kimuundo kabla ya kukubalika. Baadhi ya mahitaji haya huchukua mfumo wa vizuizi vya kifonolojia au kiarudhi. Katika Kiswahili, irabu haifai kuwa na sauti ya nazali. Pia, silabi ya Kiswahili haifai kuwa na sauti ya kikoda. Mfano neno *suit* litakuwa *suti*. Maneno mengi ya *Sheng'* yaliyotoholewa kutoka Kiingereza na ambayo huishia kwa koda, hudondoshwa au sauti koda hubadilika na kuwa irabu; *baby-bebi*. Vizuizi vya utathmini sio vizuizi vya umbotokeo tu, bali huangazia vipengele vya lugha katika viwango viwili: kiwango cha umboghafi na kiwango cha umbotokeo kama inavyodhihirika katika mfano hapa chini:

a) Umbotokeo lazima lihifadhi vipengele vyote katika umboghafi. Neno linalozalika kama umbotokeo lazima liwe na aina fulani ya mfanano na

umboghafi. Mzizi wa neno la Kiswahili lazima ujitokeze kwa umboghafi na umbotokeo. Sharti hili pia hujitokeza katika *Sheng'* kwa baadhi ya maneno kama *mtoto- mtoyi*.

b) Umbotokeo lazima lihifadhi mpangilio wa mlalo wa vipengele vya umboghafi. Mashartizuizi ambayo yatakuwa na athari kubwa kwa neno lazima yaorodheshwe mwanzoni kabla ya mashartizuizi yenye athari hafifu. Kulingana na maelezo haya, kielelezo kifuatacho chaweza kutumika kueleza uundaji wa maneno katika *Sheng'*.

Kwa mujibu wa kauli hii, maneno ya *Sheng'* yaliyokopwa kutoka lugha zingine yaweza kupitia vizuizi vifuatavyo;

**Jedwali 4: Mfano wa Umbotokeo katika *Sheng'***

| **Umbo ghafi** | **Silabi ya Kiswahili haishii kwa konsonanti** | **Silabi haiwezi kuwa na konsonanti mbili zinazofanana** | **Silabi ya Kiswahili huishia kwa irabu** | **Umbotokeo** |
|---|---|---|---|---|
| Chill | Chilly! * | - | - | |
| | Chily* | Chil | - | Chili |
| | Chili | Chili | Chili | |
| | Mbochy! * | - | - | |
| Mboch | Mboch* | Mboch | - | Mbochi |
| | Mbochi | Mbochi | Mbochi | |

c) Viumbotokeo na viumboghafi lazima viwe na mfanano katika vipengele vya sauti. Mfano neno *ongea* (zungumza) hunyambulika visivyo katika *Sheng'* na kuwa *ongelelea* jambo linalowatatiza watumizi wake. Kutokana na maelezo

haya, neno *ongelelea* haliwezi kukubalika katika KS kwa sababu linakiuka muundo sauti wa unyambuzi wa vitenzi katika KS.

d) Mashartizuizi ni ya ubia. Kizuizi kimoja chaweza kuonyesha athari zake katika lugha moja na kisionyeshe athari zake kwa lugha ya pili. Lakini kwa lugha ya tatu, athari zake zaweza kuonekana.

### 1.8.2 Utumikizi wa Nadharia ya Fonolojia Boreshi katika utafiti huu

Maneno na vidahizo vya maneno katika utafiti huu vilichunguzwa jinsi vinavyoathiriwa na masharti na taratibu maalum za uundaji wa maneno katika *Sheng'*. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, masharti na taratibu hizi zilichukuliwa kama mashartizuizi.

Maneno ya mkopo kutoka lugha zingine yalichukuliwa kama umboghafi. Maneno yaliyoundwa kwa kuchukua umbo jipya kulingana na mfumo wa kisarufi wa *Sheng'* basi yakawa ni umbotokeo. Aidha, kuna uwezekano wa baadhi ya maneno ya *Sheng'* kupenyezwa katika KS. Ukubalifu wa maneno haya huenda ni kwa sababu ya kutimiza mashartizuizi ya KS.

Wataalam wameweza kubainisha miundo tofauti ya maneno katika *Sheng'*. Warambo (2017) anaeleza kuwa maneno yanapokopwa kutoka lugha moja hadi nyingine hupitia mabadiliko ya kimuundo kisarufi. Muundo huu yamkini ni kupitia mashartizuizi ya lugha pokezi ambayo yaweza kutumiwa kama kigezo cha kukubali neno fulani au kulitupilia mbali. Hatua na mifumo ya miundo ya maneno kutoka neno ghafi hadi neno

kamilifu ilichunguzwa katika utafiti huu. Nadharia ya Fonolojia Boreshi ilifaa sana kwa sababu maneno ya mkopo yaliangaziwa kama umboghafi nayo maneno kamili yakawa umbotokeo.

Iraki (2004) alichunguza namna vitenzi vya *Sheng'* vinavyoundwa. Kiambishi #***ku***# hutangulia baadhi ya mizizi ya vitenzi vingi vya *Sheng'*. Iraki (2004) alitoa mfano wa neno *dead* (kufa) la Kiingereza. *Dead* likipachikwa kiambishi awali #***ku***# hubadilika na kuwa ***ku****dedi*. Aidha, neno *zubaa* linakuwa ***ku****zubaa* na *ngethia* (kuangalia), lililokopwa kutoka kwa Gikuyu likawa ***ku****ng'ethia.* Vivumishi navyo huchukua utaratibu tofauti. Iraki (2004) anaeleza kuwa, baadhi ya vivumishi huchukua viambishi vya ngeli. Katika ngeli ya A-WA, kiambishi awali #***m#*** hupachikwa kwa nomino na kuifanya kuwa kivumishi katika umoja. Katika wingi huchukua kiambishi #***wa***#.

Neno la Kiingereza *dead* likawa ***m****deadly*, *supu* likawa ***m****supu*. Hali hii inakaribiana sana na muuundo wa vivumishi vya KS kama vile *refu*- ***m****refu*, *zuri*- ***m****zuri*. Katika vielezi, kiambishi #***ki#*** na #***vi#*** hutumika kama kiambishi awali ili kubadilisha vivumishi na vitenzi kuwa vielezi. Kwa mfano, kitenzi *poa* kinakuwa ***vi****poa*, huku kivumishi *fala* kinakuwa ***ki****ufala*. Mashartizuizi mengine ni katika utohozi wa nomino.

Baadhi ya nomino zinapokopwa hudondosha baadhi ya silabi au kuzibadili kiasi kimatamshi. Maneno kama *Nairobi* yakawa *Nai*, *safari – safo* na *zamani* kuwa *zamo.* Utaratibu huu uliweza kuchunguzwa vyema kwa kutumia nadharia ya Fonolojia Boreshi. Maneno yaliyozalika kwa kudondosha silabi yalichukua mfumo huu wa

mpangilio wa silabi ya *Sheng'*.  Ferrari (2014) alichunguza mnyambuliko wa vitenzi katika *Sheng'*. Alikubali kuwa kuna uwiano mkubwa kati ya utaratibu wa mnyambuliko wa vitenzi kati ya *Sheng'* na KS. Madai haya yalikaribiana na Muaka (2011) aliyehoji kuwa kuna uwiano mkubwa kati ya sarufi ya *Sheng'* na KS.

Mbaabu (1994) alidadisi taratibu mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi katika KS. Taratibu alizobainisha ni kama vile: hali ya kutenda, kutendea, kutendeana na kutendeka. Madai haya yalikubaliwa na Ferrari (2014) hasa katika kunyambua vitenzi katika kauli ya kutendea na kutendeana. Hata hivyo, *Sheng'* huathirika pakubwa na lugha za Kibantu ambazo hutumia kiambishi tamati #***nga#*** katika hali ya mazoea. Kitenzi *huja* kikawa *hukuja**nga***, *unaenda* – *unaenda**nga***, na *unacheza* kikawa *unacheza**nga***. Mfumo huu wa unyambuzi wa vitenzi katika *Sheng'* huenda ukazua mfumo fulani wa mashartizuizi. Katika utafiti huu, vitenzi vilichunguzwa ili kubaini namna vivyoathiriwa na hiki kiambishi #***nga#***. Githiora (2018) anakubaliana na maoni haya kwa kuthibitisha kuwa kiambishi tamati #***nga#*** hutokana na mfumo wa awali wa Kiswahili cha kale. Mfumo huo ulifanana sana na mnyambuliko wa vitenzi vya lugha za Kibantu katika hali ya mazoea.

Katika ukanushaji, #***nga#*** hubadilika na kuwa #***ngi#***; *hukuja**nga*** – *hakuja**ngi***, *husoma**nga*** – *hasoma**ngi***. Haya ni baadhi ya mashartizuizi ambayo yalichunguzwa katika utafiti huu kwa kutumia nadharia ya Fonolojia Boreshi. Kwa ujumla, nadharia ya Fonolojia Boreshi ilifaa sana katika utafiti huu kwa kutathmini hatua za uundaji wa maneno ya *Sheng'*. Jedwali lifuatalo laweza kuwa kielelezo cha kuonyesha namna

baadhi ya maneno kama *kidi* huenda yaliundwa. Neno hili limekopwa kutoka neno la Kiingereza *kid* (mtoto).

**Jedwali 5: Namna mashartizuizi huamua umbotokeo katika maneno ya *Sheng'***

| Umboghafi | Mashartizuizi ya silabi za *Sheng'* | | | Umbotokeo |
|---|---|---|---|---|
| | Silabi huchukua umbo la KIKI au KKI | Silabi huishia kwa irabu | *Sheng'* huchukua kiambishi ngeli | |
| Kidd | Kidd* | - | - | - |
| Kidy | Kidy* | - | - | - |
| Mkid | Mkid | Mkid* | - | - |
| Mkidi | Kidi | Kidi | Kidi* | - |
| Mkidi | Mkidi | Mkidi | Mkidi | Mkidi |

Kulingana na jedwali hili, neno kubalifu linalotosheleza mashartizuizi ya uundaji wa leksimu za *Sheng'* ni *mkidi*. Hata hivyo neno *kidi* laweza kukubalika kwa sababu limevunja mashartizuizi ya kiwango cha chini. Hii ni kwa sababu baadhi ya nomino katika *Sheng'* kama *ndinga* (gari) na *inda* (sehemu ya viwandani) hazichukui viambishi vya wingi wala umoja.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Aina ya utafiti iliyotumika katika utafiti huu ni utafiti wa kimaelezo. Aina hii ilifaa sana katika utafiti huu kwa sababu hutumiwa iwapo maana na fafanuzi za tafiti zinahitajika na wala sio idadi ya matukio. Mtafiti aliamua kufanya utafiti kwa kutoa maelezo kuhusu sifa za kifonolojia za maneno ya *Sheng'* na namna zinavyotofautiana na Kiswahili sanifu.  Alianza kwa kuteua sampuli ya maneno kutoka S.E.D. Kisha akagawa maneno hayo katika mafungu matano makuu ambayo ni: nomino, vivumishi,

vielezi, vitenzi na vihusishi. Makundi haya ya maneno yalitolewa maelezo ya kina ili kudhihirisha sifa bainifu za kila sampuli ya maneno. Kwa hivyo, utafiti wa kimaelezo ulifaa zaidi kwa sababu ulimpa mtafiti nafasi bora ya kutoa maelezo ya sifa bainifu za maneno ya *Sheng'*.

### 1.9.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti uliotumika katika utafiti huu ni muundo wa kimaelezo. Kulingana na Kombo na Tromp (2006), muundo huu hufaa sana katika uchanganuzi wa data inayopatikana kupitia kwa makala yalioandikwa na maelezo. Muundo huu ni bora kwa utafiti huu kwa sababu ulimpa mtafiti fursa ya kutathmini na kueleza muundo wa maneno kama yanavyojitokeza katika *Sheng'* na KS. Maneno ya *Sheng'* yalibainishwa kutoka S.E.D. Maelezo yalitolewa kuhusu muundo wa maneno haya kifonolojia na namna yalivyobadilika hadi kupata ukubalifu wa kimatumizi katika jamii. Hatua ya pili ilikuwa uchanganuzi wa data kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile kugawa data katika majedwali ili kuchunguza taratibu za uundaji wa maneno sanifu kutoka *Sheng'*. Mwisho uwasilishaji wa data kwa njia ya maelezo ulifanywa.

### 1.9.2 Mahali pa Utafiti

Mahali pa utafiti ni maktaba katika bewa kuu la chuo kikuu cha Kenyatta, maktaba ya Chuo kikuu cha Moi na chuo kikuu cha Kisayansi na Kiteknolojia cha Masinde Muliro. Maktaba hizo zilikuwa na vitabu vya kutosha, majarida na makala mbalimbali yaliyozungumzia athari za *Sheng'* kwa KS. Kadhalika, utafiti ulifanyika mtandaoni kwa kudurusu machapisho yaliyofanywa kuhusu msimbo wa *Sheng'*.

### 1.9.3 Jumuiya ya utafiti

Data ya utafiti huu ilitokana na kamusi ya *Sheng'* – English Dictionary (2003). Kamusi hii iliteuliwa makusudi kwa sababu iliaminika kuwa muda mrefu uliochukuliwa baada ya kuchapisha (2003) unahalalisha utafiti huu kufanya uchunguzi wa kina kuhusu ukuaji wa leksimu za *Sheng'*. Kamusi ya S.E.D ina jumla ya leksimu 1783. Kutokana na orodha hizi za maneno, mtafiti alibainisha idadi ya maneno 335 ambayo hutumika katika *Sheng'* na katika KS. Orodha hii ya maneno ndiyo ilitumika kama data ya kimsingi ya kiuchanganuzi katika utafiti huu.

### 1.9.4 Uteuzi wa sampuli

Sampuli Kusudio ilitumika kuteua sampuli ya maneno kutoka S.E.D.  Maneno yaliyo katika S.E.D na yakajitokeza katika KS yaliteuliwa makusudi kama data ya kimsingi ya utafiti huu. Iliaminika kuwa kamusi ya S.E.D ingetoa data toshelevu kwa mujibu wa utafiti huu. Hii ilibainika kupitia kwa utafiti wa awali uliodondoa leksimu za *Sheng'* katika S.E.D. na kuonyesha kuwa leksimu hizo huenda zinajipenyeza katika KS. Maneno na vidahizo vya maneno katika kamusi hiyo yalichunguzwa kwa makini ili kuafiki malengo ya utafiti huu. Aina ya maneno yaliyochunguzwa yalikuwa nomino, vivumishi, vitenzi, vielezi na kwa kiasi kidogo vihusishi.

### 1.9.5 Ukusanyaji wa data

Maneno ya S.E.D yalitumiwa kama data ya kimsingi katika utafiti huu. Maneno haya yalifuatiliwa kwa makini ili kubaini iwapo yanajitokeza katika KS. Maneno yaliyo katika S.E.D na kisha kujitokeza katika KS yalichukuliwa kama data maalum ya uchunguzi.  Haya ndio maneno ambayo yangempa mtafiti sifa halisi ya namna

yanavyobadilika na kuathiri KS. Baada ya kuyabainisha, mtafiti aliyapanga kwa orodha kutegemea aina za maneno. Maneno yaliyojitokeza katika KS yalitumiwa kutoa sampuli ya uchanganuzi wa data.

### 1.9.6 Uchanganuzi wa data

Data ya kimsingi ya utafiti huu ni maneno yaliyobainishwa katika S.E.D. Maneno katika S.E.D yalipangwa kutegemea maana na miundo ya fonolojia. Data zilipangwa kulingana na mada tofauti tofauti kutegemea malengo ya utafiti kisha zikachanganuliwa kwa kutumia majedwali, maelezo na vielelezo. Maelezo kwa kina yalitolewa kwa kila aina ya sampuli ili kuafiki malengo ya utafiti.

### 1.9.7 Uwasilishaji wa data

Data iliwasilishwa kwa njia ya majedwali, maelezo, na michoro. Kwanza, mtafiti aligawa data katika majedwali kwa kutegemea aina za maneno. Kisha, kila seti ya jedwali ikafafanuliwa kutegemea sifa bainifu za maneno husika.

Sifa za maneno zinazojitokeza kwa uwazi katika majedwali zilielezwa kwa makini kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii imeeleza kiini cha utafiti na utaratibu uliozingatiwa katika kufanikisha utafiti huu. Aidha, sehemu hii imetoa usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, mipaka na upeo, sababu za kuchagua mada, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada pamoja na mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MANENO KATIKA S.E.D AMBAYO HUTUMIKA KATIKA KISWAHILI SANIFU.

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inadhamiria kubainisha baadhi ya maneno yanayojitokeza katika S.E.D na ambayo hutumika katika Kiswahili sanifu. Baada ya kuyabainisha, utafiti ulikusudia kueleza tofauti za kisemantiki zinazojitokeza katika maneno haya. Hii ni kwa sababu mtafiti aligundua kuwa, maneno hayo yanaweza kugawika katika vigezo tofauti kwa kutathmini maana za maneno husika. Vigezo hivi ni kama polisemi, sinonimu na uhamishaji wa maana. Tangu kuchapisha kwa S.E.D (2003), kuna uwezekano kuwa, huenda maneno yaliyoibuliwa katika kamusi hiyo yanapata nafasi katika KS. Matumizi mapana ya maneno haya katika KS ni dhihirisho tosha kuwa kuna athari za *Sheng'* katika KS.

## 2.2 Maneno katika Sheng'- English Dictionary yanayotumika katika Kiswahili sanifu.

Utafiti huu ulidhihirisha kuwa, kuna maneno katika S.E.D yanayotumika katika Kiswahili sanifu. Orodha ifuatayo ya maneno ilibainishwa katika S.E.D na vilevile katika kamusi za KS. Utafiti ulizama tu katika kuteua maneno ya S.E.D ambayo yanajitokeza katika KS. Ulifanya hivyo ili kuonyesha wazi namna maneno haya yanavyotumika katika aina hizi mbili za kamusi. Kwa kufanya hivyo, athari za S.E.D kwa KS zinaonekana wazi. Kamusi za Kiswahili Sanifu zilizotumiwa ni *Kamusi Teule ya Kiswahili* (2013) na *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (2016). Kamusi hizi zilikisiwa kuwa

kiwakilishi mwafaka cha baadhi ya leksimu zilizochapishwa za KS. Aina za maneno zilizobainishwa ni vitenzi, nomino, vivumishi, vielezi na vihusishi. Iligunduliwa kuwa hapakuwa na mifano mahsusi ya viunganishi, vihisishi na viwakilishi katika S.E.D. Hali hii huenda inatokea kwa sababu *Sheng'* hutumia maneno ya KS kuwakilisha dhana zinazoafiki aina hizi za maneno.

**2.2.1 Nomino katika S.E.D**

Kuna jumla ya nomino 195 kati ya maneno 335 yaliyobainishwa katika S.E.D. Hii ni asilimia 58 ya idadi ya maneno. Idadi hii ni kubwa sana kama kiwakilishi cha sampuli ya utafiti huu. Mtafiti alizipanga nomino hizo kiabjadi na akapunguza idadi hii kwa kutumia mbinu ya Uteuzi Sampuli Kihatua iliyopendekezwa na Mugenda na Mugenda (1999). Mtafiti aligawa nomino katika mafungu kumi na kuteua kila nomino katika nafasi ya kumi katika orodha. Kwa kufanya hivyo, aliweza kuchagua data ya nomino 21. Ifuatayo ni orodha ya nomino alizoteua.

**Jedwali 6: Orodha ya nomino katika S.E.D zinazojitokeza katika Kiswahili Sanifu**

| Nomino | Kamusi ya Sheng’ | Kamusi sanifu |
|---|---|---|
| 1. Ajuta | Vyatu | Asikitika |
| 2. Bako | Mpira wa vikapu | Kipimo cha kitanga cha mkono |
| 3. Buda | Baba | Mwanamme aliyezeeka sana |
| 4. Chokora | Watoto wa mitaani | Tafuta kwa kutawanya |
| 5. Deka | Kuona | Jivunia/ringia. tumainia msaada |
| 6. Gamu | Gundi | Kitu majimaji cha kunata |
| 7. Honda | Pikipiki | Gari la gurudumu mbili |
| 8. Kambambe | Mpira wa kandanda | Kubwa sana |
| 9. Kinaa | Ujinga, shida | Hali ya kutosheka na kitu |
| 10. Konda | Makanga | Kuwa mnyonge |
| 11. Linga | Mpishi | Pima kwa makini |
| 12. Mbao | Shilingi ishirini | Mazao ya mmea yenye mbegu na majimaji |
| 13. Mtambo | Saa ya mkono/ gari | Mashine/ kifaa cha kutoa nguvu |
| 14. Ng’oa | Mtu wa sura mbaya | Vuta na kutoa jiwe |
| 15. Paka | Uvumi | Eneza rangi/mnyama wa nyumbani |
| 16. Rada | Mazingira | Adhabu ya Mungu/kifaa cha kuongoza ndege |
| 17. Shari | Mtu | Jambo linalosababisha hasara |
| 18. Sugu | Kitu kigumu | Kutosikia adhabu/ugumu katika mwili |
| 19. Uganga | Ugali | Taaluma ya kutibu na kuponya |
| 20. Wati | Maji | Kipimo cha nguvu za umeme |
| 21. Zuzu | Mjinga | Mpumbavu |

Kutokana na jedwali hili iligunduliwa kuwa, aina nyingi za maneno yanayojitokeza katika S.E.D na KS ni nomino. Sababu kuu ya kuwepo kwa idadi kubwa ya nomino ni kwamba, ni rahisi kukopa nomino kutoka lugha zingine. Kama alivyoeleza Bosire (2006), leksimu nyingi za *Sheng'* hukopwa kutoka lugha za Kibantu na Kiingereza. Muundo wa nomino huchukuliwa jinsi ulivyo katika lugha changizi. Mabadiliko machache yanayotokana na kudondosha ama kuchukua viambishi hudumishwa. Hata hivyo, dhana inayorejelewa na nomino hizi ni tofauti mno katika S.E.D na KS. Kwa mfano, neno *ziki* katika S.E.D ni *aina ya muziki*. Neno hili likichunguzwa katika kamusi sanifu za Kiswahili linapata maana ya *aina ya mshono unaozunguka shingo.*

### 2.2.2 Vitenzi katika S.E.D

Kuna vitenzi 119 ambavyo vilibainishwa katika S.E.D na ambavyo pia hujitokeza katika KS. Hii ni asilimia 35.5 ya maneno yote yaliyo katika S.E.D na KS. Mbinu ya Uteuzi Sampuli Kihatua iliyopendekezwa na Mugenda na Mugenda (1999) ilitumika. Mtafiti aligawa vitenzi katika mafungu matano na kuchagua kila kitenzi kinachojitokeza kwa nafasi ya tano katika orodha vikipangwa kiabjadi. Akateua vitenzi 25 kama ilivyo katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 7: Orodha ya vitenzi katika S.E.D vinavyojitokeza katika Kiswahili Sanifu**

| **Vitenzi** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|
| Ambaa | Ondoka | Kaa mbali na mtu |
| Chanuka | Kuwa katika mtindi/hali ya kisasa | Mmea kuota maua |
| Chizika | Kuwa wazimu | Maji kudondoka kidogo kidogo |
| Chota | Kutoa pesa | Twaa au chukua sehemu ya kitu |
| Dinda | Kataa kwa kiburi | Kata/kuwa imara |
| Doti | Kuongea visivyo | Vipande vya kitambaa |
| Gota | Piga mtu vikumbo. | Fikia kikomo. |
| Hori | Ogopa | Mkono wa bahari ghuba/ chombo cha bahari |
| Jamu | Kasirika | Rojo ya kupaka kwa mkate. |
| Katia | Tongoza | Kata kwa niaba ya mwingine |
| Kishua | Kuwa ya ukweli | Mashua ndogo |
| Kusanya | Iba | Weka pamoja |
| Lola | Kuona | Tazama /angalia |
| Mea | Enda/ondoka | Kua kutoka ardhi au mwili |
| Muda | Kuwa kimya | Kipindi cha wakati |
| Ng'ota | Piga mtu | Toka baada ya kuvutwa |
| Omoka | Kuwa tajiri / fanikiwa | Bomoka sehemu ya nyumba |
| Pepea | Enda | Tikisatikisa |
| Pitisha | Leta | Penyeza kitu mahali fulani |
| Seti | Anza | Fungu la idadi fulani ya vitu |
| Tia | Kunywa | Ingiza |
| Tonga | Kula chakula | Toa sauti kali |
| Unda | Piga mtu | Jenga, tengeneza |
| Waya | Kosa pesa/filisika | Uzi mwembamba wa chuma |
| Zusha | Anzisha mgogoro/kasirika | Anzisha kuenea |

Kutokana na jedwali hili muundo na maana ya maneno hubadilika yanavyohamishwa kutoka KS hadi *Sheng'*. Neno *kinda* (mtoto wa ndege) la KS ni nomino lakini hutumika katika *Sheng'* kama *kitenzi* kwa maana ya *kuiba* au *kusaliti*. Kama zilivyo nomino, maana ya kimsingi ya vitenzi katika KS hubadilika na kupata maana mpya katika S.E.D. Neno la *Sheng' waka* linachukua maana ya *kulewa pombe* badala ya maana asilia ya *kutoa mwangaza* katika KS.

Matumizi haya yakizoeleka zaidi miongoni mwa jamii, maana asili ya neno *waka* itasahaulika na kutumika kwa maana ya *kulevya*. Hali hii ndio inaweza kuchangia kupungua kwa matumizi ya leksimu za KS.

### 2.2.3 Vivumishi katika S.E.D

Idadi ya vivumishi vilivyobainishwa katika S.E.D vilikuwa ni 15. Vilipangwa katika jedwali kama ifuatavyo.

**Jedwali 8: Orodha ya vivumishi katika S.E.D vinavyojitokeza katika Kiswahili Sanifu**

| **Vivumishi katika S.E.D.** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|
| Brandi | Mpya | Aina ya pombe kali |
| Dunda | Kataa, anguka kwa kishindo | Gonga kama mpira/pigisha kama |
| Enga | Kujifanya huoni mtu | Kata kwa kisu/upanga |
| Madoido | Kiburi | Urembo unaoongezewa kitu |
| Msamba | Mtu mjinga | Sehemu ya mwili kati ya mapaja |
| Mzubao | Changanyikiwa akili | Hali ya bumbuazi |
| Niaje | Salamu za kujulia hali | Iko namna gani |
| Nira | Mpya | Kipande cha mti kinachofungiwa fahali/farasi |
| Po | Nzuri | Neno linalotumiwa kwa ishara ya kutema mate |
| Poa | Kuwa sawa | Nyamaza/fifia |
| Sanywa | Kulewa ziadi | Chukuliwa na kuwekwa pamoja |
| Sasa | Salamu | Wakati huu/uliopo |
| Ukoo | Nzuri, muhimu | Uzawa wa jamii |
| Umbika | Rembeka, vutia | Kuwa na umbo/sura ya kupendeza |
| Undu | Kitu kisicho na maana | Kishingi chekundu cha jogoo |

Mtafiti alibainisha vivumishi 15 katika S.E.D na ambavyo hujitokeza katika KS. Kiwango hiki ni asilimia 4.47 ya jumla ya idadi ya maneno. Sababu kubwa inayofanya kuwa na idadi ndogo huenda ikawa wazungumzaji hutumia vivumishi vya kawaida katika KS wanapozungumza *Sheng'*.

Kadhalika, vivumishi vingi huchukua maumbo ya lugha changizi na kwa hivyo kuwa tofauti mno na muundo wa KS. Hali hii yaweza kufanya waandishi wengi kuvitupilia mbali kwa kuhofia kukiuka sarufi na muundo wa KS. Neno la Kiingereza *fit*, kwa maana ya *kuwa sawa* hutumika sana kama kivumishi. Sentensi kama; ngoma hii ni *fiti* (muziki huu ni mzuri) na dinga hii ni *fiti* (gari hili ni nzuri) ni mfano wa matumizi. Licha ya kutumika pakubwa katika miktadha mbalimbali, kivumishi hiki hakijanukuliwa katika chapisho la S.E.D.

Baadhi ya vivumishi huweza kuchukua viambishi ili kuafiki miktadha tofauti ya matumizi. Kivumishi *poa* (kuwa sawa) chaweza kuchukua viambishi na kuwa ***m****poa*, ***ki****poa*, ***wa****poa* au ***vi****poa* kutegemea nomino zinazorejelewa. Kwa mfano; *dem* ***m****poa* kwa maana ya msichana mzuri. *Kisanga* ***ki****poa* kwa maana ya jambo nzuri la kustaajabisha. Kama ilivyo katika nomino na vitenzi, vivumishi pia hupata maana mpya vikijitokeza katika S.E.D.

Vihusishi vilivyobainishwa vilikuwa vichache sana. Mtafiti alibainisha vihusishi vitano katika orodha ya maneno 335. Hii ikawa ni asilimia 1.49. Mifano imebainishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 9: Orodha ya vihusishi katika S.E.D vinavyojitokeza katika Kiswahili Sanifu**

| **Vihusishi** | **Aina** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|---|
| Kaa | H | Fanana | Jinsi kinavyoonekana/aina ya mnyama, keti |
| Shari | H | Mtu | Jambo linalosababisha hasara |
| Usuko | H | Enda na ondoka mahali | Namna ya kusuka |
| Wembe | H | Enda kwa kasi sana | Kifaa bapa bati cha kukatia |
| Ziara | H | Kuwa mviringo | Safari ya kuzuru mahali |

Mifano katika jedwali hili yaonyesha kuwa, huenda wazungumzaji wa *Sheng'* hutumia vihusishi vilivyo katika lugha changizi. Wengi labda hawajakuwa na uwezo wa kuvibuni kama ilivyo katika nomino na vitenzi. Neno *kaa* laweza kutumika kama kihusishi katika muktadha ufuataao.

*Anatembea kaa jambazi* kwa maana ya: Anatembea *namna* jambazi anavyotembea. Kama ilivyo kwenye vihusishi, mtafiti alibainisha vielezi vitano kama inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 10: Vielezi katika S.E.D vinavyojitokeza katika Kiswahili Sanifu**

| **Vielezi** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|
| Gizani | Gerezani | Kutokuwa na mwangaza |
| Orodha | kuwa karibu, zunguka karibu | mpangilio wa majina/vitu |
| Poa | Kuwa sawa | Tulia |
| Kishua | Kuwa nzuri | Mashua ndogo |
| Kirada | Kuwa katika mazingira | Kifaa cha kuongoza meli au ndege |

Hata hivyo, aligundua kuwa idadi nyingi ya vielezi katika *Sheng'* vyaweza kubuniwa na kutumika katika mazungumzo kwa kutumia viambishi #***ki#*** au #***vi#*** kama viambishi awali kwa baadhi ya maneno. Nomino nyingi na baadhi ya vitenzi zikipachikwa kiambishi awali #***ki#***, au #***vi#*** hubadilisha hilo neno na kuwa kielezi. Kwa mfano; *poa* – ***vi****poa, umbika* – ***ki****umbika*. Baadhi ya nomino za Kiingereza hupachikwa kiambishi awali #***ki#*** na kubadili nomino husika kuwa kielezi katika *Sheng'*. Neno *wembe* (enda kwa kasi sana) linakuwa ***ki****wembe* nalo neno *solo* (kuwa pekee kwa kukosa msaada) likawa ***ki****solo*.

Mengi ya maneno haya hayakunukuliwa katika S.E.D ndio maana kukawa na idadi ndogo ya vielezi. Kutokana na orodha hizi za maneno, mtafiti alibainisha idadi ya maneno 335 ambayo hutumika kama *Sheng'* na katika KS. Kamusi ya S.E.D ina jumla ya leksimu 1783. Kwa hivyo maneno yanayojitokeza katika S.E.D na vilevile kwa kamusi sanifu za Kiswahili ni asilimia 11.4. Inadhihirika wazi kuwa, kiwango cha kuathirika kwa Kiswahili sanifu kwa kuegemea uamilifu wa kamusi ni asilimia 11.4. Sampuli hii ni zaidi ya asilimia 10 inayopendekezwa katika utafiti wa kimaelezo (Mugenda na Mugenda,1999).

Maneno haya yanaonyesha sifa mbalimbali ambazo hutokana na maana rejelewa (semantiki) na mengine sauti mbalimbali za matamshi (fonolojia). Ili kutoa picha halisi ya maneno haya ni vyema kuyapanga kiabjadi kama ifuatavyo.

**Jedwali 11: Idadi ya maneno yakipangwa kiabjadi**

| Abjadi | Idadi ya maneno |
|---|---|
| A | 36 |
| B | 88 |
| C | 92 |
| D | 91 |
| E | 05 |
| F | 37 |
| G | 66 |
| H | 33 |
| I | 13 |
| J | 44 |
| K | 188 |
| L | 29 |
| M | 357 |
| N | 136 |
| O | 75 |
| P | 67 |
| R | 40 |
| S | 140 |
| T | 85 |
| U | 74 |
| V | 9 |
| W | 51 |
| Y | 4 |
| Z | 23 |
| Jumla ya idadi ya maneno | 1783 |

Jedwali hili linarahisisha kuonyesha namna kila herufi ya abjadi huwa na idadi tofauti ya leksimu. Kila herufi ya abjadi ina idadi fulani ya maneno yanayojitokeza. Maneno haya yakipangwa kwa orodha kuanzia herufi yenye idadi nyingi ya maneno hadi kwa ile ambayo ina idadi chache yatatoa taswira halisi ya idadi kiabjadi. Jedwali lifuatalo laweza kusawiri kigezo hiki.

**Jedwali 12: Idadi ya maneno kiorodha kuanzia idadi nyingi hadi chache**

| **Herufi ya abjadi** | **Idadi ya maneno** |
|---|---|
| M | 357 |
| K | 188 |
| S | 140 |
| N | 136 |
| C | 92 |
| D | 91 |
| B | 88 |
| T | 85 |
| O | 75 |
| U | 74 |
| P | 67 |
| G | 66 |
| W | 51 |
| J | 44 |
| R | 40 |
| F | 37 |
| A | 36 |
| H | 33 |
| L | 29 |
| Z | 23 |
| I | 13 |
| V | 9 |
| E | 05 |
| Y | 4 |
| **Jumla ya idadi ya maneno** | **1783** |

Maneno yanayoanza kwa herufi /**m**/ yana idadi nyingi ya maneno ambayo ni 357. Hiki ni kiwango cha asilimia 20% ya jumla ya idadi ya maneno yaliyomo katika S.E.D. Hali hii inatokana na dhana kuwa, maneno mengi ya *Sheng'* yanatokana na lugha za Kibantu ambazo leksimu nyingi huanza kwa herufi /**m**/. Hata yale ambayo yanakopwa kwa lugha zisizo za Kibantu kama Kiingereza na Kinailoti, mengi hulazimika kuchukua herufi /**m**/ kama kiambishi awali ili kutoa uamilifu wa sarufi ya *Sheng'*. Muundo wa maneno haya kifonolojia utajadiliwa katika sura ya tatu. Maneno

yanayoanza kwa abjadi /**y/** yana idadi ndogo sana ya leksimu, ambayo ni 4. Hii ni asilimia 0.22.

Sababu kubwa ya kutokea kwa leksimu nyingi kwa abjadi /**m/** huenda ni kwa kuwa kuna ushabihiano mkubwa wa lugha za Kibantu ambazo maneno mengi huanza kwa herufi ***m***. *Sheng'* hukopa maneno mengi sana kutoka lugha za kibantu (Githiora, 2018). Kuna maneno mengi pia ya *Sheng'* ambayo hayajapata uhalali wa kimatumizi katika lugha sanifu ya Kiswahili. Kati ya maneno 1783, ni maneno 335 pekee ambayo yameweza kujipenyeza kwa kamusi sanifu za Kiswahili. Idadi ya maneno 1448 hayajitokezi katika Kamusi za KS. Kunaweza kuwa na sababu nyingi ya kuwepo kwa hali hii. Moja ikiwa ni sababu za kimakusudi. Wachapishaji wa kamusi wanadhamiria kuhifadhi urasmi wa leksimu za KS bila kuonekana kupotoshwa na leksimu mpya za *Sheng'* zinazozuka katika jamii. Hii ndio sababu konsonanti za *Sheng'* za mpumuo zilizobainishwa na Githinji (2022) hazijitokezi katika chapisho la S.E.D. Sababu ya pili ni kutokana na dai la Mwangi na Mukhwana (2011) kuwa, *Sheng'* ni lugha ya kipindi ambayo msamiati wake huzuka na kupotea ama kubadilika kutegemea na matakwa ya wazungumzaji. Ubadilifu huu hufanya wachunguzi na wachapishaji wa makala ya KS kuwa makini wasije wakatumia leksimu ambazo huenda zikabadilika au kupotea zaidi katika matumizi.

Aidha, kuna hoja kuwa maumbo ya maneno mengi ya *Sheng'* hayachukui utaratibu wa KS kama zilivyo lugha za Kibantu. Ili leksimu za *Sheng'* zipate uhalali wa matumizi katika machapisho rasmi ya KS lazima muundo wa silabi uchukue mkondo ufuatao, *KI* (konsonanti irabu), *KKI* (konsonanti konsonanti irabu), *KKKI* (konsonanti konsonanti

irabu), *I* (irabu pekee) au *II* (irabu irabu). Miundo hii ya silabi itaangaziwa katika sura ya tatu. Vilevile, silabi ya mwisho kwa neno lazima iishie kwa irabu. Maneno mengi yaliyotoholewa kutoka Kiingereza yanapoingizwa KS, silabi ya mwisho huchukua sauti za irabu. Mfano *box* la Kiingereza linakuwa *boksi*. Hata hivyo, kuna baadhi ya maneno ya *Sheng'* ambayo yamekiuka utaratibu huu.

Mifano ifuatayo inatoa taswira halisi ya maneno hayo: Maneno kama *shags* (mashambani), *dogy* (mbwa) au *mkidy* (mtoto) hayawezi kupata uhalali wa kimatumizi katika KS. Kwa mujibu wa maelezo haya, ni dhahiri kuwa maneno ambayo yanajitokeza katika *Sheng'* na KS yanatokana na hali ya kuhamisha maana, sinonimu au polisemi. Itakuwa vyema iwapo utafiti huu utaweza kutathmini dhana hizi kama zilivyojitokeza katika *Sheng'* na KS.

## 2.3 Sifa za kisemantiki za maneno katika S.E.D

Mtafiti aligundua kuwa ni vyema kuainisha maneno yanayojitokeza katika kamusi ya S.E.D katika viwango tofauti. Maneno haya yakiangaziwa kwa makini, yanaweza kubainishwa vyema kwa kutathmini maana ya maneno husika katika miktadha mbalimbali. Uchunguzi huu wa maana za maneno ndio unaotusukuma kutalii semantiki ya maneno haya. Baadaye utafiti utachanganua fonolojia yake katika sura ya tatu.

### 2.3.1 Uhamishaji wa maana

Hii ni hali ambapo maana asili ya neno hubadilika. Neno la Kihindi *boza* lilimaanisha aina fulani ya pombe (Githiora, 2018). Katika *Sheng'* neno hili linapata maana mpya ya *bangi*. Kulingana na Githiora (2018) maneno ya kawaida katika KS yanapata maana

mpya katika *Sheng'*. Neno *mahewa* badala ya kumaanisha hewa ya kupumua au upepo, katika *Sheng'* linakuwa *muziki*. Neno *mchuma* linalotokana na vifaa vya chuma, katika *Sheng'* linapata maana ya *bunduki*. *Kago* linalotokana na *Cargo* la Kiingereza halimaanishi mizigo kama ilivyo asili yake katika Kiingereza. Katika *Sheng' kago* lamaanisha vitu vya wizi. Githiora (2018), anaona kuwa sababu kuu ya kubadili maana ya maneno haya ni kuficha siri. Vijana wakiona neno fulani limetumika pakubwa na kuenea sana, hubuni neno lingine mpya lenye maana sawa na lile tangulizi. Vilevile, sababu kuu yaweza kuwa kuonyesha ubunifu wa kiwango cha juu unaodhihirika katika watumizi wa *Sheng'*.

Kutokana na jedwali la 12 la orodha ya maneno ya *Sheng'* pale juu, maneno mengi ya KS yanapata maana mpya na tofauti sana kinyume na maana asili. Neno *tupa* katika KS ni *kurusha kitu kama jiwe* lakini kwa *Sheng'* linakuwa na maana ya *kunuka*. Nalo neno *wazi* katika *Sheng'* huashiria *asante* lakini katika KS ni *kuonekana kwa urahisi*. Licha ya kuwa Githiora (2018) alibaini na kutoa sababu za kubadilika kwa maneno haya, hakuangazia hasa maneno yanayojitokeza katika chapisho la S.E.D. Mtafiti aliona ni vyema kuchunguza zaidi hali hii kwa kuegemea kamusi ya S.E.D. Alibainisha maneno yafuatayo katika S.E.D ambayo maana yake asili imehamishwa.

**Jedwali 13: Kuhamisha maana katika S.E.D.**

| **Leksimu katika S.E.D.** | **Lugha changizi** | **Maana asili** | **Maana katika S.E.D.** |
|---|---|---|---|
| Kao | Cowboy– Kiingereza | Anayeendesha farasi | Mwenye pesa |
| Kaso | Cazzette - Kiingereza | Kanda ya muziki | Binamu |
| Mugeka | Gikuyu | Mkeka/godoro | Nguo za ndani |
| Mzinagogi | Synagogue – Kiingereza | Hekalu | Bhangi |
| Nyoa | Nyoa - Kiswahili | Kutoa nywele | Kutomsema mtu |
| Inua | Inua – Kiswahili | Beba juu | Piga/ anzisha gari |
| Andasi | Mandazi - Kiswahili | Keki | Miraa |

Kutokana na jedwali hili, maana ya maneno asili katika lugha changizi yanabadilika na kuchukua maana mpya katika S.E.D. Neno *andasi* linapobadilika maana asili na kuchukua maana mpya ya *miraa* huenda maana hiyo asili ikasahaulika au kudidimia kimatumizi. Kwa kufanya hivyo, matumizi ya neno *miraa* yataathirika au kusahaulika. Hali hii huenda ikachangia katika kupungua kwa matumizi ya KS.

### 2.3.2 Polisemi

Ni hali ambayo neno moja huwa na maana nyingi. Githiora (2018) anatoa mfano wa neno *mbao* lililokopwa kutoka kwa lugha ya Gikuyu. Kiasili, humaanisha shilingi ishirini. Katika *Sheng'* neno hili linapata maana zaidi. Linasimamia *kofi* au *kuwa katika hali ya kuchanganyikiwa*. Upolisemi ni mbinu ya kuongeza au kupanua maana ya maneno ambayo tayari yako katika lugha (Mwangi na Mukhwana 2011). Maneno ambayo tayari yako katika lugha huweza kuongezewa maana ya ziada. Neno linalotumiwa katika muktadha mmoja hupanuliwa ili litumike katika muktadha mwingine. Lugha ya Kiswahili, sawa na *Sheng'* huunda maneno yake kwa kutumia

mbinu hii. Ogechi (2005) anasema kuwa, nomino kopwa katika *Sheng'* hupata upanuzi wa maana kisemantiki. *Sheng'* hupata maneno yake baada ya kukopa maumbo ya maneno, kisha maumbo hayo hupewa maana mpya. Utafiti uligundua maneno yafuatayo yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii katika kamusi ya S.E.D:

**Jedwali 14: Polisemi katika S.E.D**

| Neno | Maana asili | Maana ziada |
|---|---|---|
| Demu | Aina ya kitambaa kuukuu | Msichana |
| Mbuyu | Aina ya mti | Baba |
| Poa | Kuwa baridi | Sawasawa |
| Chapa | Adhibu | Kutopendeza /konda |
| Dunga | Choma kwa kifaa | Vaa |
| Mhadhara | Kipindi cha somo | Shida /matatizo |
| Ubao | Kipande cha mbao | Hisa njaa |

Kutokana na mifano hii, ilibainika kuwa maneno hukopwa kisha maana hupanuliwa kwa kupewa maana mpya iliyo tofauti na maana ya neno hilo katika lugha changizi. Matumizi mapana haya ya maneno ya S.E.D yanaweza kuhalalishwa baada ya uzoefu mwingi na kwa hivyo kuchangia kupungua kwa matumizi kwa maana asilia katika KS.

### 2.3.3 Sinonimu

Kuna maneno mengi tofauti ya *Sheng'* ambayo huwa na maana sawa. Hali hii hutokea wakati maneno yanayokopwa kutoka lugha zingine hutumika kama maneno mbadala au huchukua nafasi ya maneno ya kawaida. Wakati mwingine maneno hayo hutumika kimafumbo. Kama yalivyoangazia na Githiora (2018), maneno mengi ya mkopo hayangehitajika katika *Sheng'*. Tayari kuna maneno asilia yenye maana sawia na maneno ya mkopo. Hiki ni kigezo kikuu katika utafiti huu kilichokusudiwa

kubainishwa iwapo ukopaji wa leksimu huchangia katika ufifiaji wa matumizi ya leksimu za KS. Kwa mujibu wa Githiora (2018), maneno ya mkopo hutumika kuchukua nafasi ya maneno ya KS. Nafasi za maneno hayo huzibwa kwa maneno ya mkopo kutoka lugha za Kiingereza na lugha za Kienyeji. Neno *odijo* linatumika badala ya *mwalimu*, ama *ngepa* kwa *kofia*, *mngoso* kwa *mzungu* na *njeve* kumaanisha hali ya *baridi*.

Sababu kubwa ya kuwepo kwa sinonimu kulingana na Githiora (2018), ni kuficha siri ili watu wasiohusika katika kundi la wazungumzaji wasielewe kinachozungumziwa. Sababu ya pili ikawa ni kuonyesha usasa unaokusudiwa na vijana wengi wanaotumia *Sheng'*. Hata hivyo, Githiora (2018) hakushughulika na leksimu za S.E.D. Utafiti huu ulinuia kuweka wazi namna leksimu katika S.E.D hubuniwa kupitia kwa njia ya sinonimu. Mtafiti aliweza kugawa sinonimu katika mafungu matatu kama alivyofanya Ogechi (2005); Sinonimu jozi, sinonimu utatu na sinonimu unne.

#### 2.3.3.1 Sinonimu jozi

Haya ni maneno mawili tofauti ambayo yaweza kutumika kwa njia mbadala, moja likachukua nafasi ya lingine. Ogechi (2005) anaeleza kuwa, sababu moja yaweza kuwa ni kuzuka kwa neno moja baada ya lile la awali kutumika kwa wingi na kuchakaa. Maoni haya yanaungwa mkono na Kihara (2006).

Kihara (2006), alieleza sifa moja ya *Sheng'* kwamba maneno tofauti yanatumiwa kurejelea kitajwa kimoja. Neno linapojulikana kwa watu wengi katika *Sheng'* linapoteza umuhimu wake na lingine linabuniwa kuchukua nafasi yake.

**Jedwali la 15: Sinonimu jozi katika S.E.D.**

| Neno awali | Neno la sasa | Maana |
|---|---|---|
| Jamaa | Chalii | Rafiki mvulana |
| Mathee | Masa | Mama |
| Ndhomu (bomu) | Shada | Bhangi |
| Njaro | Mchoro | Shughuli |
| Kobole | Ngovo | Shilingi tano |
| Ngoma | Mahewa | Muziki |
| Paoo | Bluu | Shilingi ishirini |
| Soo | Nyanga | Shilingi mia moja |
| Beshte | Beshti | Rafiki |
| Ugangaa | Sembe | Ugali |
| Msunye | Ngoso | Mzungu |
| Brathee | Bro | Ndugu |
| Sistee | Siz | Dada |
| Makhonya | Manduani | Mlafi |

Maneno *jamaa* na *ngoma* yanapatikana katika kamusi ya S.E.D. Kadhalika, maneno haya yamo katika S.E.D. Hii ni ishara tosha kuwa polisemi hujitokeza katika leksimu za *Sheng'*. Hali hii inaweza changia kupunguka kwa matumizi ya leksimu za KS na nafasi zake kuchukuliwa na leksimu za *Sheng'*.

### 2.3.3.2 Sinonimu utatu

Ni hali ambapo kunazuka leksimu tatu kuelezea dhana moja katika *Sheng'* (Ogechi, 2005). Hali hii huwapa watumizi wa *Sheng'* aina tatu tofauti za maneno ya kutumia kuelezea dhana moja. Maneno haya yote yaweza kutumika kwa njia mbadala. Mtafiti aliweza kubainisha mifano ifuatayo ya sinonimu utatu katika kamusi ya S.E.D.

**Jedwali la 16: Sinonimu utatu katika S.E.D.**

| Neno 1 | Neno 2 | Neno 3 | Maana |
|---|---|---|---|
| Doo | Ganji/Ganzi | Manyamoo | Pesa |
| Mozo | Fegi | Fwaka | Sigara |
| Ashara | Ashuu | Kindee | Shilingi kumi |
| Moti | Dinga | Buu | Gari |
| Fathee | Buda | Mbuyu | Mzazi |

Maneno haya matatu tofauti yanarejelea dhana moja ya maana. Watumizi wa msamiati huu wana hiari ya kuchagua moja ya maneno haya na kutumia katika mawasiliano bila kubadili maana lengwa. Dhana hii ya sinonimu utatu bado inajitokeza kwa ukubwa katika leksimu nyingi za *Sheng'*. Wazungumzaji wanapoendelea kutumia leksimu hizi basi huenda neno la kawaida la KS likapuuzwa ama kutupiliwa mbali kimatumizi.

#### 2.3.3.3 Sinonimu unne

Kulingana na Ogechi (2005), ni hali ambapo dhana moja huweza kusimamiwa na maneno manne. Mtafiti aliweza kupata mifano ifuatayo kutoka kwa S.E.D.

**Jedwali la 17: Sinonimu unne katika S.E.D.**

| Neno 1 | Neno 2 | Neno 3 | Neno 4 | Maana |
|---|---|---|---|---|
| Chik | Demu | Kasupuu | Manzi | Mchumba wa kike |
| Poonyi | Pai | Karau | Koopa | Polisi |
| Ushaago | Shake | Shags | Ocha | Nyumbani |
| Amalulu | Adamse | Chamu | Muratisi | Pombe kali ya kienyeji |
| Chepkuna | Bokyo | Churo | Kuro | Kahaba |
| Fegi | Mozo | Garazi | Fela | Sigara |

Maneno haya na mengine mengi humpa mzungumzaji uwanja mpana wa kuchagua leksimu mbadala ya kutumia katika maelezo ya miktadha tofauti. Kwa kufanya hivyo, maneno ya msingi ya KS yatapata upungufu kimatumizi kwa hivyo kuchangia katika kudunisha kwa KS. Kutokana na mifano hii, maneno manne yanatumiwa kuashiria maana moja. Hali hii yaweza kutokana na namna vijana huendelea kubuni msamiati kila kuchao kueleza dhana moja. Kusudi lao laweza kuwa ni kuhifadhi siri (Githiora, 2018), ama kuonyesha tu ubunifu. Kuna uwezekano kuwa vijana hufanya hivi ili

kuondoa neno fulani ambalo kwa misingi ya mitazamo yao, huwa limechakaa kimatumizi. Kutokana na orodha hizi za maneno, ni dhahiri kuwa kuna maneno mengi ambayo msingi wake ni KS na ambayo hutumika pakubwa katika *Sheng'*. Umbo asili la neno linabaki jinsi lilivyokuwa awali lakini hupata maana tofauti likiwa katika *Sheng'*. Hata hivyo, ni vyema kubainisha maneno mengine ya *Sheng'* yaliyo kwenye S.E.D na hujitokeza katika miktadha mbalimbali.

## 2.4 Maneno ya S.E.D yanayojitokeza katika miktadha mbalimbali.

Athari za S.E.D zaweza kutathminiwa vyema iwapo leksimu zake zaweza kuchunguzwa ili kuonyesha namna zinavyotumika katika mazingira tofauti. Umilisi wa lugha na wazungumzaji hudhihirika vyema jinsi wanavyotumia lugha husika katika miktadha mbalimbali. Utafiti huu ulichunguza namna maneno ya *Sheng'* yanavyojitokeza katika mazingira tofauti ya mawasiliano. Kwanza, uliangaza namna *Sheng'* inavyojitokeza katika muktadha wa vyombo vya habari.

Mtafiti alichunguza matumizi ya lugha katika vituo vya redio na runinga. Aidha, alichunguza namna *Sheng'* inavyojitokeza katika magazeti, mitandao ya kijamii, ughaibuni na hata katika mazingira ya shule miongoni mwa wanafunzi. Isitoshe, aligundua kuwa, kuna mchipuko wa *Sheng'* katika muktadha wa biashara. Ikabidi achunguze namna maneno ya *Sheng'* yanavyotumika katika sekta ya juakali, matangazo ya biashara na katika sekta ya uchukuzi wa matatu. Baada ya kufanya hivyo, aliona vyema kuchunguza iwapo leksimu za S.E.D zinajitokeza katika miktadha hii.

### 2.4.1 *Sheng*' katika vyombo vya habari

Kulingana na takwimu za Githiora (2018), kulikuwa na vituo vya redio 178 nchini Kenya. Kwa hivi sasa (2023), huenda idadi hii imeongezeka pakubwa. Kati ya vituo hivi kuna vituo saba ambavyo hupeperusha matangazo kwa kutumia KS. Kituo kilichoimarika zaidi katika matumizi ya *Sheng'* ni Ghetto Radio FM. Idhaa hii ni maarufu sana miongoni mwa vijana katika sehemu za mabanda jijini Nairobi. Kadhalika, vituo vingine vya redio na runinga huwa na angalau kipindi ambacho husheheni matumizi ya *Sheng'*. Katika redio *Citizen,* kuna kipindi cha *Kizazi Kipya* kinachopeperushwa na mtangazaji *Willy M. Tuva* ambacho hutumia *Sheng'* kwa wingi mno. Haya ni baadhi ya maneno ambayo yalibainishwa katika kipindi hiki ambayo yanajitokeza pia katika S.E.D.

**Jedwali 18: Maneno ya S.E.D yanayotumika katika kipindi cha Kizazi Kipya katika *Redio Citizen***

| **Maneno katika S.E.D.** | **Maana** |
|---|---|
| Ngoma | Muziki |
| Kibao | Aina mpya ya muziki |
| Msanii | Mwanamuziki |
| Madredi | Nywele ndefu zilizosokotana |
| Maskani | Makao/makaazi |

Licha ya kuwa vipindi vingine hukusudia kutumia KS, watangazaji hawana uwezo wa kuwazuia watazamaji na wasikilizaji wanaopiga simu na kutoa maoni yao wakitumia *Sheng'*.

### 2.4.2 *Sheng'* katika magazeti.

Matumizi ya *Sheng'* yamepenyezwa na hata kutengewa kurasa katika baadhi ya magazeti nchini Kenya. Gazeti la *Taifa Leo* lina ukurasa mahsusi wa *Dondoo* za *Hapa na Pale* ambao hutumia *Sheng'*. Maneno katika kurasa hizi kama vile *jombi* (mwanamme msherati), *manzi* (mpenzi wa kike), *kalameni* (mwanamme mkora), na *msupuu* (msichana mrembo) ni ya *Sheng'*.

Kulingana na Githiora (2018), kuanzia mwaka wa 2013 kulizuka chapisho la gazeti la *The Nairobian* ambalo pia lina kurasa maalum ambazo zimetengewa msimbo wa *Sheng'*. Baadhi ya makala katika gazeti hili ni kama *Story Moja* ambayo hutumia *Sheng'*. Matumizi haya katika vyombo vya habari ni ishara tosha kuwa kuna tishio kuwa huenda matumizi ya KS yakapungua. Utafiti huu uliweza kubainisha maneno kadhaa ya *Sheng'* katika gazeti la *Taifa Leo*. Kuna ukurasa wa *Dondoo za Hapa na Pale* ambazo waandishi hutumia msimbo wa *Sheng'*. Mtafiti alibainisha mifano ifuatayo kwa baadhi ya chapisho.

**Jedwali 19: Maneno ya *Sheng'* katika gazeti (Taifa Leo, Juni 22, 2022)**

| **Data** | **Jinsi ilivyotumika** | **Maana ya data pekee** |
|---|---|---|
| Polo | *Polo* wa hapa haamini kupoteza pesa zake | Mwanamme wa makamo |
| Demu | Alikuwa na mazoea ya kuchapikia kila aina ya *demu* | Msichana mrembo |
| Chonjo | Uko *chonjo* mrembo | Kuwa na sura ya kupendeza |
| Nitakuspoil | Leo *nitakuspoil* kwa lunch | Nitakununulia |
| Ilivyotuna | Alimwonyesha mifuko ya suruali na koti lake *ilivyotuna* pesa | Ilivyojaa |
| Lojingi | Alimrai demu hadi *lojingi* | Chumba cha starehe |
| Jombi | *Jombi* alinyenyekea | Mwanamme msherati |
| Manyani | Toka ama niwabadilishe *manyani* | Wanyama wa mwituni |
| Alizusha | Jamaa *alizusha* | Alikasirika |
| Kidosho | Siku iliyofuata *kidosho* alifunga viraga | Msichana mrembo |
| Stori | Leo umenipanga kwa *stori* zako | Kisa cha kusisimua |
| Alimwangushia /marungu | *Alimwangushia* jamaa *marungu* kadhaa | Alimpiga Fimbo |

Maneno kama *tuna*, *demu*, *chonjo*, *angusha*, *zusha*, *stori* na *marungu* yamo katika kamusi ya S.E.D.

Kutumika kwa maneno haya katika gazeti la *Taifa Leo*, ambalo ni gazeti pekee la KS kuchapishwa nchini Kenya, ni ishara tosha kuwa leksimu za *Sheng'* zinaweza kuathiri matumizi ya KS. Mwandishi wa makala haya aliyatumia maneno hayo makusudi ili kuwanasa wasomaji wake ambao hutumia *Sheng'*.

### 2.4.3 *Sheng'* katika mitandao ya kijamii

Kuna ushahidi wa kutosha kuwa matumizi ya *Sheng'* kwenye mitandao ya kijamii unazidi kukua. Viungo vya mitandao kama vile *facebook*, *whattsapp*, *youtube*, *Instagram* na *twitter* nchini Kenya husheheni matumizi ya *Sheng'*. Wanaotumia viungo hivi hutumia *Sheng'* kwa sababu ndio lugha yao ya kimsingi ya kujieleza.

Mitandao hii pia imevutia kampuni na wafanyi biashara kutangaza huduma na bidhaa zao kwa mitandao wakitumia *Sheng'*. Hata hivyo, maneno mengi yaliyobainishwa katika *Sheng'* mitandaoni hayamo katika kamusi ya S.E.D. Hii ni kwa sababu wakati wa kuchapisha kamusi hii (2003), matumizi mapana ya simu za mitandao na tarakilishi hayakuwa yamekita mizizi. Kwa mfano, neno *flashi* linatumika kwa maana ya *kutoa mimba*. Matumizi ya sasa ya neno hilo ni *kupiga simu ghafla na kisha kuikata*. Mtafiti aliweza kubainisha baadhi ya jumbe za simu kwa mitandao na kuona namna leksimu za *Sheng'* hujitokeza:

**Jedwali 20: Matumizi ya *Sheng'* katika mitandao ya kijamii**

| **Data** | **Jinsi ilivyotumika** | **Maana ya data pekee** |
|---|---|---|
| Sasa | *Sasa* Jim? | Hujambo |
| Poa | Nko *poa*. | Nimetulia |
| Shags | Ulienda *shags*? | Mashambani |
| Buru. | Nko Buru. | Buruburu |
| Juu ya. | *Juu ya?* | Kwa sababu gani? |
| Set | Nko *set* kuanza *job kampu* | Natarajia kuanza kazi kwa kampuni |

Neno *nko* (nimetulia) latokana na KS *niko*. Katika *Sheng'* sauti ya irabu ***/i/*** yadondoshwa na kuwa ***/n/.*** Kadhalika, neno Buruburu (mtaa wa makaazi jijini Nairobi) ladondosha silabi tamati ***bu-ru*** na kuwa *Buru.*

### 2.4.4 *Sheng'* katika sekta ya Jua Kali

*Kamusi Teule ya Kiswahili* (2013) yafafanua Juakali kama kazi yeyote kama vile uhunzi, aghalabu inayofanyika nje kwenye jua. Katika muktadha huu, biashara ndogo ndogo, kazi za mikono na ufundi wa kiwango cha chini huweza kubainishwa kama sekta ya juakali. Kazi hizi hufanyika katika mazingira yasiyo rasmi na wafanyibiashara

wa mtaji mdogo. Miji mingi nchini Kenya imetenga maeneo rasmi kwa ajili ya huduma na biashara za juakali. Sekta hii ni maarufu sana kwa watu wa tabaka la chini kwa sababu hubuni nafasi nyingi za kazi. Lugha inayotumika katika miktadha hii ni *Sheng'* (Githiora, 2018). Katika S.E.D mtafiti alibaini maneno kama *kago* na *burungo*. *Kago* humaanisha *kibunda kikubwa cha mizigo* na *burungo* ni *mizigo mingi iliyotapakaa na kutawanyika kwa wingi*. Maneno haya licha ya kuwa machache, yalijitokeza katika S.E.D.

### 2.4.5 *Sheng'* katika matangazo ya Biashara

Msimbo wa *Sheng'* hutumika pakubwa katika matangazo ya biashara. Kampuni nyingi na wafanyibiashara siku hizi hutumia *Sheng'*. Hufanya hivi ili kunasa makini ya watazamaji wa runinga na wasikilizaji wa redio. Baadhi ya vibandiko mtaani pia hutumia *Sheng'*. Sifa za *Sheng'* kuwa ni lugha inayodhihirisha dhana za kipekee za usasa, ubadilifu, ubunifu na uchangamano huvutia sana wateja wengi ambao ni vijana (Githiora,2018). Ili kuwavutia wateja, lazima matangazo haya ya kibiashara yatumie *Sheng'*. Maneno kama vile *pata chapaa* (pata pesa), hutumiwa pakubwa katika redio na runinga. Kampuni nyingi na wafanyibiashara wengi huhiari kutangaza bidhaa na huduma zao kupitia *Sheng'*. Msimbo huu, huonekana bora kwa sababu husaidia kulinganisha bidhaa na sifa za kipekee za kuwavutia wateja.

Sifa hizi ni kama vile ubadilifu, taswira ya kimataifa, usasa na ubunifu. Hizi sifa huafiki na kuwa kishawishi cha kunasa makini ya wateja. Ferrari (2014) alitoa mifano ifuatayo kueleza namna *Sheng'* hutumika katika matangazo ya biashara na taasisi mbalimbali: Kuna tangazo la matumizi ya mipira ya mapenzi katika redio na runinga

kwa kutumia neno "*nakufeel*" neno hili lamaanisha *nina hisia kwako*. Kadhalika, kuna mfano wa; "*Bamba hapa, maliza hapa"*. Kauli hii ina maana ya *nunua kadi ya shilingi ishirini ya kupiga simu hapa*. Tangazo hili lilinukuliwa kutoka kwa duka la kuuza kadi za kupigia simu za kampuni ya Safaricom. Katika matangazo ya redio, Ferrari (2014) alinukuu ujumbe huu: *Maisha ni kudunda "*maisha ni kuchangamka". Hili tangazo ni la kituo cha redio cha Maisha FM. Maneno haya *bamba* na *dunda* yanajitokeza katika S.E.D. Hata hivyo, utafiti huu ulikuwa tofauti na Ferrari (2014) kwa sababu uliegemea leksimu za S.E.D.

**Jedwali 21: Maneno ya S.E.D katika matangazo ya biashara**

| **Neno** | **Maana** |
|---|---|
| Ashara | Shilingi kumi |
| Brandi | Kuwa mpya |
| Chapaa | Pesa |
| Chota | Kutoa pesa |
| Doo | Pesa |
| Fashoni | Mdundo wa mavazi wa kisasa |
| Finje | Shilingi ishirini |

Maneno haya hutumika kurahisisha mawasiliano kati ya muuzaji na mteja. Mchuuzi aweza kutangaza bidhaa zake kwa kuitisha shilingi kumi. *Mfano "kitambaa ni ashara tu"* kwa maana ya *kitambaa nauza kwa shilingi kumi tu.* Mteja anaweza kutaka kujua kama ni kitambaa mpya kwa kuuliza*; "ni brandi kweli?"* Kwa maana ya *ni mpya kweli?* Kisha akaambiwa na mchuuzi *"chota chapaa"* kwa maana ya *leta pesa.* Mteja anapofungiwa kitambaa anaweza kuhoji ikiwa ni *fashoni* ya kisasa. Matumizi ya leksimu hizi yakiendelea yaweza kupunguza matumizi ya KS.

Githiora (2018), alifanya utafiti kuhusu matumizi ya *Sheng'* miongoni mwa wanafunzi katika shule moja ya umma sehemu za mashambani kaskazini mwa mji wa Nairobi. Mbinu ya hojaji ilitumika katika ukusanyaji wa data ambapo wanafunzi walijaza hojaji kwa kueleza aina za lugha wanazotumia katika mazingira tofauti. Matokeo yake yameorodheshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 22: Matumizi ya *Sheng'* miongoni mwa wanafunzi katika shule za mashambani (Githiora 2018).**

| **Muktadha** | **Kiswahili sanifu** | ***Sheng'*** | **Gikuyu** | **Kiingereza** |
|---|---|---|---|---|
| Lugha ya mama | 9.4% | 0% | 88.5% | 2.1% |
| Nyumbani | 17% | 0.4% | 81.2% | 1.4% |
| Mitaani | 26.4% | 34.9% | 36.6% | 2.1% |
| Makundi | 38.3% | 28.1% | 23.4% | 10.2% |
| Shuleni | 27.7% | 1.7% | 1.2% | 69.4% |

Katika jedwali hili, lugha ya Gikuyu hutumika kwa kiwango kikubwa sana na wanafunzi wakiwa nyumbani (88.5%). Kiingereza ikiwa lugha ya lazima na ya matumizi katika kufunzia aina nyingi za masomo katika shule, ikafuata na asilimia (69.4). Msimbo wa *Sheng'* ukajitokeza kama lugha pendwa na wanafunzi wakiwa mitaani na makundini kwa asilimia 34.9 na 28.1 mtawalia. Kulingana na utafiti huu, ni wazi kuwa *Sheng'* ni msimbo wa lugha pendwa miongoni mwa wanafunzi hasa wakiwa katika mazingira yasiyo rasmi na katika mazungumzo ya wao kwa wao. Utafiti huu unashabihiana na wa Githiora (2018), kwa kuonyesha namna *Sheng'* ilivyo lugha pendwa miongoni mwa wanafunzi katika mazingira yasio rasmi. Shinikizo kwa

wanafunzi kutumia lugha ya Kiingereza au KS ni hatari kwa maendeleo na matumizi ya KS katika taasisi za elimu. Wanafunzi yafaa wajivunie lugha yao katika miktadha yote iwe rasmi ama isiyo rasmi pasi na kushurutishwa. Shuruti hii ikiendelea basi wanafunzi wengi wataanza kutumia msamiati wa *Sheng'*. Baadhi ya maneno haya yako katika S.E.D. Hii ni dhahiri kuwa kamusi ya S.E.D bado ina athari kwa KS.

### 2.4.6 *Sheng'* ughaibuni

Bidhaa na huduma nyingi katika jamii kutoka kwa Wamerika weusi hadi kwa wakaaji wa Nairobi hupokea kupitia kwa *Sheng'* (Githiora 2018). Miziki aina ya *hip hop, reggae,* na filamu za mitandao husheheni matumizi ya *Sheng'*. Mifumo ya utandawazi imefanya dunia kuwa familia moja kiasi kwamba lugha yaweza kusambaa kwa maeneo mapana kote ulimwenguni. Aidha, watu kutoka maeneo mbalimbali ya ulimwengu huweza kusafiri na kujumuika na wengine kwa kiwango kikubwa kuliko ilivyokuwa hapo awali. Wakenya wengi kwa hivi sasa wanaishi ughaibuni. Mawasiliano yao na jamii zao nyumbani hutumia *Sheng'*.

Wanamuziki wa Kenya kama vile Jua Kali, Octoppizzo hutumia *Sheng'* (Githiora 2018). Maneno ya *Sheng'* kama *yo, whassup, bling* na *blane* ni ya *Sheng'*. Wakenya wanaoishi ughaibuni hufuatilia matukio mbalimbali nchini kupitia kwa mitandao na vyombo vya habari. Kukitokea swala la mjadala katika redio au runinga hutumia *Sheng'* katika baadhi ya mawasiliano. Wanahabari wana uwezo mkubwa wa kudhibiti matumizi ya lugha rasmi wakitangaza kwa vyombo vya habari. Lakini hawana uwezo wa kudhibiti wasikilizaji na watazamaji wanaopiga simu na kuchangia mijadala mbalimbali. Wengi wa wafuasi wa mijadala hii hutumia *Sheng'*. Kusambaa huku kwa

maneno ya *Sheng'* hadi katika maeneo ya ughaibuni huenda kukaathiri pakubwa KS. Wageni katika nchi hizi za kigeni ambao wana tamaa ya kujifunza KS huenda wakapotoka kwa kushindwa kubaini leksimu za *Sheng'* na zile za KS. Mgeni aliye Marekani atakuwa na ugumu kupambanua mpaka uliopo kati ya *Sheng'* na KS.

### 2.4.7 *Sheng'* katika muziki wa reggae

Muziki aina ya reggae umevuma sana na kusikika pakubwa katika maeneo tofauti ya burudani miongoni mwa vijana. Katika vilabu, usafiri wa matatu, waendeshaji pikipiki na hata kwa vibanda vya kuuzia bidhaa mitaani na maduka, muziki wa reggae huchezwa. Wanamuziki wa Kenya kama vile Wyrie na Nazizi hutumia *Sheng'* katika nyimbo zao. Kwa sababu ya mitandao, nyimbo zao zimesambaa kote ulimwenguni. Maneno kama vile *rasta*, *mnati*, *ras*, *masivu* na *ire* yaliyo kwa S.E.D yamepenyezwa katika *Sheng'*.

*Rasta* ni mfuasi sugu wa midundo ya reggae aghalabu huwa na shungi la nywele lililosokotana, ufupisho wake ni *ras*. *Mnati* ni mwandani wa kikosi cha wafuasi wa reggae. *Masivu* ni kikundi kikubwa cha wafuasi wa reggae. *Ire* ni kuhisi raha baada ya kupagawa na midundo na miondoko ya muziki wa reggae. Awali maneno haya yalikuwa ya Reggae ya Wajamaika. Siku hizi yanasikika takribani kwa kila aina ya burudani, filamu, redioni na hata katika hafla za mikutano ya kisiasa na michuano ya mipira. Aidha, wasanii wa Kijamaika kama vile *Black Uhuru* wanatumia lakabu za *Sheng'*.

### 2.4.8 *Sheng*' katika usafiri wa matatu

Kihara (2006) alibainisha matumizi ya *Sheng'* katika sekta ya matatu. Alidai kuwa *Sheng'* hata huzungumzwa na watoto wachanga ambao hawajafikisha umri wa kwenda shule, vijana na wafanyakazi wa umri wa kati katika vikundi mbalimbali vya kijamii nchini Kenya. Matumizi haya mapana ya *Sheng'* yanaweza kuchangia katika ufifiaji wa matumizi ya leksimu za KS. Utafiki wa Kihara (2006), ulionyesha wazi namna *Sheng'* ilivyo lugha pendwa miongoni mwa wahudumu na abiria katika usafiri wa matatu. Mchango wa Kihara (2006), ni muhimu sana kwa utafiti huu kwa sababu unatoa picha halisi na umaarufu wa *Sheng'* katika sekta ya uchukuzi. Uzoefu mpana wa leksimu za *Sheng'* katika sajili ya matatu huenda ikawa tishio kubwa katika kufifisha KS. Hata hivyo leksimu nyingi alizobainisha bado zinadumu katika sekta hii hadi sasa.

Hali hii inatufanya tukubaliane na mengi ya matokeo ya utafiti wake. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini maneno ya S.E.D ambayo hutumika katika sekta ya matatu.

**Jedwali 23: Maneno ya S.E.D katika sekta ya matatu**

| **S.E.D** | **Kiswahili sanifu** | **Maana** |
|---|---|---|
| Trek | Kutembea | Kutembea kwa miguu |
| Tao | Mji | Sehemu za mji |
| Chapaa | Pesa | Pesa |
| Inua | Beba | Kuanzisha gari |
| *Sambaza* | Enea | Kibao kati ya vitu kwenye matatu cha watu kukalia |
| *Nyonga* | Ua | Pindua gari kuelekea lilikokuwa linatoka |
| *Uza* | Uza | Badilisha abiria kutoka gari moja hadi linguine kwa sababu gari la awali haliendi kulikokusudiwa |

Kulingana na jedwali hili maneno yaliyoandikwa kwa mlazo hayako katika S.E.D. Hii ni kwa sababu yamebuniwa juzi. Mtafiti ameyaweka hapa makusudi ili kuonyesha mfano wa namna misamiati zaidi inavyozidi kuzuka katika sekta hii. Mazoea ya matumizi ya maneno haya yanachukua nafasi ya msamiati wa KS kwa hivyo kuchangia kuyafifisha.

**2.5 Hitimisho**

Sura hii ililenga kubainisha leksimu za *Sheng'* katika S.E.D na ambazo hujitokeza katika KS. Mtafiti alitalii kwa kina sehemu tatu kuu za *Sheng'* zinazoafiki lengo hili. Kwanza, alibaini maneno ya *Sheng'* yaliyo kwa kamusi ya S.E.D na ambayo hujitokeza kwa KS. Hatua hii ilikuwa muhimu kwa sababu njia ya haraka ya kubaini matumizi ya leksimu za lugha ni kutalii kamusi zilizochapishwa. Hatua ya pili ikawa kuangazia migao mbalimbali ya maneno kisemantiki. Kusudi la kufanya hivi ni kwa sababu matumizi ya maneno katika jamii hubainika vyema yakichanganuliwa kwa misingi ya maana kusudiwa. Kigezo hiki kilitupa aina tofauti tofauti za maneno yanayojitokeza katika S.E.D na ambayo yana umaarufu wa kimatumizi katika KS. Mwisho, mtafiti alitathmini namna maneno yanayopatikana katika S.E.D hutumika katika miktadha ya kisasa. Kwa kufanya hivyo, alionyesha hatari ya baadhi ya leksimu za *Sheng'* kuwa maarufu kimatumizi kiasi kwamba zinaweza kusababisha kufifisha leksimu fulani za KS. Maneno ya kawaida ya KS yanapata maana mpya. Maana asili ya maneno mengi inasahaulika na ile mpya kukita mizizi kimatumizi. Kadhalika, dhana nyepesi na za kawaida katika mawasiliano zinaelezwa kwa kutumia maneno ya *Sheng'* na wala sio KS. Ubainishaji wa maneno ya *Sheng'* katika S.E.D na kuonyesha kuwa yanajitokeza katika KS yanatimiza lengo la kwanza la utafiti huu. Lengo hilo ni:

ubainishaji wa maneno ya *Sheng'* katika S.E.D na katika KS liliafikiwa katika sura hii. Hii ni thibitisho tosha kuwa kuna athari ya S.E.D kwa KS. Kadhalika, katika sura hii ilifaa kujibu swali la kwanza la utafiti huu ambalo ni: Ni maneno yapi yaliyojitokeza kwa *Sheng'-English Dictionary* na ambayo yapo kwa Kiswahili sanifu? Kwa mujibu wa utafiti huu, swali hili limejibiwa. Utafiti umefanikisha kuorodhesha aina mbalimbali za maneno yanayojitokeza katika S.E.D na vilevile katika KS. Maelezo ya kina kuhusu kila aina ya maneno pia yamewasilishwa. Isitoshe, maana ya kila neno linalojitokeza katika S.E.D na KS imefafanuliwa.

# SURA YA TATU

## MUUNDO WA KIFONOLOJIA WA MANENO YA *SHENG'*

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii utafiti unadhamiria kueleza miundo ya kifonolojia ya leksimu za *Sheng'*. Mtafiti alichunguza vipashio tofauti vya msimbo wa *Sheng'* na jinsi vinavyodhihirika kifonolojia. Miundo ya kifonolojia ya konsonanti za *Sheng'* pamoja na irabu imejadiliwa kwa kina. Istoshe, sifa bainifu zinazotofautisha irabu na konsonanti za *Sheng'* zimeelezwa. Aidha, miundo ya sauti katika silabi za *Sheng'* imechunguzwa. Mtafiti ametumia maneno kutoka S.E.D kueleza miundo hii. Mifano mahsusi imeshughulikiwa hasa kutoka kwa maneno ya S.E.D. Mwisho, sifa za arudhi za *Sheng'* zimejadiliwa. Sifa hizi ni shadda pamoja na toni.

### 3.2 Fonolojia ya *Sheng'*

Mgullu (1999) anaeleza fonolojia kama taaluma maalumu ya isimu ambayo kazi yake ni kuchambua mfumo wa sauti zinazotumika katika lugha fulani. Kwa mujibu wa utafiti huu, msimbo unaorejelewa katika muktadha huu ni msimbo wa *Sheng'*. Mgullu (1999) aliigawa fonolojia katika matawi makuu mawili: Fonolojia vipande sauti na fonolojia arudhi. Fonolojia vipande sauti hujishughulisha katika ubainishaji wa vipandesauti maalum katika lugha fulani. Vipande sauti hivi ni fonimu na alofoni. Kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti alijikita katika kuchunguza namna fonimu ya *Sheng'* inavyodhihirika na kuathiri KS. Kwa upande mwingine, Mgullu (1999) alieleza fonolojia arudhi kama taaluma inayoshughulika katika kuchunguza vipashio vikubwa

sana vya lugha kuliko fonimu. Vipashio hivi ni mkazo, toni, kiimbo na silabi. Utafiti huu, uliangazia zaidi namna toni na miundo ya silabi inavyojitokeza katika *Sheng'*. Hii ni kwa sababu vipande sauti hivi vinaweza kuwa na mchango mkubwa katika uundaji wa maneno na maana za maneno katika *Sheng'*.

### 3.2.1 Fonimu za *Sheng'*

Makini (2015) katika tasnifu yake ya uzamili, alifafanua fonimu kama kitengo cha sauti yoyote ya lugha inayobainishwa kimatamshi katika maneno ya lugha lengwa**.** Mgullu (1999) alitoa ufafanuzi wa sifa bainifu za fonimu. Baadhi ya sifa hizo ni kuwa kila fonimu hushiriki katika kujenga na kutofautisha maana katika jozi finyu ya neno.

Kigezo hiki kilifaa sana katika uchunguzi huu kwa sababu mtafiti aliweza kubaini namna fonimu mbalimbali zinavyoshiriki kujenga na kutofautisha maana katika msimbo wa *Sheng'*. Utafiti ulichunguza namna sauti mbalimbali za vokali na konsonanti zinavyoshiriki katika kujenga na kutofautisha maana katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Kwa mfano, neno la KS *mzee* linabadilika na kuwa *msee* katika *Sheng'*. Mfanyiko huu wa kifonolojia ni jozi mlinganuo finyu. Kikwamizo ghuna cha ufizi **/z/** kinabadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na kikwamizo cha ufizi sighuna **/s/.** Hali hii inajitokeza katika kielelezo cha mazingira yafuatayo;

**/z/**< --- >**/s/** → **/s/.** Mabadiliko haya yanatathminiwa na kihimili cha uzalishi cha nadharia ya Fonolojia Boreshi. Sauti /**s/** na **/z/** zinakuwa maumbo shindani. Sauti hizi zikiingizwa katika *Sheng'* konsonanti **/s/** inakuwa umbotokeo na kushiriki katika uundaji wa neno *msee*

Mgullu (1999) alizidi kueleza kuwa, ukibadili fonimu katika neno, maana ya neno hilo itabadilika au kupotea. Aidha, mpangilio wa fonimu kwa baadhi ya maneno ukivurugwa maana ya neno husika itabadilika au kupotea. Dai hili liliafiki uchunguzi huu kwa sababu, mtafiti aliweza kubainisha namna fonimu fulani katika baadhi ya maneno katika data ya utafiti huu inavyobadilika. Katika S.E.D tuligundua maneno kama *gwara* (iba) na *gwaya* (ogopa). Maneno haya yanakaribiana lakini fonimu **/r/** ikibadilishwa na **/y**/, maana kusudiwa huathirika. Hali hii hutokea katika mazingira ya; /**r/** /< --- >**/y/**→**/y**/. Kauli ya mwisho ya Mgullu (1999) kuhusu fonimu kuwa, kila lugha ina fonimu zake na fonimu za lugha mbili tofauti haziwezi kufanana, ilifaa sana katika uchunguzi huu.

Kama itakavyodhihirika katika maelezo yafuatayo, tuliweza kuchunguza namna fonimu mbalimbali zinavyoshiriki kuzua tofauti kati ya *Sheng'* na KS. Tuligundua kuwa fonimu za irabu **/ɛ/** na **/ɔ/** hazipatikani katika KS lakini ziko katika *Sheng'*. Kulingana na Mgullu (1999), kuna taratibu mbalimbali zinazotumiwa kutambua fonimu. Taratibu hizi ni zifuatazo: kufanana kifonetiki, jozi mlinganuo finyu, na mpishano huru. Kigezo cha fonimu kufanana kifonetiki kilitumika katika utafiti huu kuainisha sauti za irabu na konsonanti za *Sheng'*. Kutokana na data ya utafiti huu, maneno kama *banɔ* na *bakɔ* yaliainishwa kwa msingi ya kuwa na sauti ya irabu **/ɔ/.**

Irabu hii katika maneno yote mawili inafanana kifonetiki na ilisaidia katika uchunguzi huu kueleza namna fonimu za *Sheng'* zilivyo tofauti na KS. Katika data ya utafiti huu umbo la irabu **/ɔ/** na **/o/** ni alofoni**.** Kwa mujibu wa Mgullu (1999) alafoni na maumbo mbalimbali ya kiisimu ambayo hayaleti tofauti za maana katika neno. Licha ya kuwa

irabu /ɔ/ na /o/ ni tofauti, utafiti huu ulidhihirisha kuwa irabu hizi hubadilishana nafasi kwa baadhi ya maneno bila kuathiri maana kusudiwa. Hali hii huibua mfanyiko wa kifonolojia wa jozi mlinganuo finyu.

Kigezo cha jozi mlinganuo finyu kilitumiwa katika utafiti huu kueleza tofauti ndogo sana zinazojitokeza katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Mgullu (1999) alieleza jozi mlinganuo finyu kuwa, ni tofauti ndogo sana ya kifonolojia iliyopo baina ya maneno fulani. Mtafiti aliweza kugundua namna irabu **/ɔ/** na **/o/** zinavyochangia kuleta maana tofauti katika neno *bak**ɔ*** (mchezo wa vikapu) na *bak**o*** la KS linalomaanisha (kipimo cha kitanga cha mkono). Utaratibu wa mpishano huru ulitumika katika utafiti huu kubainisha baadhi ya maneno katika *Sheng'* ambayo yana fonimu moja ambayo ni tofauti lakini tofauti hizo hazisababishi tofauti katika maana. Maneno *ma**d**a* na *ma**nd**a* katika S.E.D yote yana maana sawa ya *kuua*. Tofauti inajitokeza katika sauti za silabi **/*d*/** na **/*nd*/.**

### 3.2.2 Vokali za *Sheng'* katika leksimu za S.E.D

Mwihaki (2007) alibaini kuwa *Sheng'* inazo vokali saba ambazo ni; ***/a/, /e/, /i/,*** /ɛ /, /ɔ/ na ***/u/*** kama zilivyo katika lugha nyingi za kibantu. Kiswahili kwa kawaida huwa na vokali tano ambazo ni /a/, /e/, /i/, /o/, na /u/. Hata hivyo, *Sheng'* imekopa vokali /ɛ/ *na* /ɔ/ kutoka kwa lugha za kibantu. Vokali inaweza kutumika katika mazingira yoyote ya neno, na inaweza kuambatana na konsonanti yoyote. Vokali hizi zimefafanuliwa zaidi kwa kuzingatia sehemu ya kuzitamkia na mwinuko wa ulimi katika kinywa. Kuhusu mahali pa kutamkia vokali, sehemu tatu hutumiwa kuzitofautisha kama zilivyoainishwa katika jedwali hili.

**Jedwali la 24: Vokali za *Sheng'* (Mugambi 2007)**

| **Mwinuko wa ulimi** | **Sehemu ya ulimi** | | |
|---|---|---|---|
| | **Mbele** | **Kati** | **Nyuma** |
| Juu | i | | u |
| Kati-juu | e | | o |
| Kati- chini | ɛ | | ɔ |
| Chini | | a | |

Utafiti ulitathmini aina hizi za vokali na kuweza kuzibainisha kutoka baadhi ya maneno yaliyo katika data ya utafiti huu. Vigezo vifuatavyo vilitumika:

a) **Sehemu ya mbele ya ulimi kati.**

Sehemu hii huwa na irabu **/e/.** Kwa mujibu wa Mgullu (1999), vokali hii inapotamkwa ulimi huwa mbele, sehemu ya kati juu na midomo huwa tandazwa. Vokali hii imetokea kwa maneno kama ***e**nga* ambalo lamaanisha *kujifanya huoni*. Vokali hii hutumika pamoja na sauti za konsonanti kuunda silabi mbalimbali za *Sheng'* na katika KS. Maneno kama vile *f**e**ri* na *jezi* yameundwa kwa silabi #***fe***# na #***je***# ambazo zina irabu **/e/.** Utafiti uligundua kuwa irabu hii yaweza kutumika katika silabi tamati kwa baadhi ya nomino za mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza.

Maneno kama *shond**e*** (kusanyiko la kinyesi), *shomb**e*** (mpenzi wa kiume) na *tel**e*** (runinga) yana irabi **/e/** katika silabi za tamati. Kupitia kwa mifano hii iligunduliwa kuwa, matumizi ya irabu **/e/** kuunda silabi za *Sheng'* yanakaribiana sana na jinsi ilivyo katika KS.

**b) Sehemu ya mbele ya ulimi juu.**

Vokali **/i/** hutamkiwa mbele juu. Hujitokeza kimatamshi ulimi ukiwa mbele sehemu ya juu huku midomo ikiwa katika hali tandazwa. Kutokana na data ya utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa vokali **/i/** huunda silabi huru za kwanza kwa baadhi ya maneno. Maneno kama ***i****nda* (sehemu ya viwandani) na ***i****nua (piga mtu)* zina irabu hii. Hata hivyo, kuna baadhi ya maneno yaliyokopwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza yenye sauti ya konsonanti katika silabi tamati, ambayo huchukua irabu hii. Mifano ya maneno haya ni kama vile: *set****i*** (anza), *stor****i*** (hadithi) na *stad****i*** *(*uga wa mpira). Aidha, baadhi ya mizizi ya maneno katika S.E.D imeundwa kwa vokali hii. Maneno kama *ar****i****fu* (rafiki) na *bad****i****li* (baba) yana irabu ***/i/*** kwenye mzizi.

**c) Sehemu ya kati- chini.**

Katika jedwali la 24, vokali ya kati -chini ni **/a/.** Irabu hii hudhihirika katika mazingira ya mbele chini huku midomo ikiwa imeviringwa. Katika *Sheng'* maneno kama vile ***a****juta* (vyatu), ***a****mbaa* (ondoka) na ***a****rifu* (rafiki) huanza kwa vokali hii. Kutokana na mifano hii, inadhihirika kuwa matumizi ya irabu **/a/** yanaweza kujitokeza kama silabi wazi ya irabu moja hasa ikitokea mwanzoni mwa neno. Kadhalika, silabi nyingi za *Sheng'* huambatisha irabu ***/a/***. Maneno kama *ch****a****p****a*** *(funga bao mchezoni)*, *d****a****r****a*** (papasa) na *f****a****l****a*** (mjinga) yana irabu **/a/.** Aidha, mtafiti aligundua kuwa irabu hii, yaweza kujitokeza tamati mwa neno kwa kuunda irabu ya mvuto.

Kulingana na Makini (2015), irabu ya mvuto hutokea iwapo kuna irabu moja inayofuatana katika silabi. Neno kama *vaa* (kupiga/kuchapa) limeundwa kwa mpangilio huu. Muundo wa silabi unafanana na KS lakini katika matamshi irabu ***/a/*** tamati hujitokeza kama silabi tofauti. Neno *vaa* katika *Sheng'* linakuwa na silabi mbili #***va***# na #**a#** lakini katika KS **vaa** ni silabi moja. Hali hii huchangia kuwepo kwa tofauti kati ya silabi za *Sheng'* zenye sauti ya irabu ya mvuto /**aa/** na zile za KS.

**d) Sehemu ya chini ya ulimi mbele.**

Kindija (2012) anafafanua sauti */ɛ/* kuwa, ni irabu ya nusu-chini mbele siviringo. Ikitamkwa, ulimi huwa nusu-chini na mbele kabisa katika kinywa. Mgao wa midomo katika kutamka irabu hii ni siviringo au tandazwa. Kwa mujibu wa utafiti huu, ilibainika kuwa kuna baadhi ya maneno katika S.E.D yenye irabu */ɛ/*. Maneno kama *mkalɛ* (mtu kutoka kwa jamii ya Kalenjini) na *telɛ* (runinga), huwa na irabu hii. Mtafiti alipolinganisha irabu za *Sheng'* na za KS kwa mujibu wa Mwihaki (2007), aligundua kuwa irabu */ɛ/* haiko katika KS.

Hali hii ni mojawapo ya sababu ya kuzuka kwa tofauti za kimatamshi katika baadhi ya maneno ya *Sheng'* na KS. Neno *tele* la KS lina maana ya *kujaa*. Hata hivyo katika *Sheng'* linatamkika *telɛ* na kuzua maana ya runinga. Matumizi mapana ya irabu hii katika *Sheng'* huenda yakazoeleka na kuhamishwa hadi KS. Irabu hii hudhihirika kimatamshi ulimi ukiwa mbele, sehemu ya nusu chini na midomo huwa tandazwa. Tofauti iliyopo kati ya vokali /e/ na /ɛ/ ni kuwa /e/

hutamkiwa mbele nusu juu ilhali /ɛ/ hutamkiwa sehemu ya mbele nusu chini. Kadhalika irabu /ɛ/ huwa na wakaa mrefu kuliko irabu /e/.

**e) Sehemu ya kati ya ulimi chini.**

Irabu hii hutokea kimatamshi ulimi ukiwa kati sehemu ya chini kinywani huku midomo ikiwa imetandazwa. Kwa mujibu wa utafiti huu, *Sheng'* huwa na irabu **/a/** ambayo hujitokeza kwa maneno mengi yenye asili ya kibantu. Katika baadhi ya maneno, irabu hii huweza kujitokeza kama silabi wazi mwanzoni mwa maneno. Maneno kama ***a**ndasi* (matawi ya miraa) na ***a**rifu* (rafiki) yana irabu **/a/** mwanzoni. Kuna maneno mengine ambayo irabu **/a/** huwa kwenye mzizi. Maneno kama *b**a**be* (msichana mdogo) na *d**a**ra* (papasa) yana irabu **/a/** kwenye mzizi. Isitoshe, kuna maneno mengine ya *Sheng*' ambayo irabu **/a/** hujitokeza katika silabi tamati, kwa mfano, neno *k**a**a* ***(**kufanana**)*** na *j**aa*** (kunona).

**f) Sehemu ya nyuma ya ulimi juu.**

Irabu hii hudhihirika kimatamshi ulimi ukiwa nyuma sehemu ya juu kinywani huku midomo ikiwa imeviringwa. Kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa irabu **/u/** hutumika kuunda baadhi ya silabi za maneno ya *Sheng'*. Ikitokea mwanzoni mwa neno huunda silabi wazi. Maneno kama ***u**goro* (dhahabu) na ***u**kara* (karatasi) yana irabu **/u/** inayojitokeza mwanzoni mwa neno. Kuna baadhi ya maneno ambayo irabu /**u/** hutumika katikati mwa neno. Kutokana na data ya utafiti huu, mtafiti alibainisha maneno kama *t**u**na* (lala), *t**u**pa* (nuka), *v**u**nja* (piga mtu) na *z**u**sha* (anzisha mgogoro). Maneno

haya yameundwa kwa irabu **/u/** ambayo hutumika kama sehemu ya mzizi wa neno. Kadhalika, irabu /**u/** hujitokeza katika mazingira ya tamati ya baadhi ya maneno. Maneno kama *mbuy**u*** (baba), *sug**u*** (kitu kigumu), na *zuz**u*** (mjinga) yameundwa kwa irabu **/u/** inayojitokeza katika mazingira ya tamati mwa neno.

**g) Sehemu ya nyuma ya ulimi kati-juu.**

Irabu hii hujitokeza kimatamshi ulimi ukiwa nyuma, sehemu ya nusu juu huku midomo ikiwa imeviringwa. Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, irabu **/o/** yaweza kujitokeza katika mazingira ya awali mwa neno. Silabi inayoundwa huwa ni silabi wazi. Baadhi ya maneno yaliyobainishwa yenye irabu **/o/** mwanzoni mwa meneno ni kama ***o**moka* (kuwa tajiri) na ***o**zoni* (kiwango cha juu). Aidha, yaweza kutumika katikati mwa baadhi ya maneno na kuunda mzizi wa maneno. Mtafiti alibainisha maneno kama *p**o**ri* (polisi), *sh**o**mbe* (mpenzi wa kiume), *sh**o**na* (rithika) na *sh**o**nde* (kusanyiko la kinyesi). Aidha, aliweza kugundua kuwa irabu **/o/** yaweza kutumika katika mazingira ya tamati mwa baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Utafiti ulibainsha maneno kama *bang**o*** (shilingi moja), na *finy**o*** (ongeza uongo).

**h) Sehemu ya nyuma ya ulimi kati chini.**

Irabu **/ɔ/** hutumika katika mazingira ya sehemu ya nyuma ya kinywa, ulimi ukiwa kati chini. Kwa mujibu wa utafiti huu, maneno kama *ban**ɔ*** (aina fulani ya jiwe)) na *bak**ɔ*** (mchezo wa mpira wa vikapu) yana irabu hii. Irabu hii huzua tofauti kubwa kati ya *Sheng'* na KS. Sababu kuu ni kuwa, irabu hii haipatikani katika KS. Isitoshe, inapotumika katika *Sheng'* huzua toni katika matamshi ya


maneno husika. Maelezo haya yanaweza kuwasilishwa vyema kupitia kwa jedwali lifuatalo.

**Jedwali 25: Maneno yanayotokana na vokali za *Sheng'* katika S.E.D**

| Fonimu | Vokali | Maneno |
|---|---|---|
| /a/ | a | arifu |
| /e/ | e | enga |
| /ɛ/ | ɛ | mkalɛ |
| /i/ | i | inda |
| /o/ | o | omoka |
| /ɔ/ | ɔ | pepo |
| /u/ | u | ukara |

Kando na kutoa mifano ya maneno yanayoundwa kutoka kwa irabu za *Sheng',* ni muhimu kuonyesha sehemu katika ulimi ambapo sauti za irabu hutamkwa. Kielelezo kifuatacho kinatupa muhtasari wa sehemu katika ulimi zinazohusika katika kutamka irabu za *Sheng'*.

**Kielelezo 1: Mchoro wa IPA wa vokali za *Sheng'***




Kutokana na kielelezo hiki, ilidhihirika kuwa msimbo wa *Sheng'* una vokali tatu za mbele ambazo ni; **/i/, /e/** na **/ɛ/**; moja ni ya kati ambayo ni **/a/** na tatu za nyuma ambazo

ni **/u/**, **/o/** na **/ɔ/**. Sifa hizi za mbele, kati na nyuma zinatambua ulalo wa ulimi wa mzungumzaji wakati wa matamshi. Kutokana na mwinuko wa ulimi, msimbo wa *Sheng'* unadhihirisha vokali tatu za juu **/i/, /e/** na **/u/.** Vokali za kati nazo ni; **/ɛ/, /o/**na **/ɔ/,** vokali ya chini kabisa ni **/a/.** Irabu **/ɛ/,** na **/ɔ/** katika baadhi ya maneno ya *Sheng'* zinaonyesha tofauti kubwa sana ya kifonolojia kati ya *Sheng'* na KS. Irabu **/ɛ/** pia hutamkwa hali ya midomo ikiwa tandazwa. Irabu **/ɔ/** nayo hutamkwa midomo ikiwa katika umbo viringwa. Kuna uwezekano kuwa wazungumzaji wa *Sheng'* wanaweza kuhamisha irabu hizi kimatamshi hadi kuingizwa katika KS.

### 3.2.2.1 Fonimu /ɛ/ katika *Sheng'*

Mtafiti aligundua kuwa baadhi ya maneno katika *Sheng'* huwa na silabi yenye irabu **/ɛ/.** Baadhi ya maneno yameorodheshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 26: Fonimu /ɛ/ katika *Sheng'***

| **Maneno katika S.E.D.** | **Maana** |
|---|---|
| *Babɛ* | Msichana mdogo |
| Gafɛ | Kahawa |
| Palɛ | Rafiki mkuu |
| Kalɛ | Jamii ya Wakalenjin |
| Telɛ | Runinga |

Irabu /ɛ/ haijitokezi katika KS (Mugambi, 2007). Ikitumika katika *Sheng'* hubadilisha matamshi ya maneno kwa kubadili kidatu kinachozua toni katika *Sheng'*. Kuzuka kwa maneno mengi katika *Sheng'* yenye irabu **/ɛ/** huenda kukazua athari za kifonolojia kwa KS. Maneno ya KS yasiyokuwa na toni huenda yakaanza kutamkika yakiwa na toni. Neno kama *kale* (zamani) la KS laweza kutamkika visivyo na kuwa *kalɛ* (jamii ya Kalenjin).

#### 3.2.2.2 Fonimu /ɔ/ katika *Sheng'*

Kwa mujibu wa utafiti huu, iligunduliwa kuwa irabu **/ɔ/** hutokana na maneno ya mkopo kutoka Kiingereza na lugha za kienyeji nchini Kenya. Kindija (2012) anaibainisha kuwa irabu **/ɔ/** ni ya nusu-chini ya nyuma mviringo. Inapotamkwa, ulimi huwa katikati ya irabu ya chini na irabu ya kati. Kadhalika, ulimi huwa sehemu ya nyuma kabisa kinywani huku mgao wa midomo ukiwa katika umbo la mviringo. Mtafiti aligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* yaliyokopwa kutoka Kiingereza na kufupishwa, silabi za mwisho huwa na irabu hii.

**Jedwali 27: Fonimu /ɔ/ katika *Sheng'***

| **Neno** | **Lugha changizi** | **Maana** |
|---|---|---|
| Bakɔ | Kiingereza | Mpira wa vikapu |
| Banɔ | Kiingereza | Adhabu |
| Bayɔ | Kiingereza | Somo la viumbe hai |
| Taɔ | Kiingereza | Sehemu ya mji |
| Pangɔ | Mtaa wa Pangani jijini Nairobi | Nafasi kubwa katika miti/majabali |

Kutokana na maelezo haya, irabu **/ɔ/** inajitokeza wazi katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Irabu hii haiko katika KS kwa sababu huzalika kwa wingi kutokana na lugha ya Kiingereza baada ya kudondosha silabi tamati katika neno. Mtindo huu wa kufupisha maneno ya mkopo kutoka Kiingereza kwa kudondosha silabi tamati za neno hauko katika KS. Mtaa wa *Pangani* katika KS unabaki tu kuwa *Pangani* lakini katika *Sheng'* neno hili linafupishwa na kuwa *Pang***ɔ**. Hali hii husababisha maneno kutamkwa kwa kidatu cha juu ambacho huzalisha toni. Kindija (2012) anaeleza kuwa, lugha nyingi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara huwa na toni. Ni lugha chache tu zisizo na toni ikiwemo lugha ya KS. Kidatu kinachojitokeza katika matamshi ya baadhi ya maneno yenye irabu **/ɔ/** huzua toni ya juu katika matamshi. Toni imepenyezwa katika

*Sheng'* kutokana na maneno ya mkopo ambayo yatokana na lugha za fonimu **/ɔ/** na **/ɛ/.** Kwa mujibu wa Kindija (2012), aina hii ya toni ni ya kupanda. Huanzia kidatu cha kati na kupanda hadi kidatu cha juu.

Githiora (2018:93) anaeleza kuwa lugha ya Dholuo huwa na mfumo wa kiambishi **/o/** au **/ɔ/.** Kiambishi hiki huwa kinapachikwa mwanzoni au mwishoni mwa nomino za pekee hasa zinazorejelea mahali au watu mahsusi. Githiora (2018) alitoa mifano ya maneno ya Dholuo kama odukɔɔ (duka), *Oriabaa* (mtaa wa Kariobangi mjini Nairobi), na *Ɔkuyɔɔ* (mtu kutoka jamii ya Gikuyu). Mfumo huu wa sauti ndio uliokopwa na kuingizwa katika msimbo wa *Sheng'*. Nomino za kipekee zinazorejelea mahali katika *Sheng'* zimechukua mkondo huu.

Katika data ya utafiti huu maneno kama, *Dagɔ* (mtaa wa Dagorreti) na *Pangɔ* (mtaa wa Pangani) ni baadhi ya mifano. Huenda matumizi makubwa ya irabu /**ɔ/** miongoni mwa vijana yaweza kuhamishwa hadi katika KS. Hali hii ikiendelea basi maneno yenye irabu **/ɔ/** yaweza kuhamishwa kwa kupata matumizi katika KS. Hali hii itachangia katika kupungua kwa matumizi ya KS.

### 3.2.2.3 Vokali /i/ na /e/ katika *Sheng'*

Katika utafiti huu, mtafiti aligundua baadhi ya maneno ya *Sheng'* ambayo huchukua sauti ya irabu ***/i/*** au ***/e/*** katika tamati mwa maneno. Maneno mengi ni yale yaliyokopwa kutoka Kiingereza, kama inavyoonyeshwa katika jedwali 28.

**Jedwali 28: Maneno mkopo ya *Sheng'* katika S.E.D**

| **Kiingereza** | ***Sheng'*** | **Maana** |
|---|---|---|
| Dot | Doti | Kuongea visivyo |
| Gang | Gange | Kazi ya kuajiriwa |
| Jersy | Jezi | Sare ya shule |
| Maize | Mei | Mahindi |
| Brandy | Brandi | Mpya |

Maneno ya Kiingereza yanayoishia kwa konsonanti hupachikwa irabu ili kuafiki muundo wa silabi wa *Sheng'*. Kwa mujibu wa Mwihaki (2007), silabi nyingi za *Sheng'* huchukua muundo wa KV. Neno *dot* (alama) linapachikwa irabu **/i/** na kuwa *dot**i*** (kuongea visivyo). Aidha, *gang* (kikosi cha majambazi) nalo linapachikwa irabu **/e/** na kuwa *gang**e***. Hata hivyo, kuna baadhi ya konsonanti ambazo hulazimika kudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu. Katika neno *brand**y***, konsonanti */**y**/* inatolewa na mahali pake kuchukuliwa na irabu */**i**/.* Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, muundo wa silabi wa KV unachukuliwa kama kihimili cha shartizuizi. Muundo huu unaamua namna silabi zinazotokana na maneno ya mkopo zinavyofaa kujitokeza katika *Sheng'*. Silabi #***ndy#*** katika neno *bra**ndy*** linakiuka shartizuizi hili. Inalazimika konsonanti /**y**/ idondoshwe na mahali pake pachukuliwe na irabu /**i**/. Kwa hivyo silabi inayozalika inakuwa #**ndi#**. Neno mpya linaloundwa na kuwa umbotokeo linakuwa *bra**ndi***. Kwa mujibu wa data ya jedwali la 28 kuhusu maneno ya mkopo, mtafiti ameangazia namna irabu /**i**/ na /**e**/ zinavyochangia katika uundaji wa leksimu mpya. Neno asili linalazimika kuchukua irabu hizi katika silabi za tamati mwa neno. Hata hivyo, baadhi ya maneno yanalazimika kuwa na mpangilio wa silabi wa KV. Kutokana na data katika S.E.D, mpangilio huu hujitokeza kwa silabi za mwisho katika baadhi ya maneno.

Mfano mzuri unaweza kuonekana kutokana na maneno ya Kiingereza *set* na *plan*. Maneno haya yanachukua irabu ***/i/*** katika silabi ya mwisho na kuwa *seti* (anza) na *plani* (makubaliano) mtawalia. Katika maneno haya, silabi za mwisho zinabadilika kutoka kuwa konsonanti pekee (K) hadi kuwa KV. Konsonanti ***/t/*** katika *se**t*** inatiwa irabu ***/i/*** na kuwa #***ti*#.**

Vilevile, konsonanti **/n/** katika neno *pla**n*** inatiwa irabu ***/i/*** na kuwa ***#ni#.*** Mpangilio wa silabi KV linakuwa shartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Badala ya silabi za maneno haya kuishia kwa konsonanti, zinaishia kwa irabu kwa kuunda maneno *seti* na *plani* mtawalia. Aidha, neno la Kiingereza *brandy* lenye konsonanti /***y*/** kwa silabi ya mwisho**, /y/** inadondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu ***/i***/. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, mhimili wa utathmini unatumika kuamua umbo la silabi itakayoundwa baada ya *Sheng'* kukopa baadhi ya maneno. Maneno ya *Sheng'* yanayoishia kwa konsonanti pekee yanalazimika kupachikwa irabu ili yaafiki muundo wa silabi wa KI.

### 3.2.2.4 Vokali ndefu katika *Sheng'*.

Ferarri (2014) alibainisha kuwepo kwa vokali fupi na vokali ndefu katika msimbo wa *Sheng'*. Vokali ndefu hutokea ikiwa irabu moja itajirudia kimfuatano katika silabi. Vokali ndefu ndiyo inayobainishwa na Makini (2015) kuwa irabu ya mvuto. Neno la *Sheng' ukoo* (nzuri, muhimu) lina irabu **/o/** inayotokea mara mbili kwa mfululizo. Vokali hizi huwa huru kama vokali sahili yaani hazifungwi na mazingira ya kifonetiki. Kwa upande mwingine KS huwa tu na vokali fupi. Hata iwapo kuna mfuatano wa irabu katika sehemu ya tamati mwa neno, irabu ya mwisho hutamkika tofauti na

kuunda silabi mahsusi. Maneno kama *paa*, *kaa* na *twaa* huchukua umbo hili. Kwa mujibu wa utafiti huu uvutaji wa silabi hufanya *Sheng'* kuwa tofauti na KS.

### 3.2.3 Konsonanti za *Sheng'*

Mwihaki (2007) na Mugambi (2007) walieleza kuwa konsonanti za *Sheng'* hubainishwa kwa kutumia sifa bainifu kama vile za kimatamshi, kiakustika au kimasikizi. Mgullu (1999) alieleza kuwa, konsonanti huainishwa kwa kuzingatia namna zinavyotamkwa. Katika KS Mgullu (1999) alibainisha konsonanti 24. Naye Mwihaki (2007) akatambua konsonanti 28 katika msimbo wa *Sheng'*. Fonimu za konsonanti za *Sheng'* ni: /b/ /c/ /d/ /f/ /g/ /j/ /k/ /l/ /m/ mb/ /n/ /nd/ /ɲʃ/ /nt/ / ŋ/ /nŋ/ /ð/ /ɲ/ /p/ /r/ /s/ /s/ /t/ /ts/ /θ/ /w/ /v/ /z/. Konsonanti hizi zaweza kuainishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 29: Konsonanti za *Sheng'* (Mwihaki 2007)**

| **Jinsi ya kutamka** | | **Mahali pa kutamkia** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Midomoni** | **Menoni** | **Ufizi** | **Burutioni** | **Kaakaa laini** | **kooni** |
| Vipasuo | Ghuna | b, mb | | d | | g | |
| | Sighuna | p | | t/ nt | | k, c | |
| Vizuiwa | Ghuna | | | | j | | |
| | Sighuna | | | | ð | | |
| Vikwaruzo | Ghuna | v | ð | z | | | |
| | Sighuna | f | θ | S, ts | Š | | |
| Nazali | Ghuna | | m | | n | ɲ | ɳ |
| | Sighuna | | | | | | |
| Vilainisho | Ghuna | | | l, r | | | |
| Viyeyusho | Ghuna | | | | | | |
| | Sighuna | | | | | y | w |

Githinji (2022) alikubaliana pakubwa na uainishaji huu. Alianisha konsonanti 34 za *Sheng* kama zinavyojitokeza katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 30. Konsonanti za *Sheng'*: Githinji (2022).**

| | Midomo | meno | midomo na meno | ufizi | kaakaa gumu | kaakaa laini | glotta |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vipasuo | p, $^{m}$p<br>b, mb | | | t, $^{n}$t<br>d, nd | | k, $^{n}$k<br>g, $^{n}$g | |
| Vikwamizo | | ð | f, v | s, $^{n}$s, z<br>$^{n}$z, ʃ, $^{n}$ʃ | | | h |
| Vizuio | | | | | c, $^{n}$c<br>ɟ, $^{n}$ɟ | | |
| Kwamizo | | | | | | | |
| nazali | m | | | n | | ɲ, ŋ | |
| likwidi | | | | l, r | | | |
| viyeyusho | w | | | | j | | |

Mtafiti alipolinganisha konsonanti za *Sheng'* na za KS kwa mujibu wa Mgullu (1999) na kisha Mwihaki (2007) pamoja na Githinji (2022), alibaini kuwa kuna konsonanti za *Sheng'* ambazo hazipatikani katika KS nazo ni*:* *nt*, *ts*, $^{m}$p' $^{n}$t, $^{n}$κ, $^{n}$c, $^{n}$g, $^{n}$s, $^{n}$z na *c*. Kwa mfano, konsonanti za mpumuo $^{m}$p' $^{n}$t, $^{n}$κ, $^{n}$c, $^{n}$g, $^{n}$s, $^{n}$z zinatokana na maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, katika data ya utafiti huu, sauti hizi hazikutokea kwa sababu maneno yenye sauti hizi huswahilishwa kabla ya kupenyezwa katika KS. Konsonanti hizi nyingi ni zile zinazotokana na maneno ya mkopo hasa kutoka lugha ya Kiingereza. Githinji (2022) alidokeza kuwa, *Sheng'* inapokopa maneno kutoka lugha zingine hukopa vile vile na mkururo wa kifonolojia wa maneno husika. Mtafiti aligundua maneno yafuatayo kutoka S.E.D ambayo yameundwa kwa sauti za konsonanti hizi.

**Jedwali 31: Konsonanti za *Sheng'* katika S.E.D ambazo hazipatikani katika KS**

| **Neno** | **Konsonanti** | **Maana** |
|---|---|---|
| Cha**nt**i | *nt* | Kucheza densi kwa haraka. |
| Tukone**c**t | *c* | Tupange kukutana. |
| Ja**nt**a | *nt* | Kazi ambayo mtu ameajiriwa kufanya |
| A**nt**i | *nt* | Mwanamke wa heshima |
| Chi**nt**u | *nt* | Msichana mdogo |

Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, ilibainika kuwa konsonanti *nt, ts*, $^{m}p$' $^{n}t$, $^{n}κ$, $^{n}c$, $^{n}g$, $^{n}s$, $^{n}z$ na *c*, hazipatikani katika KS. Licha ya kuwa (Mugambi 2007) na Githinji (2022) walibainisha sauti hizi, mtafiti hakupata maneno yanayoundwa na konsonanti hizi katika KS. Sababu kuu huenda ikawa wachapishaji wa KS huhofia kukiuka muundo wa silabi za KS. Hata hivyo, licha ya maneno haya kuwa katika S.E.D, hayajajitokeza katika machapisho ya KS. Uchanganuzi wa fonimu za *Sheng'* umedhihirisha kuwa vokali na konsonanti kwa ujumla huchukua maumbo na miundo tofauti. Uhusiano wa vokali na konsonanti utazidi kujitokeza katika uchanganuzi ufuatao wa ruwaza za sauti katika silabi. Sauti hizi zitachangia katika utafiti huu kwa sababu zitatumika kuonyesha namna fonolojia ya *Sheng'* ilivyo tofauti na KS. Tofauti hizi kadhalika, zaonyesha uwezekano wa fonimu za *Sheng'* kuathiri KS.

### 3.3 Silabi za Sheng'

Baada ya kuchanganua fonimu za *Sheng'* mtafiti aliona kuwa, ni vyema kutathmini namna fonimu hizi huunda silabi za *Sheng'*. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), fonimu zinapokaa pamoja hujenga silabi ambazo huweza kutamkwa kama kitu kimoja. Kila lugha huwa na muundo wake wa silabi.

Kwa hivyo, kutokana na maelezo haya ya Mgullu (1999), msimbo wa *Sheng'* vilevile una miundo yake mbalimbali ya silabi. Kwanza, utafiti ulirejelea maelezo ya Mgullu (1999) na kuzigawa silabi za *Sheng'* katika makundi mawili; silabi funge na silabi wazi. Silabi funge kwa mujibu wa Mgullu (1999), ni zile ambazo huishia kwa konsonanti. Matamshi ya silabi funge hukatika ghafla. Silabi wazi ni zile ambazo huishia kwa irabu. Zinapotamkwa matamshi hayakatiki kwa haraka au ghafla.

Makini (2015) katika tasnifu yake ya uzamili, alieleza kuwa silabi wazi ni zile ambazo hazina kifungio. Silabi za aina hii kwa kawaida huwa na vokali mwishoni ambayo hujenga kilele cha silabi hiyo. Baada ya kugawa silabi katika aina mbili kuu, Mgullu (1999), aliweza kubainisha aina saba kuu za miundo ya silabi za KS. Nazo ni: konsonanti irabu (KI), irabu pekee (I), konsonanti pekee (K), konsonanti konsonanti irabu (KKI), konsonanti, nusu irabu, irabu (K$\frac{1}{2}$II), konsonanti konsonanti, nusu irabu, konsonanti (KK$\frac{1}{2}$II), na mwishowe silabi funge.

Uainishaji huu wa Mgullu (1999), ulifaa sana katika utafiti huu kwa sababu ulitumika kulinganisha miundo ya silabi za KS na miundo ya silabi za *Sheng'* ilivyobainishwa na Mwihaki (2007). Aidha, miundo hii ya silabi za KS imechukuliwa kama mashartizuizi kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi. Kila neno la KS lazima lichukue muundo huu wa silabi. Maneno ambayo yanakiuka utaratibu wa muundo huu yanatupiliwa mbali. Kwa hivyo, hayawezi kukubalika katika KS kama umbotokeo. Maneno mengi ya *Sheng'* huundwa kwa silabi wazi. Utafiti uliweza kubainisha aina hizi za silabi katika data ya utafiti huu.

**Jedwali 32: Silabi funge na silabi wazi katika S.E.D**

| Maneno katika S.E.D. | Lugha changizi | Magao wa silabi | Aina ya silabi |
|---|---|---|---|
| Kinda | Kiswahili | #Ki$nda# | Silabi wazi, silabi wazi. |
| Kuli | Kiswahili | #Ku$li # | Silabi wazi, silabi wazi |
| Plani | Kiingereza | #Pla$ni# | Siilabi wazi, silabi wazi. |
| Stadi | Kiingereza | #Sta$di# | Silabi wazi, silabi wazi. |
| Stori | Kiingereza | #Sto$ri# | Silabi wazi, silabi wazi. |
| Maskani | Kiswahili | #Mas$ka$ni# | Silabi funge, silabi wazi, silabi wazi. |

Kutokana na maneno yaliyo katika jedwali hili, mtafiti aligundua kuwa maneno mengi ya *Sheng'* huundwa kwa silabi wazi. Hata maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiingereza, na yanayoishia kwa silabi ya konsonanti tu, hulazimika kuchukua irabu na kuwa silabi wazi. Huenda sababu kuu ni kufanya matamshi ya silabi hizi yaafikiane na muundo wa KI unaojitokeza kwa wingi katika silabi za KS na lugha za Kibantu. Mtafiti alitumia uainishaji wa Mwihaki (2007) na Githinji (2022), kubainisha aina tofauti za silabi za *Sheng'.* Silabi hizi ni: KI, KIK, I, N, IK na KKI. Mifano imetolewa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 33: Miundo ya silabi za *Sheng'***

| Muundo wa silabi za *Sheng'* | Neno katika S.E.D. | Maana |
|---|---|---|
| KI, | **#Ja**&ka# | Mtu kutoka jamii ya Wajaluo |
| KIK | **#Mas$**kani # | Chumba cha kujificha |
| I | **#O**$na# | Piga kofi |
| K | **#M**$zizi# | Mmea wa kulevya |
| IK | **#Ar**$me# | Wanajeshi |
| KKI, | **#Bra**$ndi# | Mpya |

Githiora (2018) anaunga mkono dai hili kwa kuonyesha kuwa sauti ***/sh/*** na ***/ch/*** hujitokeza kwa wingi sana kama kiambishi tamati kwa maneno mengi ya *Sheng'*. Maneno kama *odu**sh*** kwa maana ya *jiwe* na *Kibi**ch*** kwa maana ya *Kibera* huchukua umbo hili.

Inaaminika kuwa matamshi ya irabu huwa hayakatiki kwa haraka kama yale ya konsonanti na kwa hali kama hiyo silabi wazi huonekana kama ipo huru au wazi zaidi. Hata hivyo, kwa mujibu wa data ya utafiti huu iligunduliwa kuwa maneno ya S.E.D yanayopatikana katika KS hulazimika kuchukua irabu kwa silabi zinazoisha kwa konsonanti. Hali hii hufanya silabi nyingi za *sheng*' kuwa wazi ilhali umbo asili ni silabi funge. Kama ilivyofafanuliwa pale juu, neno kama *seti* latokana na *set* la Kiinegereza. Konsonanti ***/t/*** inaambatanishwa irabu ***/i/*** na kubadili na kuunda silabi wazi. Aidha, maneno ya Kiingereza *plan* na *dot* yanachukua umbo la silabi wazi na kuwa *plan**i*** na *dot**i*** mtawalia. Hata hivyo, mtafiti alipochunguza S.E.D kwa makini alibainisha maneno mengi ya *Sheng'* ambayo yana silabi funge. Jedwali lifuatalo linadhihirisha mifano ya maneno hayo:

**Jedwali 34: Silabi funge za *Sheng'* katika S.E.D**

| **Neno** | **Silabi funge** | **Maana** |
|---|---|---|
| Baksi | $bak$(KIK) | kutulia/kupumzika |
| Beksi | $bek$(KIK) | shilingi moja |
| Bangla | $bang$(KIK) | Mtaa wa Kariobangi |
| Boksa | $bok$ (KIK) | Msichana wa chuo kikuu |
| Fasta | $fas$ (KIK) | Harakisha |

### 3.3.1 Miundo ya silabi za *Sheng'*

Mwihaki (2007) alibaini miundo saba mikuu ya silabi katika *Sheng'*; KI, KIK, I, N, IK, KKI, na KIKK. Utafiti huu ulipolinganisha miundo hii ya silabi na ile iliyodokezwa na Mgullu (1999) iligunduliwa kuwa, kuna uwiano mkubwa kati ya silabi za *Sheng'* na za KS. Mgullu (1999) pia alibainisha miundo saba ya silabi katika KS. Nayo ni: KI (konsonanti irabu), I (irabu pekee), K (konsonanti pekee), KKI (konsonanti konsonanti irabu), K$\frac{1}{2}$II (konsonanti, nusu irabu konsonanti), KK$\frac{1}{2}$II (konsonanti konsonanti, nusu irabu konsonanti) na silabi funge. Mgullu (1999:77) anaeleza silabi funge kuwa ni silabi inayoishia kwa konsonanti. Silabi hizi katika KS hutokana na maneno ya mkopo. Baadhi ya maneno yaliyobainishwa na Mgullu (1999:77) ni: ***lab****da*, ***Al****hamisi*, ***il****hali*, ***daf****tari* na ***ink****shafi*. Katika data ya utafiti huu, mtafiti amebainisha maneno kama ***mas****kani* na ***shaf****ti* ambayo pia huwa na silabi funge.

Uchunguzi huu, uligundua kuwa nomino za *Sheng'* ambazo hukopwa kutoka lugha zingine ambazo huwa na miundo ya silabi tofauti na *Sheng'* kama alivyoainisha Mwihaki (2007), hubadilishwa ili kuwiana na muundo wa silabi za KS. Iraki (2004) alitoa mfano wa neno la Kihindi *chokra* (watoto wanaorandaranda mitaani). Katika *Sheng'* mfumo wa sauti unabadilishwa na kuwa *chokora*. Silabi zake zinachukua umbo la KVKV. Maneno mengi ya *Sheng'* huchukua mkondo huu.

#### 3.3.1.1 Miundo ya silabi za nomino za *sheng'*.

Utafiti ulipochunguza kamusi ya S.E.D uliweza kubainisha nomino zenye miundo mbalimbali ya silabi. Baadhi ni kama ifuatayo.

1. **Muundo wa KI (konsonanti irabu)**

   Mtafiti aligundua kuwa, nomino nyingi zenye silabi za muundo wa **KI** zilikopwa kutoka KS au lugha za Kibantu. Lugha nyingi za Kibantu huwa na silabi wazi. Mifano ya nomino alizobainisha ni: *hara* (kuelewa, kukosa pesa*),* *jaka* (mtu wa jamii ya Wajaluo), *kago* (vitu vya thamana) na *kale* (mtu kutoka jamii ya Kalenjini).

2. **Muundo wa KIK (konsonanti konsonanti irabu)**

   Hizi ni nomino zenye silabi ambazo irabu huwa katikati mwa konsonanti mbili. Utafiti ulipolinganisha muundo huu wa silabi na ule wa KS kama alivyodokeza Mgullu (1999), uligundua nomino chache za muundo huu wa silabi katika data ya utafiti. Nomino ***mas****kani* (chumba cha kujificha) imeundwa kwa silabi #**mas#,** ambayo ina mpangilio wa **KIK.**

   Istoshe, nomino ***shaf****ti* (mkoba) ina silabi **shaf-** ambayo inaafiki muundo wa silabi wa **KIK.**

3. **Muundo wa I (irabu pekee kwenye silabi)**

   Utafiti uligundua kuwa irabu ***/i/*** yaweza kutokea kama silabi mwanzoni mwa baadhi ya nomino. Katika data ya utafiti huu, nomino ***i****nda* (sehemu ya viwandani), ina silabi ***/i/*** ambayo inajitokeza mwanzoni mwa nomino.

Hata hivyo, baadhi ya nomino, irabu ***/i/*** ilidhihirika kutokea kama silabi ya irabu pekee katika mazingira ya mwishoni mwa nomino. Nomino kama *me**i*** (mahindi) ina silabi ya irabu ***/i/*** katika mwisho wa nomino.

**4. Muundo wa K (konsonanti pekee kwenye silabi)**

Kama ilivyo katika KS *Sheng'* pia huwa na konsonanti ambazo zinaweza kuwa silabi. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), KS huwa na konsonanti mbili tu ambazo zinaweza tumika kama silabi. Nazo ni **/m**/ na **/n/**. Aina hizi za silabi pia hujitokeza katika *Sheng'*. Hata hivyo, utafiti ulibainisha kuwa baadhi ya nomino zilizokopwa kutoka lugha ya Kiingereza huwa na silabi ya konsonanti pekee. Ingawa aina hii ya nomino ziko katika S.E.D hazijitokezi katika KS. Huenda sababu ikawa zinakiuka muundo wa silabi za KS jinsi alivyoeleza Mgullu (1999) kuwa silabi nyingi za KS huishia kwa irabu. Kutokana na data ya utafiti huu, utafiti ulibainisha nomino zifuatazo.

**Jedwali 35: Nomino zenye muundo wa konsonanti pekee kwenye silabi.**

| **Nomino katika S.E.D.** | **Silabi ya konsonanti** | **Maana** |
|---|---|---|
| **M**kale | #m# | Jamii ya wakalenjini |
| **M**taa | #m# | Town |
| **M**tambo | #m# | Saa ya mkono/ gari |
| **M**tumba | #m# | Nguo kuukuu |
| **M**zubao | #m# | Changanyikiwa akili |
| **N**dusi | #n# | Mbwa |

Hata hivyo, utafiti uligundua kuwa silabi za nomino nyingi za *Sheng'* huchukua muundo wa KI kama ilivyo katika KS. Muundo huu wa silabi unakuwa kigezo kinachotumika kama shartizuizi kuamua ni umbo gani la nomino litaundwa katika *Sheng'* baada ya kukopwa kutoka lugha zingine. Kwa mujibu wa uchambuzi wa data ya utafiti huu, nomino ya Kiingereza kama *dot* (alama) inabadilishwa na kuwa *doti* (kuongea visivyo). Kuna nomino za Kiingereza ambazo hushia kwa konsonanti. Sauti ya konsonanti hupachikwa sauti ya irabu ili kufanya muundo wa silabi uwiane na wa KS.

Nomino *plan,* kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi linakuwa umboghafi. Nomino hii ina silabi ***-n*** ambayo inajitokeza kama konsonanti pekee. Inalazimika kuchukuwa irabu /i/ na kuwa #***ni#***. Nomino inayoundwa inakuwa *plani*, kwa hivyo inakuwa umbotokeo. Kanuni hii inatimiza mhimili wa uzalishi kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi. Kadhalika utafiti uligundua kuwa nomino nyingi za *Sheng'* zilizo na silabi inayoisha kwa konsonanti pekee hazijapata nafasi katika machapisho ya KS. Hii ni kwa sababu silabi nyingi za KS hasa zinazojitokeza mwishoni mwa nomino huishia kwa irabu na wala sio konsonanti.

Mgullu (1999) alieleza kuwa KS huziruhusu konsonsnti chache kuwa silabi. Hata hivyo konsonanti hizo ni mbili tu. Nazo ni **/m/** na **/n/**. Kwa mujibu wa maelezo haya ya Mgullu (1999), KS hakiwezi kukubali nomino za konsonanti pekee hasa zikitokea katika mazingira ya tamati mwa nomino. Hili ni shartizuizi kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi. Silabi za konsonanti pekee zikitokea katika mwisho wa nomino za KS lazima zikuwe irabu kabla ya kuamliwa kuwa umbotokeo. Hali hii ndio

iliyosababisha nomino zilizogunduliwa katika S.E.D kama: *rait* (ngumi), *red* (noti ya shilingi mia moja), *shan* (kujua mengi) *shiz* (kutazama), *ros* (mfalme) na *ruuts* (muziki wa reggae) kutojitokeza katika KS. Huenda ni kwa sababu nomino nyingi ya KS huchukua silabi zenye muundo wa KI.

### 3.3.1.2 Silabi za vitenzi vya *Sheng'*

Vitenzi vingi vya *Sheng'* hukopwa kutoka kwa lugha zingine. Baadhi hutokana na vitenzi vya KS, lugha za Kibantu na Kiingereza. Kama ilivyo katika KS mtafiti aligundua kuwa, baadhi ya vitenzi huchukua silabi #***ku#*** kama kiambishi awali kabla ya mzizi. Alibainisha mifano kutoka S.E.D kama inavyoonyeshwa katika jedwali 36.

**Jedwali 36: Vitenzi katika *Sheng'***

| **Kitenzi** | **Kiambishi ku** | **Maana** |
|---|---|---|
| Manda | **Ku**manda | Kuua |
| Manga | **Ku**manga | Kula chakula |
| Dinda | **Ku**dinda | Kataa kwa kiburi |
| Sanya | **Ku**sanya | Iba |
| Mada | **Ku**manda | ua |
| Choma | **Ku**jichoma | Kuanzisha mradi halafu ushindwae kukamilika |
| Sanya | **Ku**sanya | iba |
| Seti | **Ku**jiseti | Kuwa tayari |

Jedwali hili la vitenzi katika *Sheng'* linaonyesha namna vitenzi huchukua kiambishi #***ku#*** katika kauli ya kutenda kama kiambishi awali. Muundo huu wa silabi unakaribiana sana na KS. Hata hivyo, katika S.E.D mtafiti aligundua kuwa baadhi ya vitenzi vilivyokopwa kutoka Kiingereza huhifadhi umbo lake asili kabla ya kuchukua silabi #***ku#***. Kitenzi *seti* (kuwa tayari) kinatokana na kitenzi cha Kiingereza *set* chenye maana pia ya *kuandaa mpangilio*. Kinavyoingizwa katika *Sheng'* umbo la silabi

linabadilishwa ili kuafiki mpangilio wa silabi za *Sheng'* za KI. Kwa hivyo badala ya kuandika *kujise****t,*** kitenzi kinabadilishwa na kuwa *kujise****ti***. Mpangilio huu wa silabi za *Sheng'* unatimiza mhimili wa shartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Hii ni kwa sababu kuwepo kwa irabu katika silabi ni sharti ambalo yafaa litimizwe.

Muundo wa silabi za *Sheng'* wa KI unakuwa kigezo cha kuamua ni umbo gani la silabi linakubaliwa. Katika muktadha huu, kitenzi *kujise****t*** linakuwa na silabi ya konsonanti pekee katika tamati mwa kitenzi. Inabidi irabu ***/i/*** iongezwe kwa konsonanti ***/t/*** na kuunda silabi ya muundo wa **KI** ambayo ni ***#ti#***. Kitenzi *kujise****ti*** kinakuwa umbotokeo kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi. Vitenzi vya KS kama ***ku****la*, ***ku****nywa* au ***ku****cheza* huchukua utaratibu huu. Hata hivyo silabi #***ku#*** hupachikwa kwa vitenzi vya mkopo bila kubadilisha sauti za silabi ili kuafiki mfumo wa KS. Kitenzi cha Kiingereza kama vile *dead* (kufa) kinakuwa ***ku****dedi* (kukufa). Kuna baadhi ya mifumo mingine ya vitenzi hasa vilivyokopwa kutoka Kiingereza ambavyo havijachapishwa katika S.E.D. Vitenzi vilivyohifadhi maumbo asilia ya Kiingereza na kuchukua silabi za *Sheng'* kama viambishi, havikuchapishwa. Vitenzi kama; ***ku****relax*, ***ku****jienjoy*, ***ku****fight* na ***ku****travel* hayajachapishwa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Fonolojia Boreshi, kuna shartizuizi kuwa muundo wa silabi za *Sheng'* lazima uchukue mkondo wa KV. Vitenzi visivyochukua umbo hili vinapuuziliwa mbali.

Ferrari (2004) aligundua kiambishi cha hali isiyodhihirika #***nga#*** katika *Sheng'*. Kiambishi hiki hujitokeza katika baadhi ya vitenzi vya Kiswahili vya zamani. Kitenzi kama hufinya***nga*** huchukua mkondo huu. Hata hivyo katika *Sheng'* kiambishi #***nga#***

kinatumika katika hali zote za nyakati na hali. Ikiwa kitenzi katika hali ya kutenda huishia kwa irabu ***/a/*** basi silabi #***nga#*** hupachikwa kwenye kitenzi. Hata hivyo, ikiwa kitenzi kina irabu ***/i/*** basi silabi #***ngi***# itatumika. Kigezo hiki kinafanya silabi hii kuzua tofauti kubwa kati ya KS na *Sheng'*. Katika ukanushi, kiambishi hiki hubadilika na kuwa #***ngi***#. Mtafiti alipochunguza baadhi ya vitenzi katika S.E.D, aligundua kuwa kuna vitenzi fulani ambavyo vyaweza kuchukua silabi #***nga#*** katika kuonyesha nyakati na hali tofauti katika sentensi. Mtafiti alijaribu kunyambua vitenzi vinavyopatikana katika data ya utafiti huu ili kutathmini ikiwa maelezo ya Ferrari (2014) yanaafikiwa. Jedwali lifuatalo linatoa taswira halisi ya uchunguzi huu.

**Jedwali 37: Silabi #*nga#* ya ukanushi katika S.E.D.**

| **Kitenzi katika S.E. D** | **Sentensi katika KS** | **Sentensi katika *Sheng'*** | **Ukanushi katika *Sheng'*** |
|---|---|---|---|
| Mezea. | A**na**mezea chakula. | Amezea**nga** ukweli. | Amezea**ngi** ukweli. |
| Penya. | A**li**penya katika umati. . | Amepenya**nga** na kupotea. | Apenya**ngi** na kupotea. |
| Shiriki. | **Hu**shiriki kanisani. | Ashiriki**ngi** akipewa pombe. | Ashiriki**ngi** akipewa pombe. |
| Seti. | A**li**panga viti katika orodha ya seti tatu. | Amejiset**ingi** kuanza kampeni. | Ajiset**ingi** kuanza kampeni. |
| Tuna. | Alituna tumbo baada ya kula sumu. | Atuna**nga** mchanga. | Atuna**ngi** mchana. |
| Vunja. | Alivunja kalamu. | Avunja**nga** watu kwa ngumi. | Avunja**ngi** watu kwa ngumi. |

Katika jedwali hili la 37, mtafiti ameonyesha namna viambishi vya hali na nyakati vinavyobadilishwa katika vitenzi vya KS na mahali pake kuchukuliwa na kiambishi #***nga***# na #***ngi***# katika *Sheng'*.

Katika hali ya ukanushi, kiambishi #***ngi***# hutumika kama kiambishi tamati katika vitenzi vya *Sheng'*. Kiambishi #***nga#*** na #***ngi***# hutumika kama mashartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Viambishi hivi vinaamua ni aina gani ya maneno yanayoweza kuzalika katika *Sheng'* yenye silabi tamati #***nga#*** na #***ngi#***. Maneno yanayoundwa katika *Sheng'* yenye viambishi hivi basi huwa umbotokeo Hali hii ni tofauti na KS kwa sababu katika KS, vitenzi vya hali ya ukanushi huchukua kiambishi tamati #***ki***#.

### 3.3.1.3 Silabi za vivumishi vya *sheng'*

Vivumishi vingi baada ya kukopwa hubadilishwa kwa kuchukua viambishi tofauti ili kuleta upatanisho wa kisarufi katika *Sheng'*. Utafiti ulijaribu kuchunguza baadhi ya miundo ya silabi za vivumishi katika S.E.D. Matokeo ni kama yafuatavyo.

**Jedwali 38: Vivumishi katika S.E.D**

| **Kivumishi katika S.E.D.** | **Kivumishi katika *Sheng'*** | **Lugha asilia** |
|---|---|---|
| Supu | M-supu –mrembo sana | Kiingereza - super |
| Poa | M-poa- mzuri | Kiswahili – poa |
| Chafu | M-chafu – mtaalamu /mwerevu | Kiswahili - mwovu |
| Fala | M-fala – asiyejua kusoma na kuandika | Kiswahili -Mpumbavu |
| Zubaa | M-zubao- changanyikiwa akili | Kiswahili -hali ya bumbuazi |

Kutokana na data hii, kipasuo ghuna cha mdomo ***/m/*** kikitiwa kwa baadhi ya nomino na vitenzi kabla ya mzizi, hubadilisha maneno hayo na kuwa vivumishi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, kipasuo ghuna cha mdomo ***/m/*** kinatumika kama kihimili cha utathmini. Kinashiriki katika kuamua ni aina gani ya vivumishi

vinavyoweza kuzalika kutoka kwa nomino za *Sheng'*. Maneno yaliyoorodheshwa katika jedwali la 38, yanatumika kama umboghafi.

Vivumishi vinavyozalika vinakuwa umbotokeo. Hali hii ni tofauti sana na KS ambapo viambishi vya maneno kama #***mwa$****na#* hutumika. Neno *jeshi* linakuwa ***mwa****najeshi*. Matumizi mapana ya kipasuo cha midomo **/m/** yakizoeleka pakubwa huenda yakapata matumizi katika KS. Hali hii yaweza kuchangia katika kupungua kwa matumizi ya KS.

### 3.3.1.4 Silabi za vielezi katika *Sheng'*

Uchambuzi wa data ya utafiti huu ulidhihirisha kuwa vielezi vingi vya *Sheng'* huundwa kutoka kwa nomino au vivumishi ambavyo hukopwa kutoka lugha zingine. Kiambishi #***ki#*** au #***vi#*** kinapotiwa kwa baadhi ya nomino na vitenzi, hubadilika na kuwa vielezi.

**Jedwali 39: Muundo wa vielezi katika *Sheng'***

| **Maneno asili** | **Vielezi** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|---|
| Orodha - Kiswahili | **Ki**orodha | Kuwa karibu, zunguka karibu | Mpangilio wa majina/vitu |
| Poa – Kiswahili | **Vi**poa | Kuwa sawa | Tulia |
| Sure - Kiingereza | **Ki**shua | Kuwa nzuri | Mashua ndogo |
| Radar – Kiingereza | **Ki**rada | Kuwa katika mazingira | Kifaa cha kuongoza meli au ndege |
| Fala – Kiswahili | **Ki**fala | Mjinga | Mpumbavu/bozi |
| Chizi – Kiswahili | **Ki**chizi | Wazimu | Mwenye akili punguani |

Maneno ya S.E.D kama vile *orodha*, *poa*, na *shua* yanaweza kuchukua silabi #***ki#*** au #***vi***# na kubadilika kuwa vielezi. Kielezi *poa* kikichukua silabi #***vi***# kinabadilika na kuwa kielezi ***vi****poa*. Mfano huu waweza kudhihirika katika sentensi; *yule odijo hufunza*

***vi**poa* (Yule mwalimu hufunza vizuri). Nomino *fala* inakuwa ***ki**fala* na *chizi* linakuwa ***ki**chizi*. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, viambishi #***ki#*** na #***vi#*** vinatumika kama mhimili wa utathmini. Vinachangia kuamua ni umbo gani la vielezi vinavyoweza kuundwa baada ya kuchukua viambishi awali #***ki#*** na #***vi#***.

Mkururo huu huenda ndio hufanya wazungumzaji wa *Sheng'* kutumia baadhi ya nomino na vitenzi kama vielezi. Uzoefu mkubwa wa maneno ya sampuli hii yaweza kuathiri leksimu za KS.

### 3.3.3 Dhana ya ukanushi katika *Sheng'*

Ferrari (2014) alichunguza namna dhana ya ukanushi inavyojitokeza katika *Sheng'*. Ukanushi wa *Sheng'* hufanana na wa KS. Hata hivyo fonimu za ukanushi #***ha#*** na #***hu#*** hubadilika na nafasi yake kuchukuliwa na irabu **/a/** au */**i**/*. Konsonanti */**h**/* hudondoshwa na sauti za irabu huchukua mahali pake. Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, ilibainika vitenzi vifuatavyo ambavyo huchukua mkururo huu wa ukanushi.

**Jedwali 40: Ukanushi katika *Sheng'***

| **Kitenzi katika S.E.D.** | **Yakinishi** | **Kukanusha katika *Sheng'*** |
|---|---|---|
| Ambaa | Mtoii anaambaa – *Mtoto anaondoka* | Mtoi aambai – Mtoto haondoki |
| Choma | Mgeni anachoma fegi – mgeni anavuta sigara. | Mgeni achomi fegi – mgeni havuti sigara |
| Dinda | Abiria adinda kusafiri – Abiria akataa kusafiri | Abiria adindi kusafiri. Abiria hajakataa kusafiri. |
| Lenga | Rafiki yake amemlenga – Rafiki wake anajifanya hamuoni. | Rafiki yake amlengi – Rafiki yake hajifanyi anamuona. |
| Ng'oka | Mgonjwa ameng'oka – Mgonjwa amekufa. | Mgonjwa ajang'oka – Mgonjwa hajakufa. |

Mifano ya sentensi katika jedwali hili la 40, inaonyesha namna sauti ya vokali **/a/** hutumika katika ukanushi katika *Sheng'*. Hii ni mojawapo ya sifa inayofanya *Sheng'* kuwa tofauti na KS. Mazoea ya aina hii yakishamiri, yaweza kufanya wazungumzaji kupuuza matumizi ya maneno ya KS yenye konsonanti **/h/.**

Vokali **/a/** yatumika katika data hii kama kihimili cha utathmini katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Kinatumika kuamua aina za vitenzi vinavyoweza kuzalika katika hali ya ukanushi kikitokea mwanzoni mwa vitenzi.

### 3.3.4 Nyakati na hali katika *Sheng'*

Maelezo ya Iraki (2004) yanaonyesha kuwa viambishi vya nyakati na hali katika *Sheng'* ni tofauti na KS. KS huwa na viambishi vya nyakati ambavyo huonyesha wakati wa tukio kutendeka. Wakati uliopo huchukua kiambishi #***na#***, wakati ujao #***ta#***, na wakati uliopita #***li#***.

Vitenzi vingi vya *Sheng'* huchukua utaratibu huu. Hata hivyo, kuna mazingira fulani ambapo *Sheng'* hukiuka mtindo huu kwa kuchukua kiambishi #***sh#***. Katika sentensi *Juma amepoa, Sheng'* itakuwa *Juma a***sh***apoa*. Tukio likiwa limekamilika kiambishi cha hali ni #***me#***. Mfano katika sentensi *ameandika*. Sentensi hii inaashiria kuwa tendo limekamilika muda mfupi uliopita. Hata hivyo, *Sheng'* hupuuza matumizi ya viambishi hivi vyote; #***me#***, #***ta#*** na #***li***# na badala yake kiambishi #***na#*** hutumika ambacho huchukua nafasi hizo. Mtafiti alijaribu kunyambua vitenzi kwa mujibu wa data ya utafiti huu na akagundua kuwa hali hii ni dhahiri katika msimbo wa *Sheng'*.

**Jedwali 41: Hali ya mazoea katika *Sheng'***

| **Kitenzi katika S.E.D** | **Nyakati na hali katika *Sheng'*** | **Nyakati na hali katika KS** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| Laiki | A**sha**mlaiki. | Anampenda | Silabi #sh #yatumika badala ya #na# |
| Lenga | A**sha**lenga wenzake. | Amepuuza wenzake | Silabi #sh# yatumika badala ya #me# |
| Manga | A**sha**manga chakula jana. | Alikula chakula jana. | Silabi #sh# yatumika badala ya #li# |
| Ng'oka | A**sha**ng'oka | Ameng'oka na mizizi | Silabi #sh# yatumika badala ya #me# |
| Nyoa | Mhalifu a**na**mnyoa mahakamani kesho | Mhalifu atamwambia ukweli mahakamani kesho. | Kiambishi cha wakati uliopo #na# kinabadilika kuwa #ta# |
| Dinda | A**na**dinda kucheza. | Hukataa kucheza. | Silabi #na# yatumika badala ya #hu# |

Kwa mujibu wa utafiti huu, iligunduliwa kuwa baadhi ya vitenzi katika S.E.D vyaweza kuchukua kiambishi #***sha#*** kusimamia hali na nyakati zote katika KS. Kiambishi #***na#*** nacho kinatumika hata katika mazingira ya wakati ujao na hali ya mazoea.

Kwa mujibu wa Iraki (2004) katika *Sheng'* kiambishi cha wakati uliopo katika KS #***na#*** hubadilika na kutumika katika hali ya mazoea. Kiambishi #***na#*** hutumika katika *Sheng'* kurejelea nyakati na hali zote ambazo husimamiwa na viambishi #***li#***, #***me#*** na hata #***hu#.*** Mwingiliano huu na mpishano wa viambishi vya nyakati na hali vyaweza kuathiri KS. Wazungumzaji wa *Sheng'* huenda wakawa na utatanishi kubaini ni muktadha upi mahsusi wa matumizi ya viambishi hivi. Katika hali ya mazoea, KS hutumia kiambishi #***hu#*** kuonyesha hali ya mazoea.

**1.4. Mifanyiko ya kifonolojia katika *Sheng'***

Fonimu za *Sheng'* hushiriki katika ujenzi wa maumbo mbalimbali ya viambishi na silabi. Mifanyiko hii huchangia katika kuzuka kwa leksimu mpya za maneno ambayo hupata maana pana katika mawasiliano. Uchambuzi wa data ya utafiti huu ulidhihirisha mifanyiko ifuatayo ya kifonolojia:

**3.4.1 Kudhoofika kwa fonimu**

Owino (2016) na Mgullu (1999) wanaeleza kuwa, mfanyiko wa kudhoofika kwa fonimu unahusu fonimu kubadilika kutoka kuwa fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu zaidi na kuwa fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali. Katika utafiti huu, kudhoofika kwa fonimu kulibainika kwenye maneno kama vile;

**Jedwali 42: Fonimu za udogo katika maneno ya S.E.D**

| **Nomino katika S.E.D** | **Udogo katika KS** | **Udogo katika S.E.D.** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| Babe | K**i**jibabe | K**a**babe | Msichana mdogo |
| Bano | K**i**jibano | K**a**bano | Aina fulani ya jiwe |
| Buyu | K**i**jibuyu | K**a**buyu | Baba |
| Chizi | K**i**jizi | K**a**chizi | Wazimu |
| Buda | K**i**buda | K**a**buda | Mwanamme mzee mdogo |
| Fala | K**i**jifala | K**a**fala | Asiyejua kusoma na kuandika |

Kutokana na data katika jedwali 42, imedhihirika kuwa irabu **/i/** katika silabi #***ki***# inadondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu **/a/**. Katika matamshi, irabu **/a/** hutamkika kwa sauti hafifu ikilinganishwa na **/i/**. Kwa kufanya hivyo, silabi ya udogo katika *Sheng'* inakuwa #**ka#**. Umbo hili la silabi ya udogo limedhihirishwa na Githinji

(2022) aliyetoa mfano wa maneno kama vile; ***ka****mlango* na ***ka****mchoro*. Mfanyiko huu hutokea katika mazingira ya /i/ < --- > /a/.

Fonimu ya udogo /**a/** inatumika kama shartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Ni nomino zinazoweza kuchukua fonimu ***/a/*** ya udogo katika *Sheng'* ndizo hukubalika.

### 3.4.2 Usilimishwaji wa fonimu

Uchambuzi wa data ya utafiti huu ulidhihihirisha usimilishwaji wa baadhi ya fonimu zinazotamkika katika mazingira jirani. Kipashio jirani huweza kuathiriwa na kipashio kingine kilicho mkabala nacho na hivyo kuchukua sifa za kimatamshi za kipashio hicho jirani. Owino (2016) katika tasnifu yake ya uzamili, alieleza kuwa usilimishwaji unaweza kutokea konsonanti ikiathiri vokali au vokali ikiathiri konsonanti au vokali ikiathiri vokali nyingine au hata konsonanti ikiathiri konsonanti nyingine. Usilimishwaji ulibainika katika mifano ifuatayo: *wa**z**ee* – *wa**s**ee* (sauti ***/z/*** kubadilika na kuwa /***s/***).

*Jersy – jazi* (/***s/*** < --- > ***/z/*).** Na vile vile ***P****ano* -***b****ano* ambapo sauti ***/p/*** inabadilika na kuwa ***/b/)*** kwa hinyo mazingira haya yanakuwa: *(/p/* < --- > /b/). Katika wingi wa nomino hasa katika ngeli ya *A-WA* mtafiti aligundua kuwa, KS huwa na kiambishi #***wa#*** cha wingi. Katika *Sheng'* kiambishi hiki hubadilika na kuwa #***ma#***. Kiyeyusho **/w/** hubadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na kipasuo cha midomo **/m/.** Muundo wa wingi katika baadhi ya maneno ya *Sheng'* ulidhihirishwa na maelezo ya Bosire (2006). Bosire (2006) alitathmini namna nomino zisizokuwa na umbo la wingi na umoja katika KS huwa zinabadilika na kuchukua kiambishi **/m/** katika *Sheng'*. Aidha, nomino za mkopo hasa kutoka lugha ya Kiingereza zikijitokeza katika *Sheng'*

huchukua silabi #***ma#*** kama kiambishi cha wingi. Alitoa mfano wa neno *ndizi* ambalo katika wingi hubadilika na kuwa ***ma****ndizi*. Hali hii hudhihirika katika mazingira ya {Ɵ} < --- > {ma}. Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, iligunduliwa kuwa baadhi ya nomino katika S.E.D zaweza kuchukua muundo huu katika wingi.

**Jedwali 43: Umbo la wingi la nomino katika S.E.D**

| **Nomino katika S.E.D.** | **Wingi katika *Sheng'*** |
|---|---|
| Babe | Mababe |
| Bano | Mabano |
| Buyu | Mabuyu |
| Chizi | Majizi |
| Dafu | Madafu |
| Fala | Mafala |
| Gomba | Magomba |
| Kuli | Makuli |
| Mchuma | Machuma |

Kutokana na jedwali hili ni wazi kuwa, baadhi ya nomino katika *Sheng'* huchukua silabi #***wa#*** kama kiambishi awali kwa nomino ili kutoa dhana ya wingi. Hata hivyo, utafiti uligundua kuwa baadhi ya nomino zinakiuka utaratibu huu. Nomino kama *mtumba* haiwezi kuwa ***ma****tumba* bali huwa *mitumba*.

Mpishano kati ya neno *mtumba* na *mitumba* inadhihirisha mhimili wa uzalishi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Katika kihimili hiki, maneno haya yanashindana kama umboghafi. Baada ya ushindani huu, neno *mitumba* linakubalika kama umbotokeo baada ya kupitia kwa shartizuizi la kiambishi cha wingi #***mi#*** katika *Sheng'*.

### 3.4.3 Udondoshaji wa silabi katika maneno ya S.E.D.

Mgullu (1999) alieleza jinsi irabu hudondoshwa katika KS na kuunda sauti tofauti za maneno. Kutokana na data ya utafiti huu, mtafiti aligundua maneno mengi katika S.E.D ambayo hayadondoshi irabu jinsi Mgullu (1999) alivyoeleza katika KS. Badala ya *Sheng'* kudondosha irabu, iligunduliwa kuwa, udondoshaji wa silabi nzima ndio hujitokeza kwa wingi kwa baadhi ya maneno. Mifano ifuatayo inaonyesha maelezo haya:

Panga – Panga**ni** (Silabi #***ni#*** imedondoshwa)

Kiswa – Kiswa**hil**i (silabi #***hi#*** na #***li***# zimedondoshwa)

Nai – Nai**robi** (silabi #***ro#*** na ***#bi#*** zimedondoshwa)

### 3.4.4 Tangamano la irabu katika *Sheng'*

Kulingana na Mgullu (1999), huu ni utaratibu ambao irabu fulani hukubali kuandamana katika mazingira maalum. Katika maneno ya S.E.D kuna baadhi ya irabu ambazo huwa katika mzizi wa neno. Irabu hizi zinajitokeza vilevile kwa baadhi ya viambishi tamati ikiwa neno linanyambuliwa katika hali tofauti. Katika vitenzi vya *Sheng'* vyenye irabu **/o/** kwa mzizi, mtafiti aligundua kuwa irabu hii huhusika katika kuunda viambishi tofauti. Neno *ch**o**ma* linakuwa *ch**o**m**o**ka* na *t**o**b**o**a* linakuwa *t**o**b**o**ka*. Kutokana na mifano hii, irabu **/o/** inashiriki kuunda mzizi wa neno na kisha kuunda viambishi.

### 3.5 Sifa za arudhi za Sheng'

Makini (2015) anaeleza sifa za arudhi kuwa ni zile zinazowekwa kwenye vipashio vikubwa zaidi ya fonimu. Sifa hizi huwa kwenye silabi, neno, kirai au sentensi. Mifano ya sifa arudhi ni shadda, toni na kiimbo.

#### 3.5.1 Jinsi shadda inavyojitokeza katika Sheng'.

Kindija (2012), alieleza kuwa shadda ni utamkaji wa nguvu zaidi katika sehemu ya neno au fungu la maneno. Makini (2015) anaendelea kusema kuwa, utamkaji wa nguvu hufanywa kwenye silabi kuliko sehemu nyingine yoyote ile. Shadda huweza kuwa na msisitizo au ubainishaji wa maana za maneno. Maneno ya KS hutiwa shadda katika silabi ya pili kuanzia mwisho mwa neno. Katika neno *m**ko**no*, shadda itatiwa kwa silabi #***ko***# kwa sababu ni ya pili kuanzia mwisho wa neno.

Baadhi ya maneno katika *Sheng'* pia huchukua shadda kwenye silabi ya pili kutoka mwisho. Maneno kama ***chu**ja* (vyatu) na *chi**zi**ka* (kuwa wazimu) hutiwa shadda kwa silabi ya pili kuanzia mwisho. Hata hivyo, utafiti huu uligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* huwa na shadda mwishoni mwa neno. Githiora (2018) ana mtazamo kuwa wakati ambapo irabu ya mwisho inavutwa, shadda huhamishwa kutoka silabi ya pili kuanzia mwisho. Irabu za tamati ndizo hutiwa shadda kwa sababu huwa na uzito wa sauti kimatamshi.

Maneno yenye sauti ya mvuto kama *amba**a*** hutiwa shadda kwa irabu ya mwisho **/a/** inayochukua nafasi ya silabi ya tamati. Hata hivyo, mtafiti alipochunguza S.E.D alipata mifano zaidi japo haijachapishwa katika KS.

**Jedwali 44: Shadda katika maneno ya *Sheng'***

| **Neno katika S.E.D** | **Silabi iliyotiwa shadda katika *Sheng'*** | **Silabi iliyotiwa shadda katika KS** |
|---|---|---|
| Ambaa | A-mba- '**a** | a- '**mba-**a |
| Seti | Se- '**ti** | **'Se**-ti |
| Bako | Ba- '**ko** | **'Ba**-ko |
| Pango | Pa – **'ngo** | **'Pa-** ngo |
| Tele | Te**- 'le** | **'Te-** le |

Kutokana na maneno yaliyo katika jedwali hili la 44, utafiti huu uligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* hutiwa shadda katika silabi ya mwisho mwa neno. Hali hii ni tofauti mno na jinsi ilivyo katika KS. Mgullu (1999) alieleza kuwa mkazo katika KS hutiwa katika silabi ya pili kuanzia mwisho. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, mhimili wa shartizuizi la KS kuwa, silabi ya pili kuanzia mwisho mwa neno ndilo hutiwa shadda unakiukwa neno hilo likikopwa katika *Sheng'*.

Shadda ikitiwa tamati mwa neno, hufanya muundo wa kifonolojia wa *Sheng'* kuwa tofauti na ule wa KS. Maneno mengi ya mkopo kutoka Kiingereza yana shadda katika silabi tamati. Kuna hatari kuwa wazungumzaji wa KS wanaweza kuathirika kwa kutia shadda katika silabi tamati kwa hivyo kuathiri mfumo wa matamshi ya maneno katika KS. Utafiti huu ulibainisha maneno yafuatayo katika S.E.D ambayo shadda hutiwa kwa silabi tamati.




**Jedwali 45: Shadda katika silabi tamati katika *Sheng'***

| **Neno** | **Maana** |
|---|---|
| Ba'**ko** | Mpira wa vikapu |
| Ba'**ngo** | Shilingi moja |
| Ba'**no** | Aina fulani ya jiwe |
| Mzuba'**o** | Changanyikiwa akili |
| Pe'**po** | Adhabu |

### 3.5.2 Kiimbo katika *Sheng'*.

Kindija (2012), alieleza kiimbo kama umbo la sauti linalotokana na mpandoshuka wa sauti za maneno wakati wa usemaji. Kiimbo ni utaratibu wa kupanda au kushusha kwa sauti katika usemaji. Kwa mujibu wa Kindija (2012), kiimbo hufanya sehemu fulani za sentensi kusikika zaidi kuliko zingine. Kimsingi, hujumuisha mambo yote yanayohusiana na uzungumzaji, kama kidatu, shadda na toni. Utafiti huu uligundua kuwa, kiimbo katika *Sheng'* huwa na mfanano mkubwa sana na KS. Hata hivyo, namna maneno fulani yanavyotumika katika mawasiliano ya *Sheng'* yanaweza kuzua maana tofauti au kufanya kauli fulani isieleweke ipasavyo. Mtafiti aliweza kugundua kuwa neno kama *sasa* laweza kudhihirisha maana tofauti kutegemea namna kiimbo kilivyotiwa katika mazungumzo. Aliweza kubainisha aina zifuatazo za viimbo katika sentensi za *Sheng'* kama inavyoonyeshwa katika jedwali 46.

**Jedwali 46: Kiimbo katika maneno ya S.E.D**

| Aina ya kiimbo | Neno | Sentensi | Alama za kiimbo | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Kiimbo kauli | Sasa | Kuja sasa. |  | Mawimbi huwa katika kiwango cha wastani |
| Kiimbo cha maulizo | Sasa | Utakuja sasa? |  | Mawimbi huteremka chini |
| Kiimbo cha amri | sasa | Ondokeni sasa. |  | Mawimbi hupanda juu |
| Kiimbo cha mshangao | Jo | Amefika sasa jo! |  | Mawimbi hunda juu |

#### 3.5.2.1 Kiimbo cha kauli au maelezo.

Kindija (2012) alifafanua kiimbo kauli kuwa hudhihirika wakati msemaji wa lugha huwa katika kidatu chochote cha mawimbisauti yakiwa katika mstari mnyoofu. Neno la *Sheng'; sasa* laweza kutumika katika sentensi kudhihirisha kiimbo kauli. Sentensi

kama: *Amekuja sasa*, ina mawimbi ya sauti katika msitari mnyoofu. Kidatu hakipandi juu wala kuteremka chini. Hali ya mawimbi ya sauti yanabakia katika hali ya wastani.

#### 3.5.2.2 Kiimbo cha maulizo

Kindija (2012) anaeleza kuwa, kiimbo maulizo hutokea mzungumzaji anapofika mwishoni mwa swali na kupandisha kidatu na kisha kumalizia kwa kukishusha kidatu. Sentensi *Amekuja sasa*, inajitokeza ikiwa katika kiimbo cha kauli. Hata hivyo, mawimbi ya sauti yaweza kubadilishwa na kuwa; *Amekuja sasa?* Katika sentensi hii, kiimbo kinabadilishwa kutoka kuwa kiimbo kauli na kuwa kiimbo cha maulizo.

#### 3.5.2.3Kiimbo cha amri

Kwa mujibu wa Kindija (2012), kiimbo cha amri hutumia kidatu cha juu zaidi kuliko ilivyo katika kiimbo cha maelezo. Neno moja laweza kupata maana tofauti kutegemea na namna kiimbo kilivyotiwa wakati wa mazungumzo. Kwa kutumia neno *Sasa*, kiimbo kinabadilika na kuwa amri katika sentensi kama: *Enda sasa*.

#### 3.5.2.4Kiimbo cha mshangao

Kindija (2012) alieleza kuwa mawimbi ya kiimbo cha mshangao hutolewa huku yakiambatana na kupandisha kidatu katika silabi za mwisho mwa neno. Baadhi ya maneno ya S.E.D yenye kiimbo cha mshangao ni kama *Jo*! *Salala*!

### 3.5.3 Toni katika *Sheng'*

Kindija (2012) anaeleza toni kuwa, ni kiwango pambanuzi cha kidatu cha silabi katika neno ambacho chaweza kubadilisha maana. Alisistiza kuwa, toni huambatana na vitamkwa ghuna katika neno na wala sio vitamkwa sighuna. Ili toni ijitokeze katika

neno, lazima vitamkwa ghuna viambatane na irabu. Kwa msingi wa maelezo haya, irabu ndizo hubeba toni katika silabi. Kauli hii inaafiki sana utafiti huu kwa sababu utafiti huu uliweza kubainisha baadhi ya maneno katika S.E.D ambayo yanakuwa na maana tofauti kwa sababu ya toni. Kwa mfano neno *zima* linakuwa na maana mbili. Likitamkwa bila toni linamaanisha *tuliza*. Hata hivyo toni ikitiwa kwa irabu /a/ inabadilisha maana ya neno na kuwa *zima* lenye maana ya mtaa wa Zimmerman mjini Nairobi. Kama zilivyo lugha za kibantu, msimbo wa *Sheng'* huwa na toni. Hali hii inafanya *Sheng'* kuwa tofauti na KS. Kadhalika, katika uchambuzi wa data ya utafiti huu, utafiti huu uligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* yaliyokopwa kutoka kwa lugha za kibantu na Kiingereza huwa na toni.

Sauti ya irabu **/ɛ/** na **/ɔ/** husababisha toni katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Kutokea kwa irabu **/ɛ/** na **/ɔ/** katika *Sheng'* kunatimiza mhimili wa uzalishi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Irabu hizi zinatumika kuzalisha aina nyingi ya maneno ya *Sheng'*. Maneno yanayokopwa kutoka lugha zingine yanakuwa umboghafi. Yakitokea katika *Sheng'* baada ya kuchukua irabu **/ɛ/** na **/ɔ/,** yanakuwa umbotokeo. Neno *mabao* likitamkwa katika hali ya kawaida humaanisha *idadi nyingi ya goli zilizofungwa katika mchezo wa kandanda.*

Hata hivyo, neno hili likitamkwa na kubadilisha sauti ***/o/*** na kuwa **/ɔ/;** mauba**ɔ** litakuwa na maana ya *njaa*. Mifano ifuatayo yaweza kuthibitisha haya.

**Jedwali 47: Maneno yenye toni katika S.E.D**

| Neno | Alama ya toni | Maana |
|---|---|---|
| Bako | | Kipimo cha kitanga cha mkono |
| Bak ɔ | ɔ$^{v}$– toni ya kupanda | Mpira wa vikapu |
| Bano | | Chombo cha kubania mbao/chuma |
| Ban ɔ | ɔ$^{v}$– toni ya kupanda | Aina fulani ya jiwe |
| Bango | Toni ya wastani | Karatasi kubwa ya maandishi |
| Bang ɔ | ɔ$^{v}$– toni ya kupanda | Shilingi moja |

Kutokana na jedwali hili, mtafiti amebainisha baadhi ya maneno ambayo yana silabi zinazokaribiana kimatamshi kupitia kwa irabu. Irabu hii ndio inayochangia kuzuka kwa toni katika maneno haya. Hii ni kwa sababu katika *Sheng'* iraabu **/o/** hubadilika na kuwa /ɔ$^{v}$/ ya mpumuo. Hali hii hujitokeza katika mazingira ya:

/o/ < --- >/ɔ$^{v}$/. Wazungumzaji wa KS wasiokuwa na uwezo wa kutofautisha sauti hizi kimatamshi huenda wakaathirika kwa kushindwa kufahamu maana kusudiwa. Hali hii huweza kuchangia katika kuathirika kwa KS kifonolojia.

### 3.6 Hitimisho

Katika sura hii utafiti umeainisha namna msimbo wa *Sheng'* unavyotofautiana kifonolojia na KS. Umebainisha namna fonimu za *Sheng'* zinavyodhihirika katika irabu na konsonanti. Mtafiti ameonyesha aina mbalimbali za irabu za *Sheng'* na namna zinavyoshiriki kuunda aina tofauti za Silabi. Miundo ya fonimu za konsonanti za *Sheng'* imeonyeshwa. Ameweza kuonyesha jinsi irabu na konsonanti za *Sheng'* zinavyotofautiana na za KS. Kadhalika, amechunguza namna fonimu za *Sheng'* zinavyohusika katika uundaji wa silabi na viambishi mbalimbali vya maneno katika

*Sheng'*. Mtafiti ameweza kuonyesha namna fonimu za *Sheng'* zinavyoshiriki katika uundaji wa aina mbalimbali za maneno ya *Sheng'*. Aina za maneno zilizobainishwa ni nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi.

Aidha, sura hii imefanikisha kuonyesha mifanyiko mbalimbali ya fonimu za *Sheng'*. Mifanyiko hii ni pamoja na: kuhafifika kwa fonimu, usilimishwaji wa fonimu, udondoshaji wa silabi na tangamano la irabu**.** Sifa za kiarudhi pia zimejadiliwa katika sura hii. Utafiti huu umedhihirisha kuwa shadda katika *Sheng'* hujitokeza katika mazingira tofauti na namna ilivyo katika KS. Isitoshe, utafiti umeonyesha namna kigezo cha toni kinavyosababisha tofauti za kifonolojia katika baadhi ya maneno ya *Sheng'* na KS. Umehusisha uchunguzi huu na mihimili ya nadharia ya Fonolojia Boreshi. Mtafiti ameonyesha jinsi maneno yanayokopwa kutoka lugha zingine yanavyotumika kama umboghafi. Katika *Sheng'*, maneno haya hupitia taratibu mbalimbali za kifonolojia. Taratibu hizi amezionyesha kuwa baadhi ya mashartizuizi kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi.

Maneno ambayo yanazalika baada ya kupitia taratibu hizi yanakuwa umbotokeo baada ya kuamuliwa na mhimili wa uzalishi. Hali hii inaonyesha kuwa, nadharia ya Fonolojia Boreshi, imefaa zaidi katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu. Kwa kufanya hivyo, lengo la pili la utafiti huu ambalo ni kuonyesha tofauti za kifonolojia kati ya *Sheng'* na KS limetimika. Isitoshe, swali la pili la utafiti huu limejibiwa. Swali hili ni: muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* unatofautiana vipi na Kiswahili sanifu? Mtafiti ameweza kueleza hatua kwa hatua namna miundo mbalimbali ya

fonimu za KS na *Sheng'* inavyotofautiana. Ameonyesha pia namna silabi za *Sheng'* na KS zinavyotofautiana. Kadhalika, ameonyesha namna sifa za kiarudhi za *Sheng'* zinavyokuwa tofauti na KS.

# SURA YA NNE

# SABABU ZA TOFAUTI ZA KIMUUNDO KATIKA MATUMIZI YA SHENG' NA KISWAHILI SANIFU.

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, utafiti unadhamiria kueleza sababu mahsusi ambazo zinachangia kuwepo kwa tofauti za kimuundo katika matumizi ya leksimu za *Sheng'* na za KS. Utafiti huu ulizingatia namna maumbo mbalimbali ya fonolojia ya *Sheng'* yanavyojitokeza na kuwa tofauti na KS na sababu za kuwepo kwa tofauti hizo. Kwa kufanya hivyo, mpaka uliopo kati ya KS na *Sheng'* utadhihirika wazi. Baadhi ya sababu zinazochangia kuwepo kwa tofauti kati ya *Sheng'* na KS ni kama zifuatazo:

## 4.2 Sababu zinazochangia kuwepo kwa tofauti kati ya *Sheng'* na KS

Utafiti huu umefanikisha kubainisha sababu kadhaa zinazochangia kuzuka kwa tofauti kati ya muundo wa maneno ya *Sheng'* na maneno ya Kiswahili sanifu. Baadhi ya sababu ni: kuficha siri, athari za lugha changizi, ubunifu wa wazungumzaji, mienendo ya kisasa, hali ya maisha na uchumi, kurahisisha mawasiliano, kutenga wahusika na sababu za tasfida. Sababu hizi zimeelezwa kwa kina na mtafiti.

### 4.2.1 Kuficha siri katika *Sheng'*

Wataalam wengi wanathibitisha kuwa msimbo wa *Sheng'* ulizuka kwa sababu ya kuficha siri. Mbaabu na Kipande (2003) wakizungumzia kuhusu chimbuko la *Sheng',* walieleza kuwa jamii za mitaa ya mabanda jijini Nairobi zinaishi katika hali ya msongamano mkubwa. Vijana walipotaka kujieleza miongoni mwao kwa masuala

yanayohusu mambo ya faraghani walishindwa. Hii ni kwa sababu hawakutaka mazungumzo yao yatambulike na wazazi au watu wazima wanaowazunguka. Iliwalazimisha kubuni msimbo wa lugha unaoweza kuwasilisha masuala haya kwa njia ya siri. Hata hivyo, wataalamu hawa hawakutoa mifano mahsusi na maelezo ya jinsi *Sheng'* inavyoficha siri.

Katika S.E.D, utafiti huu uliweza kubainisha baadhi ya maneno yaliyobuniwa ili kuficha siri. Kusudi la kuficha siri huenda likawa ni kuhakikisha dhana inayozungumziwa isije ikajulikana na watu wengi. Neno la KS *msichana* ni la kimsingi sana na linaeleweka na takribani wazungumzaji wote wa *Sheng'*. Hata hivyo, kutokana na data ya utafiti huu, neno hili limetungiwa visawe vingi vinavyotumika katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano. Baadhi ya maneno yaliyogunduliwa yanayotumika katika *Sheng'* badala ya neno *msichana* ni kama yafuatayo; *babe, kifaranga, lebo, matunda, mwasi, shaba, shabu, toti* na *manze*. Kwa ujumla, haya ni maneno manane yanayotumika kama visawe vya neno *msichana*. Lengo kuu la vijana kubuni aina nyingi ya maneno kurejelea neno *msichana* ni kuficha siri. Wakizungumza miongoni mwao kumhusu msichana fulani, huenda hawataki kutambulika na hadhira kuhusu msichana wanayemzungumzia. Ubunifu wa maneno mbadala yenye maana ya neno msichanna, huchangia katika kupungua kwa matumizi ya istilahi 'msichana". Huu ni mfano wa jinsi *Sheng'* inavyoathiri KS.

Aidha, huenda msichana anayelengwa katika mazungumzo haya asije akajua kuwa yeye ndiye hadhira lengwa. Tatizo ni kwamba, matumizi ya maneno haya mbadala

yanakinzana na maana zinazojitokeza katika KS. Maumbo ya maneno na hata baadhi ya matamshi ya visawe hivi yanakaribiana na ya KS. Nadharia ya Fonolojia Boreshi imehusika vilivyo katika kuamua ni maumbo gani ya visawe vinavyoweza kutumika kama maneno ya mbadala ya neno *msichana*.  Neno *msichana* linakuwa umboghafi na visawe vya *msichana* vinakuwa umbotokeo. Hali hii inazua hatari kwa KS kwa sababu maneno ya *Sheng'* mwishowe yataweza kuingizwa kwa KS.

Isitoshe, maneno yanayotoholewa kutoka lugha ya Kiingereza na kuingizwa kwa *Sheng'* yanafanyiwa ukarabati hadi umbo linalotokea linakuwa tofauti mno na neno asilia. Neno *toti* limeundwa kutoka kwa neno *daughter* la Kiingereza. Hatua ya kwanza ya kuunda leksimu *toti* katika *Sheng'* ni kudondosha baadhi ya sauti za konsonanti. Kwa hivyo, silabi -***ughter*** zikadondoshwa.

Pili, mahali pa silabi zilizodondolewa pakachukuliwa na irabu ***/o/***. Nazo sauti za mwisho -***er*** zikadondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu ***/a/***. Mwisho, neno linalozalika linakuwa *toti* na wala sio *daughter*. Kusudi la kuunda *toti* ni kuwa, neno *dota* laweza kujulikana haraka kwa sababu sauti zake bado zinakaribiana na za *daughter* la Kiingereza. Ikabidi konsonanti ya kipasuo ghuna **/d/** idondoshwe na mahali pake pachukuliwe na konsonanti ya kipasuo sighuna **/t/.** Hali hii inajitokeza katika mazingira yafuatayo /d/ < --- > /t/. Irabu ya silabi #ta# inabadilika na kuwa #ti# katika mazingira ya /a/ < --- > /i/. Kwa hivyo, neno linalozalika likawa *toti*.

Neno *toti* likitamkwa, silabi #***ti#*** inapewa kidatu cha juu zaidi kuliko #***to#***. Hali hii inahamisha mkazo kutoka kwa silabi ya pili kutoka mwisho mwa neno hadi silabi tamati. Kama alivyoeleza Kindija (2012), mkazo katika KS hutiwa kwa silabi ya pili kuanzia mwisho wa neno. Neno *toti* katika *Sheng'*, mkazo unatiliwa katika silabi tamati. Kusudi la kukopa na kulikarabati neno *daughter* hadi kuwa *toti* inaaminika ni kwa sababu ya kuficha siri. Mfano zaidi ni neno *tini* (kijana mdogo) ambalo pia limeundwa kutoka kwa neno *teenager* la Kiingereza. Haiwezi kuwa rahisi kwa mtu asiye na ufahamu wa msimbo wa *Sheng'* kuelewa maana halisi ya neno *tini*. Lazima aambiwe au atangamane na vijana ndio apate kufahamu maana yake. Mifano hii ni ishara tosha kuwa *Sheng'* wakati mwingine hutumika kuficha siri miongoni mwa wazungumzaji.

### 4.2.2 Athari za Lugha changizi.

Mwihaki (2007) anaeleza kuwa, *Sheng'* ni msimbo wa lugha ambao hukopa maneno kutoka lugha za Kiafrika. Bosire (2006) alisistiza sifa ya *Sheng'* kuwa, huchukua leksimu na sarufi yake kutoka aina nyingi za lugha. Lugha hizi sio tu Kiingereza na KS, bali pia kutoka kwa lugha zingine zaidi ya arobaini nchini Kenya. Iraki (2014) aliongeza kwa kudai kuwa, baadhi ya maneno hukopwa kutoka lugha za Kiingereza, na Kifaransa. Baada ya kuyakopa maneno, huyabadilishwa ili kuafikiana na muundo wa KS.

Ferrari (2014) alisistiza kuwa *Sheng'* hukopa maneno yake kutoka kwa Kiswahili, Kiingereza na lugha zingine nchini Kenya kama vile Gikuyu, Luhya, Dholuo na Kikamba. Maelezo haya ya wataalamu yalichochea utafiti huu kuzama zaidi ili

kuonyesha namna lugha changizi zinavyochangia kuwepo kwa tofauti za kifonolojia kati ya *Sheng'* na KS. Zifuatazo ni baadhi ya sababu:

#### 4.2.2.1 Athari za lugha changizi kwa irabu za *Sheng'*

Lugha changizi ndizo zinazochangia kuwepo kwa irabu saba katika *Sheng'* kinyume na ilivyo katika KS. Mgullu (1999) alieleza kuwa KS kina irabu tano. Naye Mwihaki (2007) akaonyesha kuwa *Sheng'* ina irabu saba. Irabu za ziada mbili ambazo ni **/ɛ/**, na /ɔ/ huenda zimekopwa kutoka lugha zingine za Kibantu. Makini (2015) katika tasnifu yake ya uzamili, alionyesha kuwa, lugha ya Ekegusii ina irabu saba. Irabu hizi ni */a/*, */e/***,** **/ɛ**/, /i/, /o/, /ɔ/ na /u/*. Makini (2015) anaonyesha mifano ya irabu za Ekegusii kupitia kwa jedwali lifuatalo.

**Jedwali 48: Kutambua vokali za Ekegusii (Makini,2015)**

| Fonimu | Maneno | Maana |
|---|---|---|
| /a/ | Aba | Hawa |
| /e/ | Eba | Sahau |
| /ɛ/ | Enda | Chawa |
| /i/ | Iba | Iba |
| /o/ | Oigwe | Sikia |
| /ɔ/ | Ito | yetu |
| /o/ | Ura | Nyanganya |

Uhusiano uliopo kati ya Ekegusii na *Sheng'* ni kuwa zote zina irabu saba ambazo zinafanana. Hali hii ni tofauti sana na lugha ya KS ambayo ina irabu tano. Kutokana na muktadha huu, uchunguzi huu ulidhihirisha kuwa irabu */ɛ/ na /ɔ/* zimekopwa kutoka lugha za Kibantu ikiwemo Ekegusii. Irabu hizi zinafana na za *Sheng'* kama alivyobainisha Mwihaki (2007). Githiora (2018) alipochunguza jinsi lugha ya Gikuyu

huathiri *Sheng'*, alitoa mfano wa maneno ya Gikuyu; *shɔshɔɔ* (nyanya) na *mɔkɔrɔ* (mzazi, mtu mzima). Maneno haya yana irabu ***/ɔ/.***

Aidha, alitoa mfano wa neno la Gikuyu *gith***ɛ***ri* (chakula cha mchanganyiko wa mahindi na maharagwe). Neno hili lina irabu */ɛ*/. Kutokana na uchunguzi huu, yamkinika kuwa, kuzuka kwa irabu saba katika *Sheng'* ni kwa sababu ya mchango wa lugha changizi ikiwemo lugha ya Ekegusii na Gikuyu. Ekegusii na Gikuyu ni miongoni mwa lugha za Kibantu ambazo msimbo wa *Sheng'* hukopa leksimu nyingi. Kutokana na maelezo haya, irabu zinazosababisha tofauti kubwa kati ya *Sheng'* na KS ni **/ɛ/** *na* ***/ɔ/.*** Aidha, irabu hizi huwa katika lugha ya Kiingereza ambayo Kiswahili hukopa maneno mengi. Kutokana na data ya utafiti huu, utafiti ulibainisha baadhi ya maneno yenye irabu **/ɔ/** katika S.E.D**.** Baadhi ya maneno yenye irabu hii ni kama: *ban***ɔ** (aina fulani ya jiwe), *depɔ* (naibu wa mwalimu mkuu) na *dir***ɔ** (dirisha). Isitoshe, irabu **/ɛ/** iligunduliwa kudhihirika kwa maneno kama *kalɛ* (mtu kutoka jamii ya Kalenjin), *palɛ* (rafiki mkuu) na *telɛ* (runinga). Irabu hizi haziko katika KS lakini hujitokeza kwa baadhi ya lugha za Kibantu kama vile Gikuyu.

Kadhalika, utafiti huu umeonyesha kuwa kuna athari za lugha ya Dholuo kwa sauti za irabu za msimbo wa *Sheng'*. Neno *mosi* ambalo pia liko katika S.E.D limetokana na neno la Dholuo *mos* lenye maana ya *pole pole*. Neno hili baada ya kukopwa kutoka Dholuo, lilipachikwa irabi **/i/** katika silabi tamati na kuwa *mos**i***. Msimbo wa *Sheng'* umekopa muundo wa uundaji maneno kutoka Dholuo. Nomino za pekee katika lugha ya Dholuo aghalabu hupachikwa irabu **/o**/ katika silabi tamati. Kwa mujibu wa data ya

utafiti huu, imebainika kuwa kuna baadhi ya maneno ambayo huundwa kwa kupachikwa irabu ***/o/*** au */ɔ/* katika silabi ya tamati. Maneno kama *dag**o*** (mtaa wa Dagoretti mjini Nairobi), *dir**o*** (dirisha), *pang**o*** (mtaa wa Pangani mjini Nairobi) na *bak**o*** (mchezo wa vikapu) yameambishwa irabu **/o/**. Hata maneno ambayo usuli wake sio lugha ya Dholuo yanaongezwa irabu hii. Hii ni ishara tosha kuwa kuna athari ya lugha ya Dholuo kwa fonolojia ya *Sheng'*. Kushiriki kwa irabu */ɛ/ na /ɔ/* katika utafiti huu kunatimiza mhimili wa uzalishi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi.

Mhimili wa uzalishi hueleza kuwa, kila lugha ina uwezo wa kuzalisha aina nyingi za maneno katika lugha fulani. Irabu */ɛ/ na /ɔ/* zinashiriki kuunda aina mbalimbali ya silabi za maneno katika *Sheng'*. Maneno yanayoundwa kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi yanakuwa umboghafi. Yale yanayozalika na hatimaye kukubalika kama leksimu za *Sheng'*, basi yanakuwa umbotokeo.

### 4.2.2.2 Athari za lugha changizi kwa toni ya *Sheng'*

Kindija (2012) anasema kuwa lugha nyingi kusini mwa bara la Afrika huwa na toni. Anaendelea kueleza kuwa, kuna lugha chache sana zisizokuwa na toni na KS ni miongoni mwao. Utafiti huu uligundua baadhi ya maneno katika S.E.D yenye toni. Chanzo cha tofauti kati ya muundo wa maneno ya *Sheng'* na KS ni kwa sababu ya mchango wa lugha changizi. Kutokea kwa irabu **/ɛ**/ *na /ɔ /* kwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* hufanya hayo maneno kutamkwa kwa kidatu cha juu zaidi kuliko maneno mengine. Hali hii huzua toni. Maneno yenye silabi hizi kama: *umɔ* (mtaa wa Umoja jijini Nairobi), *satɔ* (Jumamosi), *tel**ɛ*** **(**runinga**)** na *bakɔ* (mchezo wa vikapu) yana toni. Maneno *satɔ, tel**ɛ*** na *bakɔ* yalikopwa kutoka lugha ya Kiingereza. Silabi za mwisho

katika maneno haya zinatamkwa kwa kidatu cha juu zaidi kwa hivyo kusababisha toni. Kando na maneno haya, kuna baadhi ya maneno mengine yaliyokopwa kutoka kwa KS lakini hutumika katika *Sheng'* yakiwa na toni. Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, kuna neno *zimaa* (mtaa wa Zimmerman). Muundo wa neno hili unatokana na neno la KS *zima* lenye maana ya *fanya kisiendelee kuwaka*.

Hali hii pia inatokea katika matamshi ya neno *inda*. Neno hili lisipotiwa toni, *inda* linamaanisha *wivu*. Likitiwa toni, maana yake asili inabadilika na kuwa; *sehemu ya viwandani mjini*. Mhimili wa shartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi umetumika kuamua ni aina gani ya maneno yanayoweza kuzalika kutokana na irabu **/ɛ/** *na* ***/ɔ/.*** Mhimili huu huweka mashartizuizi yasiyoweza kuvunjwa wakati wa kuunda maneno.

Maneno ya *Sheng'* yanayokopwa kutoka lugha ya Kiingereza yanakuwa umboghafi. Yanapitia shartizuizi la mpangilio wa silabi za *Sheng'* kuwa, silabi lazima iwe na muundo wa KI. Neno *Saturday* katika muktadha huu ni umboghafi. Nalo neno *sato* ni umbotokeo baada ya kupitia kwa shartizuizi kuwa silabi ya *Sheng'* lazima iwe na umbo la KI.

**4.2.2.3 Athari za lugha changizi katika unyambuzi wa vitenzi.**

Ferrari (2014) aligundua kuwa miundo ya viambishi katika *Sheng'* na KS sanifu hufanana kwa kiasi kikubwa. Hata vitenzi vya *Sheng'* ambavyo hukopwa kutoka lugha zisizo na vitenzi vinavyoweza kunyambulika, hunyambulika vikijitokeza katika *Sheng'*. Hata hivyo, tofauti kubwa inayojitokeza kati ya *Sheng'* na KS ni kuwepo kwa

kiambishi tamati cha hali, #***nga#***. Katika utafiti huu, mtafiti alijaribu kupachika kiambishi #***nga#*** kwa baadhi ya vitenzi vya *Sheng'* na matokeo yakawa ifuatavyo.

**Jedwali 49: Matumizi ya kiambishi #*nga#* katika vitenzi vya *Sheng'***

| **Vitenzi katika S.E.D** | **Kiambishi *nga* kwa vitenzi** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1. Chanuka | Chanuka**nga** | Kuwa katika mtindi/hali ya kisasa |
| 2. Chizika | Chizika**nga** | Kuwa wazimu |
| 3. Chota | Chota**nga** | Kutoa pesa |
| 4. Dinda | Dinda**nga** | Kataa kwa kiburi |
| 5. Kusanya | Sanya**nga** | Iba |
| 6. Lola | Lola**nga** | Kuona |
| 7. Mea | Mea**nga** | Enda/ondoka |
| 8. Pitisha | Pitisha**nga** | Leta |

Mfumo huu wa kunyambua vitenzi kwa kupachika kiambishi #***nga#*** umekopwa kutoka lugha za Kibantu. Matumizi ya kiambishi hiki hujitokeza kwa wingi katika lugha za Kibantu. Kwa hivyo, *Sheng'* imekopa mfumo huu wa unyambuzi kutoka lugha za Kibantu. Kutokana na jedwali hili, kiambishi #***nga#*** ni sehemu ya mhimili wa upangiliaji katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Kwa mujibu wa mhimili huu, mashartzuizi ya lugha hupangwa kiutaratibu kutoka kwa vizuizi vinavyoweza kuvumilika na vile visivyoweza. Sauti #**nga**# ni shartizuizi kutoka lugha za Kibantu. Kiambishi hiki ***#nga#*** katika data ya utafiti huu kinashiriki vilivyo kuzalisha aina mbalimbali za maneno katika *Sheng'*. Maneno yanayoundwa na kukubalika katika *Sheng'* kwa kupachikwa kiambishi #***nga***# yanatumika kuunda aina tofauti za leksimu.

### 4.2.3 Ubunifu wa wazungumzaji

Kihara (2006) katika tasnifu yake ya uzamili alifanya uchunguzi jinsi msimbo wa *Sheng'* unavyotumika katika sajili ya matatu. Katika uchunguzi wake, alithibitisha kuwa uchanganyaji msimbo katika sajili ya matatu hudhihirisha kuwa wazungumzaji hukusudia kufafanua dhana, kuwa wa kuvutia, na kujitambulisha kwa hadhira. Hadhira lengwa kwa muktadha huu ikawa ni abiria. Wahudumu wa sekta ya matatu hubuni aina nyingi za misamiati ili kuwavutia abiria na kujitambulisha katika biashara yao.

Katika data ya utafiti huu, mtafiti alibainisha baadhi ya maneno katika sekta ya uchukuzi wa matatu ambayo dhamira yake ni kuvutia abiria, na kujitambulisha kwa hadhira. Maneno kama *dondoka* (shuka kwa gari), *manyanga* (gari mpya), *matwana* (matatu), *mbu* (basi kubwa), *mtambo* (gari) yanatumika kujitambulisha na kuvutia abiria. Huenda gari likitajwa kuwa *manyanga* au *mbu* linavutia zaidi wateja. Abiria huenda wanavutiwa na umaridadi na umbo la kisasa la magari yanayotajwa kuwa *manyanga*. Ferrari (2014) alionyesha namna wazungumzaji wa *Sheng'* hudhihirisha ubunifu katika kuunda leksimu za *Sheng'*. Alitoa mfano wa neno *baro* ambalo limeundwa kutoka kwa neno *barabara*.

Katika utafiti huu, kuna baadhi ya maneno katika S.E.D yaliyokopwa kutoka lugha changizi. Baada ya kukopwa, baadhi ya silabi hudondoshwa na wakati mwingine irabu kupachikwa kwa konsonanti ya silabi tamati. Katika data ya utafiti huu, mtafiti alibainisha mifano ifuatayo.

**Jedwali 50: Maneno ya S.E.D yanayoonyesha ubunifu.**

| **Maneno ya *Sheng'*** | **Neno asili** | **Lugha changizi** |
|---|---|---|
| Bako | Basketball | Kiingereza |
| Depo | Deputy | Kiingereza |
| Diro | Dirisha | Kiswahili |
| Kago | Cargo | Kiingereza |
| Lebo | Label | Kiingereza |
| Mango | Mangoes | Kiingereza |
| Sato | Saturday | Kiingereza |

Kutokana na jedwali hili, neno *basketball* (mpira wa vikapu) limekopwa kutoka lugha ya Kiingereza. Silabi ***s-et-ba-ll*** zimedondoshwa. Muundo wa neno linalobaki unakuwa *bak*. Irabu **/o/** inapachikwa katika konsonanti /**k/** na kuunda neno *ba**ko***. Neno dirisha, viambishi tamati -***isha*** vimedondoshwa na mahali pake kupachikwa irabu **/o/.** Neno linalozalika linakuwa *diro*. Kando na ubunifu, Githinji (2006) alieleza kuwa leksimu nyingi za *Sheng'* huzuka ili wazungumzaji waweze kujinasibisha katika jamii.

Maelezo ya Githinji (2006) ni kuwa, lugha yaweza kutumika kutenga kikundi fulani cha watu kutoka kingine. Lugha pia yaweza kufanya jamii ya watumizi wa lugha fulani kukubali aina fulani ya watu katika makundi na kuwatenga wengine. Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, mtafiti aligundua neno *rafiki* la KS ambalo katika *Sheng'* limetungiwa visawe. Baadhi ya maneno yaliyogunduliwa yanayorejelea neno *rafiki* ni kama: *tini* (kijana mdogo), *arifu* (rafiki), *laghai* (rafiki wa karibu sana), na *pale* (*rafiki mkuu).*

Maneno haya yamkini hutumika tu na vikundi fulani vya vijana katika miktadha mahsusi. Si rahisi kusikia wazee au wataalam wakitumia maneno haya. Kusudi la kuunda maneno haya ni kuonyesha ubunifu.

### 4.2.4 Mienendo ya kisasa

Githiora (2018) alieleza kuwa baadhi ya maneno katika msimbo wa *Sheng'* huzalika kutokana na matokeo ya mfumo wa kiisimu katika jamii ya kisasa. Jinsi mfumo wa kijamii ya kisasa unavyoendelea ndivyo *Sheng'* inavyooendelea kukua na kubadilika. Kama alivyodai Cheruiyot (2022), Visababishi vya mabadiliko ya lugha hurejelea mambo ambayo huleta mabadiliko na mazingira yanayowezesha mabadiliko. Kwa mujibu wa utafiti huu, athari hizi hujitokeza katika mitandao ya kijamii, muziki wa kufoka (hip hop) na reggae. Nchini Kenya, *Sheng'* imepata umaarufu kwa kujipenyeza katika vyombo vya habari, kampeni za kisiasa na matangazo ya biashara ya kampuni kubwa kubwa. Kutokana na data ya utafiti huu, utafiti uliweza kupata baadhi ya maneno ya *Sheng'* ambayo yamezalika kutoka kwa mienendo ya kisasa.

Neno *soksi* (mipira ya mapenzi) limezalika kutoka lugha ya Kiingereza *soksi*. Katika lugha ya Kiingereza, neno *soksi* lina maana ya *vazi livaliwalo miguuni kabla ya viatu*. Linapoingizwa katika *Sheng'* linapata maana mpya ya *condom*. Hiki ni kifaa kilichotengenezwa kwa jamii ya kisasa kwa ajili ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya ukimwi. Aidha katika data ya utafiti huu, kuna neno *rada* linalotokana na neno la Kiingereza *radar*. Hiki ni kifaa kinachotumika kuelekeza ndege angani na meli baharini. Kwa sababu ya muktadha wa matumizi yake, nahodha wa meli anaweza kuyamudu mazingira yake akiendesha meli. Kwa hivyo *Sheng'* ikabuni neno *rada*

lenye maana ya *kuwa makini ili kuelewa kinachotokea*. Katika sentensi ya *Sheng'*: *Tumekaa rada* inamaanisha; *bado tuko makini na tuanaelewa kinachotokea katika yale mazingira*. Matumizi haya yakipenyezwa katika KS baadaye yataathiri KS. Utaratibu huu wa kuzalisha neno *soksi* na *radar* unatimiza mhimili wa upangiliaji.

Huu ni mhimili uanoamua namna mashartizuizi ya lugha hupangwa katika hali amabayo yaweza kuvumilika. Nano *soksi* limetokana na *socks* la Kiingereza. Neno hili limepitia shartizuizi la muundo wa silabi za Kiswahili kabla ya kukubalika na kuwa *soksi*. Vijana wanakuwa na uwezo wa kubuni misamiati tofauti kutoka mienendo ya kisasa ili kuwawezesha kufanikisha mawasiliano.

### 4.2.5 Hali ya maisha na uchumi

Katika utafiti huu, utafiti uligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* yamebuniwa na kuingizwa katika *Sheng'* kwa sababu ya shughuli za kibiashara na hali ya uchumi ya jamii husika. Baadhi ya maneno yaliyogunduliwa katika S.E.D yanayorejelea shughuli za uchumi na biashara ni kama: *chota* (kutoa pesa), *chukulia* (nunua kitu), *genge* (kazi ya kuajiriwa), *gesi* (kosa pesa), *peremba* (chukuwa pesa), *waya* (kuishiwa na pesa) na *jahi* (tajiri). Kadhalika, utafiti uligundua maneno mengi katika data ya utafiti huu yanayorejelea neno *pesa*. Baadhi ya maneno yaliyobainishwa yanayorejelea *pesa* ni yafuatayo: *kenge (*pesa*)*, *bango* (shilingi moja), *chuma* (shilingi moja), *dafu* (shilingi mia moja), *haja* (shilingi mia moja), *hamasa* (shilingi hamsini), *jongo* (sarafu ya shilingi moja), *kavu* (noti ya shilingi elfu moja), *koma* (shilingi elfu moja), *mbao* (shilingi ishirini), *mwango* (noti ya shilingi mia tano), na *ngiri* (noti ya shilingi elfu moja). Kwa ujumla, kuna maneno 11 katika S.E.D yanayotumika kurejelea *pesa*. Pesa

ni kiungo muhimu sana katika uchumi na biashara. Jinsi wafanyibiashara wanavyoendelea kutagusana katika biashara ndivyo wanavyoendelea kubuni misamiati mingi. Matumizi mapana ya maneno mbadala yanayotumika kuashiria *pesa* yaweza kuhamishwa hadi kwa KS na kwa hivyo kuchangia kupungua kwa matumizi au kupotea kwa neno asilia ambalo ni pesa. Kando na uchumi, hali ya maisha, tabia na mienendo ya vijana huenda inawasukuma kubuni misamiati mbalimbali kuelezea tabia na mienendo yao. Baadhi ya tabia na mienendo inayokinzana na maadili ya jamii imetungiwa misamiati mingi.

Maneno ya kawaida ya KS yanakopwa. Yakiingizwa katika *Sheng'* yanatumika kwa njia ya kimafumbo ili yapate kueleweka tu na vijana pekee katika makundi mahsusi. Katika data ya utafiti huu, utafiti uligundua maneno yaliyoundwa kurejelea mihadarati. Maneno kama; *boza*, *kiapo*, *kitete*, *shada*, *mzizi*, *tembe*, na *ganja* yanatumika kurejelea mihadarati. Neno *bhangi* linawakilishwa na neno *choma*. Kijana akimwambia mwenzake *Nipe choma* (nisadie na bhangi), mzee au mzazi aliye karibu naye huenda hataelewa kinachozungumziwa. Aidha katika S.E.D, neno *miraa*, limeundiwa maneno mengi katika *Sheng'*. Baadhi ya maneno katika S.E.D yanayorejelea *miraa* ni; *fifi*, *gomba*, *andasi*, na *bachu*. Neno *andasi* lilizalika kutoka kwa *andazi* la KS kumaanisha *aina ndogo ya mkate uliokaangwa kwa mafuta* (Kamusi Teule ya Kiswahili, 2003).

Matumizi yake katika *Sheng'* yanadhamiria kuwapotosha wazazi au wazee katika jamii wasielewe kinachomaanishwa katika muktadha huu. Katika sentensi *anakula andasi* (anatafuna miraa) wazazi watafikiri ni *andazi* linalotumika kama chakula na

wala sio *miraa*. *Miraa* ni matawi yanayotafunwa na huchukuliwa kuwa miongoni mwa dawa za kulevya. Wazazi mara nyingi huwa na hofu kuhusu watoto wao wasije wakaanza kutafuna miraa.

Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, utafiti uligundua kuwa neno *miraa* linazalisha aina nyingi ya maneno yenye maumbo tofauti. Maneno haya yanakuwa umboghafi. Hata hivyo kuna yale ambayo yanadumu na hatimaye kuingizwa kwa sarufi ya KS kama vile *andazi*, baada ya kutimiza mashartizuizi. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kufanikisha mawasiliano na kutoa hisia mbalimbali kuhusu neno miraa. Hali hii inaafiki vilivyo msingi wa nadharia ya Fonolojia Boreshi ya uzalishaji. Katika muktadha huu, neno *miraa* linazalisha maumbo tofauti ya maneno kama vile: *fifi, gomba, andasi*, na *bachu*. Maneno haya yanatumika kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji.

### 4.2.6 Kurahisisha mawasiliano

Katika utafiti huu, mtafiti aligundua namna baadhi ya maneno ya *Sheng'* yanavyotumika na wazungumzaji kurahisisha mawasiliano. Kulingana na Ferrari (2014), KS huwa na ngeli 18 kama ifuatavyo: M/WA (1/2), M/MI (3/4), JI/MA (5/6), KI/VI (7/8), N (9/10), U (11:14), KU (15), na PA/KU/MU (16/17/18). Lugha nyingi za Kibantu vile vile huwa na mfumo wa ngeli unaokaribiana na wa KS. Hata hivyo, *Sheng'* ina mfumo wa ngeli ambao ni tofauti na KS. Kulingana na Ferrari (2014), *Sheng'* ina aina mbili kuu za ngeli: maneno yanayorejelea binadamu kama ngeli ya kwanza, na yanayorejelea viumbe na vitu visivyo hai kuwa ngeli ya pili. Katika hali ya udogo maneno ya *Sheng'* huchukua viambishi vya ngeli ya 12/13 ambavyo ni KA/TU.

Kiambishi #***ka#*** hutumika katika umoja na #***tu#*** katika wingi. Maumbo haya ya udogo hayajitokezi katika KS lakini huwa katika lugha za Kibantu kama vile Gikuyu. Mzungumzaji wa KS asipokuwa mwangalifu huenda akaanza kudunisha nomino za KS visivyo kwa kutumia mfumo huu wa *Sheng'*. Kutokana na data ya utafiti huu, mtafiti alijaribu kudunisha baadhi ya nomino ili kutathmini namna udunishaji huu hujitokeza katika *Sheng'*. Jedwali lifuatalo linadhihirisha haya:

**Jedwali 51: Udogo katika *Sheng'***

| **Nomino** | **Udogo katika *Sheng'*** | **Udogo katika KS** |
|---|---|---|
| Mtambo | **Ka**mtambo – **tu**mtamba | Kijitambo - vijitambo |
| Mtumba | **Ka**mtumba – **tu**mtumbo | Kijimtumba – vijitambo |
| Ndusi | **Ka**ndusi – **tu**ndusi | Kijindusi – vijindusi |
| Ngiri | **Ka**ngiri – **tu**ngiri | Kajingiri – vijingiri |
| Paka | **Ka**paka -**tu**paka | Kijipaka – vijipaka |
| Sembe | **Ka**sembe – **tu**sembe | Kisembe – vijisembe |
| Shari | **Ka**shari -**tu**shari | Kijishari - vijishari |

Kutokana na nomino katika jedwali hili, inaonekana wazi kuwa kiambishi cha udogo katika *Sheng'* ni #***ka#*** katika umoja na #***tu#*** katika wingi. Katika KS hali ya udogo kwa umoja hutumia kiambishi #***ki***# na #***vi***# katika wingi. Mifumo hii ya udunishaji wa nomino inazua tofauti kati ya miundo ya maneno ya *Sheng'* na KS. Tofauti hizi zinatokana na athari za lugha za Kibantu ambazo *Sheng'* hukopa leksimu nyingi. Sababu kubwa ya kudunisha maneno ya *Sheng'* kwa kuzingatia mfumo huu, ni kurahisisha mawasiliano. Vijana wengi hawataki kujiingiza katika taratibu za kisarufi za kudunisha maneno ipasavyo. Wanatumia njia ya mkato unaoafiki lugha zao za

kwanza, mradi wametimiza mawasiliano. Huenda wazungumzaji wengi wa *Sheng'* ambao lugha zao za kwanza ni za Kibantu wana maumbo haya ya udogo katika leksimu zao. Kwa hivyo inakuwa rahisi kuyatumia katika *Sheng'* kuliko kutatizika na miundo changamano ya ngeli 18 za KS. Kufupisha kwa ngeli 18 za KS hadi mbili pekee za *Sheng'* ni kwa kusudi la kurahisha mawasiliano.

Kutokana na maelezo haya, mfumo wa kuandika maneno ya *Sheng'* katika hali ya udogo kwa kutumia kiambishi KA/TU, unaojitokeza katika mazingira ya:
{ka} < --- > {tu}. Utaratibu huu unatimiza msingi wa nadharia ya Fonolojia Boreshi ya uzalishi. Msingi huu ni kuwa lugha huwa na jukumu la kuzalisha aina nyingi ya maumbotokeo mbalimbali ili kupasha ujumbe. Uwezo wa vijana kubuni aina nyingi ya maneno kwa kutumia kiambishi KA/TU, unatumiza msingi huu. Vijana wa *Sheng'* wamebuni jamii moja ya mawasiliano. Wametafuta njia ya mkato na urahisi ya kuwasiliana kwa kubuni maumbo ya udogo ya nomino kwa kutumia viambishi **#ka#** na **#tu#.**

**4.2.7 *Sheng'* hutumika kama lugha tenganishi.**

Maoni haya yalichochewa na kauli ya Echessa (1990) kuwa, *Sheng'* ilibuniwa kutosheleza mahitaji ya kijamii ya vijana. Vijana walitambua kuwa lugha zilizokuwepo za KS, Kiingereza na lugha za kienyeji hazikuafiki mahitaji yao ya mtagusano wa kimakundi vilivyo.

Wakaamua kubuni msimbo wao wa lugha ambao ungeweza kutosheleza mahitaji ya mawasiliano miongoni mwao. Maoni haya yanaungwa mkono na Mmbwanga (2016), alipofanya uchunguzi kwa wanafunzi wa chuo kikuu cha Machakos na akagundua

kuwa vijana wengi hutumia *Sheng'* kujitambua na kujitenga na watu wengine. Hii ndio sababu kunazuka misamiati mingi ya *Sheng'* kurejelea dhana inayowakilishwa na maneno ya kawaida ya KS.

Baadhi ya maneno yanayotumika katika *Sheng'* yanadhihirisha kuwa, msimbo huu haukuzuka kwa sababu ya ukosefu wa lugha ya mawasiliano. Tayari vijana walikuwa na lugha zao za kwanza za kutumika katika mawasiliano. Maoni haya yanadhihirishwa na Konnor G. na Hinter M. (2021). Wataalamu hawa wanadai kuwa *Sheng'* ni aina ya lugha ambayo huwaunganisha vijana kwa kuunda makundi madogo madogo yanayodhamiria kujitenga na kuwa tofauti na jamii pana. Haja kubwa ya kutafuta lugha ambayo ingeweza kutumika na vijana kuwasilisha hisia na matakwa yao katika makundi mahsusi ndio iliyowasukuma kubuni msimbo wa *Sheng'*. Kutokana na data ya utafiti huu, mtafiti aligundua baadhi ya maneno ambayo kubuniwa kwake kulikuwa kwa ajili ya kujitenga na jamii pana. Kwa mfano maneno: *chizika, ambaa, kata, kitoe, penya,* na *usuko* yote yanarejelea maana moja ya neno *ondoka.* Neno *ondoka* tayari lilikuwepo katika KS na linaeleweka vyema na jamii pana ya wazungumzaji wa KS.

Mazoea makubwa ya kutumia aina hii ya maneno yanaweza kuchangia katika kupungua kimatumizi kwa baadhi ya maneno ya KS. Kwa hivyo, KS kitaathirika kwa sababu maneno ya *Sheng'* yanapata umaarufu mkubwa kimatumizi kuliko ya KS. Kuzuka kwa maneno haya mbadala, ni dhihirisho tosha kuwa leksimu nyingi za *Sheng'* hubuniwa kwa kusudi la vijana kujitenga na jamii pana kimawasiliano. Kijana akitaka kuondoka katika kundi fulani la watu, huenda akatumia aina hii ya maneno. Jamii pana haitaelewa kinachomaanishwa na maneno haya.

Kando na kujitenga kwa ajili ya kukuza utangamano miongoni mwa vijana, mtafiti aligundua kuwa baadhi ya leksimu za *Sheng'* zinaundwa kutenga makundi ya kihuni ama ujangili. Kutokana na data ya utafiti huu, kuna baadhi ya maneno katika S.E.D yanayotumika kurejelea matendo ya kihuni. Maneno haya ni kama; kupiga/kuumiza mtu. Neno la KS *piga* linapata visawe vifuatavyo: *vunja, unda, vaa, inua, gota, ona, ng'ota,* na *koboa*. Visawe hivi vya neno *piga* ni kwa sababu ya kutumika kutenga kundi fulani la vijana kwa ajili ya kutenda maovu. Vijana wakitumia neno *piga* katika mazungumzo yao huenda hadhira lengwa ikachukuwa hali ya tahadhari mapema ya kujikinga au kuponyoka. Lakini wakitumia neno *koboa*, anayelengwa *kupigwa* hatakuwa na ufahamu. Majangili wakitaka kupiga watu hawatatumia neno *piga* katika mawasiliano bali watatumia baadhi ya hivi visawe ili mtu anayelengwa asije kutambua mipango ya uhuni huu. Kadhalika, polisi na vikosi vya usalama havingeweza kuelewa kusudi la mawasiliano haya kwa sababu neno *piga* limefumbwa.

### 4.2.8 Sababu za tasfida

*Kamusi Teule ya Kiswahili* (2013) inafafanua tasfida kama *mbinu ya utumiaji lugha inayoficha maneno machafu; lugha safi yenye upole*. Katika data ya utafiti huu, mtafiti aliweza kubainisha maneno ya *Sheng'* ambayo yametumika kuficha lugha chafu isiyo na heshima. Mifano imetolewa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 52: Maneno ya tasfida katika S.E.D**

| **Neno katika S.E.D.** | **Maana** |
|---|---|
| Daba | Matako |
| Katia | Tongoza |
| Kiki | Kufa |
| Bomu | Nyamba |
| Jikamua | Kojoa |
| Shonde | Kwenda haja |
| Dodosa | Tingiza kiuno |
| Mango | Matiti |

Maneno katika jedwali la 52 yametumika badala ya maneno asilia ambayo yaweza kuzua aibu, kuchafua roho au kushtua hadhira. Kwa hivyo, wazungumzaji wa *Sheng'* wakaamua kubuni msamiati mbadala kuafiki maana kusudiwa. Mazoea makubwa ya kutumia aina hii ya maneno yanaweza kuchangia katika kupungua kimatumizi kwa baadhi ya maneno ya KS. Hali hii huathiri KS kwa sababu maneno ya *Sheng'* yanapata umaarufu mkubwa kimatumizi kuliko ya KS. Kwa mfano neno *katia* ni maarufu sana miongoni mwa vijana na hutumika katika *Sheng'* badala ya *tongoza*. Kuna hofu kuwa, maana asili ya neno hili yaweza kupotea na mahali pake kuchukuliwa na neno *katia*. Isitoshe, maana sahihi ya neno *katia* jinsi ilivyo katika KS itapotea. Maelezo haya yanatimiza mhimili wa uzalishi kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi. Vijana wakikumbwa na hali ya kuwasiliana kwa lugha ya heshima wanatafakari na kuanza kuzalisha aina nyingi za maneno ya *Sheng'* ili kuficha lugha ya ukali, aibu au kufedhehesha. Neno la KS linalozua aibu kama vile *tongoza* linakuwa umboghafi. Neno linalozalika kama vile *katia* linakuwa umbotokeo. Hata hivyo, kabla ya neno hili kukubalika lazima lipitie katika mhimili wa shartizuizi unaoamua mpangilio wa silabi za *Sheng'*.

## 4.3 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti ameweza kueleza sababu zinazochangia kutokea kwa tofauti kati ya maumbo ya leksimu za *Sheng'* na za KS. Amebainisha sababu kadhaa zinazosababisha tofauti hizi. Sababu hizi ni pamoja na: kuficha siri katika *Sheng'*, athari za lugha changizi, ubunifu wa wazungumzaji, mienendo ya kisasa, hali ya maisha na uchumi, kurahisisha mawasiliano, *Sheng'* kutumika kama lugha tenganishi na sababu za tasfida. Hata hivyo, athari zinazotokana na lugha changizi huchangia pakubwa kutokea kwa tofauti kati ya *Sheng'* na KS. Utafiti uligundua kuwa hali hii hutokea kwa sababu msimbo wa *Sheng'* unavyozidi kukua ndivyo unavyozidi kupanuka kwa kukopa misamiati mingi kutoka lugha zingine. Matumizi haya mapana ya leksimu za *Sheng'* huathiri KS. Kama ilivyodhihirishwa, maneno ya KS yanapokopwa katika *Sheng'* maana asilia hupotoshwa au kubadilishwa kwa kiasi kikubwa.

Utaratibu wa uundaji wa maneno ya *Sheng'* ambayo yanazua tofauti kati ya *Sheng'* na KS yanatimiza msingi wa nadharia ya Fonolojia Boreshi wa uzalishaji. Misingi huu ni kuwa lugha huwa na jukumu la kuzalisha aina nyingi za maneno. Kwa mujibu wa nadharia hii, aina hizi nyingi za maneno hujitokeza kama umboghafi. Maneno yanayoundwa na hatimaye kupata ukubalifu wa kimatumizi katika mawasiliano huwa na umbotokeo. Msingi huu imetumika kuonyesha namna vijana walivyo na uwezo mkubwa wa kuunda aina nyingi za maneno. Maneno yanayoundwa katika muktadha huu yanatumika kueleza hisia za wazungumzaji, kutoa fikra zao na kurekodi habari akilini kuhusu matukio tofauti. Maneno yanayozalika katika *Sheng'* yanakuwa katika

msingi wa uzalishaji ambao umekitwa katika mhmili wa nadharia ya Fonolojia Boreshi wa ukiukwaji. Maneno yanayoafiki sarufi na masharti ya *Sheng'* baada ya kubuniwa hukubalika. Yale yanayokiuka hutupiliwa mbali kwa kukosa kutimiza mashartizuizi.

Hoja hizi zimetimiza vilivyo lengo la tatu la utafiti huu. Lengo hilo ni; kueleza sababu za tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu. Kadhalika, maelezo haya yanatoa majibu mwafaka kwa swali la tatu la utafiti huu ambalo ni: ni sababu zipi za kimuundo zinazoleta tofauti katika matumizi ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu? Sababu zinazochangia kuwepo kwa tofauti kati ya *Sheng'* na KS zimejadiliwa kwa kina. Tofauti hizi zitawasaidia wanafunzi wa Kiswahili kubainisha mipaka iliopo kati ya *Sheng'* na KS ili wasije wakatatizika katika mawasiliano yao.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inadhamiria kutoa muhtasari wa utafiti huu. Kwa kufanya hivyo, itaangazia muhtasari wa kila sura kuanzia sura ya kwanza hadi ya nne. Sura hii pia imetoa maelezo kuhusu matokeo makuu ya utafiti huu kwa kurejelea malengo na maswali ya utafiti. Kusudi la kufanya hivyo ni kudhihirisha namna S.E.D inavyoathiri KS.

### 5.2 Muhtasari wa tasnifu.

Utafiti huu umegawika katika sura tano kuu. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa mada, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Malengo ya utafiti yalikuwa matatu. Lengo la kwanza lilikuwa, kubainisha maneno yaliyomo katika *Sheng'- English Dictionary* na katika Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa utafiti huu, lengo hili limeweza kufanikiwa kwa sababu maneno yanayojitokeza katika S.E.D na KS yamebainishwa. Lengo la pili lilikuwa, kuonyesha miundo ya kifonolojia ya maneno ya *Sheng'* na namna inavyotofautiana na KS. Mtafiti ameweza kuonyesha aina tofauti za miundo ya kifonolojia ya *Sheng'* na kudhihirisha jinsi inavyotofautiana na KS. Lengo la tatu lilikuwa, kutoa sababu zinazochangia kuzuka kwa tofauti kati ya fonolojia ya *Sheng'* na KS. Mtafiti amefanikiwa kutoa sababu kadhaa ili kutimiza lengo hili.

Nadharia ya Fonolojia Boreshi imetumiwa na mtafiti kuchunguza na kuchanganua malengo ya utafiti huu. Amechunguza namna maneno ya *Sheng'* yanavyokopwa na kushirikishwa kupitia mashartizuizi mbalimbali kabla ya kukubalika katika lugha pokezi. Mtafiti ameweza kuonyesha namna mihimili ya nadharia hii inavyoshiriki kuteua maumbo mbalimbali ya leksimu za *Sheng'*. Nadharia hii ina mihimili minne mikuu. Mihimili hii ni; umajumui, ukiukwaji, upangiliaji na usambamba.

Mihimili hii inadhihirika katika misingi mitatu mikuu ambayo ni; msingi wa uzalishi, msingi wa mashartizuizi na msingi wa utathmini**.** Mtafiti ameweza kuonyesha namna misingi hii hushiriki kuteua aina mbalimbali za maneno kutoka lugha changizi. Baada ya maneno kukopwa, mtafiti ameonyesha jinsi mashartizuizi mbalimbali ya kifonolojia hushiriki kuteua neno mwafaka kutoka kwa aina nyingi za maneno shindani na hatimaye kukubalika hadi lugha pokezi.

Sura ya pili imeangazia lengo la kwanza la utafiti. Lengo hili ni; kubaini aina mbalimbali za maneno yaliyo katika S.E.D na vilevile katika KS. Lengo hili la utafiti limeambatana na swali la kwanza la utafiti huu ambalo ni: maneno yapi yaliyojitokeza katika *Sheng'-English Dictionary* na ambayo yapo katika Kiswahili sanifu? Mtafiti ameweza kubainisha aina tofauti za maneno na kuyaoredhesha kwa majedwali na kuyafanyia uchanganuzi wa kina. Ameweza kuyagawa maneno katika makundi matano makuu. Makundi haya ni nomino, vivumishi, vitenzi, vielezi na vihusishi. Miundo tofauti ya maneno haya imebainishwa na kuchunguzwa kwa kutumia majedwali na maelezo kwa kina.

Sura ya tatu inaeleza miundo ya kifonolojia ya maneno ya *Sheng'* na namna inavyotofautiana na KS. Vipashio vya kifonolojia vinavyojumuisha fonimu za irabu na konsonanti vimejadiliwa. Isitoshe, vipengele vya fonolojia arudhi kama vile toni na shadda vimeangaziwa katika sura hii. Aidha, sababu zinazochangia kuzuka kwa tofauti za fonolojia kimuundo zimejadiliwa. Mifano maridhawa ya miundo tofauti ya maneno ya *Sheng'* imetolewa na kuilinganisha na ya KS.

Katika sura ya nne, mtafiti amechunguza na kubainisha sababu zinazochangia muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* kuwa tofauti na KS. Ili kufanikisha uchunguzi huu ametumia msingi wa uzalishaji katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Msingu huu umeshirikishwa kuchunguza jinsi maneno mbalimbali huundwa kwa kufuata taratibu za msimbo wa *Sheng'*. Maneno yanayokiuka taratibu hizi yanapuuzwa kimatumizi na yale yanayotimiza yanatumika katika mawasiliano.

Msingi huu ndio uliotumiwa na mtafiti kuchanganua data ya utafiti kwa mujibu wa lengo la tatu la utafiti. Lengo hilo lilikuwa: kueleza sababu za tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na kueleza athari zake kwa Kiswahili sanifu. Sababu kadhaa zinazochangia tofauti ya kimuundo ya maneno ya *Sheng'* zimejadiliwa na athari zake kuelezwa. Maelezo hayo yamejibu swali la tatu la utafiti huu ambalo ni: ni sababu zipi za kimuundo zinazoleta tofauti katika matumizi ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu? Mtafiti ameeleza sababu kadha ambazo husababisha kutokea kwa tofauti za muundo wa kifonolojia kati ya *Sheng'* na KS.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Mtafiti ameweza kugawa matokeo ya utafiti katika viwango vitatu. Kiwango cha kwanza kimetimiza lengo la kwanza la utafiti ambalo linajitokeza katika sura ya pili. Lengo hili ni: kubainisha maneno yaliyomo katika *Sheng'- English Dictionary* na katika Kiswahili sanifu. Lengo hili linaambatana na swali la kwanza la utafiti ambalo ni: ni maneno yapi yaliyojitokeza katika *S.E.D* na ambayo yapo katika KS? Kiwango cha pili ni kuonyesha miundo mbalimbali ya kifonolojia ya maneno ya *Sheng'* na jinsi miundo hiyo huwa tofauti na KS. Kiwango hiki kimekusudia kutimiza lengo la pili la utafiti ambalo ni, kuonyesha namna miundo ya maneno ya *Sheng'* inavyotofautiana na KS. Kiwango cha tatu ni kutimiza lengo la tatu la utafiti ambalo ni kubainisha sababu zinazosababisha kutokea kwa tofauti za kifonolojia kati ya maneno ya *Sheng'* na ya KS. Kwa mujibu wa utafiti huu, malengo haya yote ya utafiti yametimizwa kama itakavyodhihirika katika maelezo yanayofuata.

### 5.3.1 Ubainishaji wa maneno katika S.E.D

Utafiti umebainisha maneno yanayojitokeza katika S.E.D na ambayo hutumika katika KS. Baada ya kuyabainisha, mtafiti ameeleza tofauti za kisemantiki zinazojitokeza katika maneno haya. Hii ni kwa sababu amegundua kuwa, maneno hayo yanaweza kugawika katika makundi mbalimbali.

Mgao huo kimakundi hutumia vigezo tofauti ili kutathmini maana za maneno husika. Vigezo alivyotumia kugawa haya maneno ni polisemi, sinonimu na uhamishaji wa maana. Kwanza, mtafiti aliweza kuorodhesha jumla ya nomino 106 kati ya maneno 335 yaliyobainishwa katika S.E.D. Hii ni asilimia 51.46 ya idadi ya maneno. Kisha,

aliweza kubainisha vitenzi 82 ambavyo vinajitokeza katika S.E.D na pia katika KS. Hii ni asilimia 38.8 ya maneno yote yaliyo katika S.E.D na KS. Vivumishi ambavyo vinapatikana katika S.E.D na kisha kujitokeza katika KS ni 13. Hii ni asilimia 5.88 ya jumla ya idadi ya maneno. Mtafiti ameweza kubainisha vihusishi vinne katika orodha ya maneno 335 yanayopatikana katika S.E.D na kisha katika KS. Hii ni asilimia 1.96. Aidha, mtafiti alibainisha vielezi vinne. Hata hivyo, amegundua kuwa idadi kubwa ya vielezi katika *Sheng'* imeweza kubuniwa na kutumika katika mazungumzo kwa kutumia viambishi #***ki***# au #***vi***# kama viambishi awali kwa baadhi ya vielezi.

Mtafiti ameonyesha kuwa, nomino nyingi na baadhi ya vitenzi zikipachikwa kiambishi awali #***ki***#, au #***vi***# hubadilisha hilo neno na kuwa kielezi. Baada ya kubainisha aina tofauti za maneno, mtafiti ameweza kuyaoredhesha maneno yote yanayopatikana katika S.E.D na katika KS kiabjadi. Ameweza kugundua kuwa, maneno yanayoanza kwa herufi **m** yana idadi kubwa ya maneno ambayo ni 357. Hii ni asilimia 20 ya jumla ya idadi ya maneno yaliyomo katika S.E.D. Hali hii inatokana na dhana kuwa, maneno mengi ya *Sheng'* yanatokana na lugha za Kibantu ambazo huwa na leksimu nyingi zinazoanza kwa herufi **m**.

Hata yale ambayo yanakopwa kutoka kwa lugha zisizo za Kibantu kama vile Kiingereza na lugha za Kinailoti, maneno mengi hulazimika kuchukua herufi /**m/** kama kiambishi awali ili kutoa uamilifu wa sarufi ya *Sheng'*. Mtafiti ameonyesha kuwa maneno yanayoanza kwa abjadi /***y*** yana idadi ndogo sana ya leksimu, ambayo ni

4. Hii ni asilimia 0.22. Baada ya kubainisha maneno ya S.E.D katika viwango tofauti, mtafiti ameweza kueleza sifa za kisemantiki za maneno katika S.E.D.

Kwanza, ametumia kigezo cha kisemantiki cha uhamishaji maana. Ameonyesha namna neno la Kihindi *boza* linalomaanisha aina fulani ya pombe linavyopata maana mpya ya *bangi* katika *Sheng'*. Isitoshe, mtafiti ametumia kigezo cha kisemantiki cha polisemi kubainisha baadhi ya meneno. Ameonyesha jinsi neno *mbuyu* (aina ya mti) la KS linavyobadilishwa maana na kuwa *baba*. Aidha, ametumia kigezo cha sinonimu ili kubainisha aina tofauti za maneno katika S.E.D. Mtafiti ameweza kugawa sinonimu katika makundi matatu. Sinonimu jozi, sinonimu utatu na sinonimu unne. Katika sinonimu jozi ametoa mfano wa neno *ngoma* (muziki) ambalo kisawe chake ni *mahewa*. Katika sinonimu utatu, neno gari linapata visawe vitatu ambavyo ni; *moti*, *dinga* na *buu*.

Utafiti pia umebainisha maneno ya *Sheng'* yanayojitokeza katika miktadha tofauti. Katika muktadha wa vyombo vya habari, mifano ya maneno ya S.E.D yanayotumika katika gazeti la *Taifa Leo* imeonyeshwa. Gazeti hili lina ukurasa mahsusi wa *Dondoo* za *Hapa na Pale* ambao hutumia *Sheng'*. Ametoa mfano wa maneno katika kurasa hizi kama vile *jombi* (mwanamume msherati), *manzi* (mpenzi wa kike), *kalameni* (mwanamume mkora) na *msupuu* (msichana mrembo).

Katika muktadha wa mitandao ya kijamii, mtafiti amefanikiwa kubainisha maneno ya *Sheng'* kama vile *sasa* (hujambo), *Poa* (nimetulia), *Shags* (mashambani), *Buru* (mtaa wa Buruburu). *Juu ya* (kwa sababu), na *Set* (kuanza). Katika sekta ya Jua Kali, mtafiti

amefanikiwa kubainisha mifano ifuatayo ya maneno: *kago* (vitu vya thamana) na *burungo* (mizigo mingi iliyotapakaa na kutawanyika kwa wingi). Katika muktadha wa matangazo ya biashara, mtafiti ameweza kubainisha maneno yafutatayo: *ashara* (shilingi kumi) *brandi* (kuwa mpya), *chapaa* (pesa), *chota* (kutoa pesa), *doo* (pesa), na *fashoni* (mdundo wa mavazi wa kisasa).

Katika muktadha wa usafiri wa matatu, mtafiti aliweza kubainisha maneno ya *Sheng'* kama vile *trek* (kutembea), *tao* (mji), *chapaa* (pesa), *inua* (beba), *sambaza* (enea), *nyonga* (pindua gari) na *uza* (badilisha abiria kutoka gari moja hadi lingine). Ubainishaji huu wa aina mbalimbali za maneno katika S.E.D na KS umetosha kuthibitisha kuwa lengo la kwanza la utafiti huu limetimizwa. Lengo hili lilikuwa kubainisha maneno ya *Sheng'* yanayojitokeza katika S.E.D na kisha KS.

### 5.3.2 Muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'*

Lengo la pili la utafiti huu limekuwa kueleza muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* na kuonyesha namna unavyotofautiana na wa KS. Lengo hili linaambatana na swali la pili la utafiti ambalo ni: muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* unatofautiana vipi na Kiswahili sanifu? Mtafiti ameweza kutimiza lengo hili kwa kuonyesha miundo mbalimbali ya fonolojia ya *Sheng'* na jinsi inavyotofautiana na KS. Kwanza, ameonyesha namna fonolojia vipande sauti inavyotumika katika ubainishaji wa vipande sauti maalum katika *Sheng'*. Amejikita katika kuchunguza namna fonimu za *Sheng'* zinavyodhihirika na kuathiri KS. Utafiti umeonyesha namna sauti mbalimbali za vokali na konsonanti zinavyoshiriki katika kujenga na kutofautisha maana katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Ametoa mfano wa neno la KS *mzee*

linalobadilika na kuwa *msee* katika *Sheng'*. Kikwamizo ghuna cha ufizi **/z/** kinabadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na kikwamizo cha ufizi sighuna **/s/.** Utafiti huu umedhihirisha kuwepo kwa mifanyiko mbalimbali ya kifonolojia katika *Sheng'*. Mifanyiko hii ni kuhafifika kwa fonimu, usilimishwaji wa fonimu, udondoshaji wa silabi na tangamano la irabu. Utafiti umeonyesha jinsi mfanyiko wa kuhafifika kwa fonimu unavyojitokeza katika *Sheng'*. Utafiti umeeleza kuwa, fonimu hubadilika kiasi kwamba fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu zaidi hubadilishwa na ile fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo.

Mtafiti alitoa mfano wa neno la *Sheng' buyu* (baba) kudhihirisha mfanyiko huu. Udogo wake katika KS linakuwa *ki**j**ibuyu* (tunda ndogo la mbuyu) na katika *Sheng'* linakuwa *k**a**buyu*. Mtafiti amedhihirika kuwa irabu **/i/** katika silabi #**ki#** inadondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu **/a/**. Katika matamshi, irabu **/a/** hutamkika kwa sauti hafifu ikilinganishwa na **/i/**. Utafiti umedhihirisha namna usilimishwaji wa fonimu unavyojitokeza katika *Sheng'*.

Kipashio jirani katika neno huweza kuathiriwa na kipashio kingine kilicho mkabala nacho na hivyo kuchukua sifa za kimatamshi za kipashio hicho jirani. Usilimishwaji umebainika katika mifano ifuatayo: *wa**z**ee* – *wa**s**ee* (sauti ***/z/*** kubadilika na kuwa /***s***/). Jersy – jazi (sauti ***/s/*** kubadilika na kuwa ***/z/***. Katika udondoshaji wa silabi za maneno ya S.E.D, mtafiti amegundua kuwa udondoshaji wa silabi nzima ndio hujitokeza kwa wingi katika baadhi ya maneno. Mtafiti ametoa mfano wa neno *Pangani* ambalo silabi #***ni***# imedondoshwa na kuwa *Panga*. Aidha, utafiti umeonyesha jinsi mfanyiko wa tangamano la irabu unavyojitokeza. Irabu ambazo huwa katika mzizi wa neno,

hujitokeza vilevile kwa baadhi ya viambishi tamati. Ametoa mfano wa neno *ch**o**ma* ambalo linakuwa *ch**o**m**o**ka* na *t**o**b**o**a* linakuwa *t**o**b**o**ka*. Kutokana na mifano hii, irabu **/o/** inashiriki kuunda mzizi wa neno na kisha kuunda viambishi.

Utafiti huu umethibitisha kuwa *Sheng'* ina vokali saba. Imedhihirika kuwa *Sheng'* imekopa sauti za irabu ***/ɛ/** na **/ɔ/*** kutoka kwa lugha za kibantu. Mtafiti amezifafanua irabu hizi za *Sheng'* kwa kuzingatia sehemu ya kuzitamkia na mwinuko wa ulimi katika kinywa. Kuhusu mahali pa kutamkia vokali, ameonyesha sehemu tatu kuu zinazotumiwa kuzitofautisha. Sehemu hizo ni: sehemu ya ulimi ya mbele, sehemu ya kati na sehemu ya ulimi nyuma. Kwa kufanya hivyo, utafiti umeonyesha namna irabu za *Sheng'* huwa tofauti na za KS. Utafiti umedhihirisha kuwa idadi ya konsonanti za *Sheng'* ni tofauti na ya KS. *Sheng'* ina konsonanti 28 ambazo ni: /b/ /c/ /d/ /f/ /g/ /j/ /k/ /l/ /m/ mb/ /n/ /nd/ /ɲʃ/ /nt/ / ŋ/ /nŋ/ /ð/ /ɲ/ /p/ /r/ /s/ /s/ /t/ /ts/ /θ/ /w/ /v/ /z/.

Utafiti umethibitisha kuwa kuna konsonanti za *Sheng'* ambazo hazipatikani katika KS nazo ni*:* *nt, ts, ɲʃ*, na *c*. Utafiti huu umedhihirisha kuwa *Sheng'* ina silabi funge na silabi wazi. Mtafiti ametoa mfano wa neno *kinda* (iba, saliti) ambalo lina silabi mbili. Silabi hizi ni #-**ki#** na **#-nda#.** Silabi hizi ni silabi wazi kwa sababu zinaishia kwa irabu ***/i/*** na ***/a/*** mtawalia. Kadhalika, mtafiti ametoa mfano wa neno ***mas**kani* (chumba cha kujificha). Neno hili limeundwa kutokana na silabi #**mas**$**ka**$**ni#.** Silabi #**mas**# ni funge, ilhali silabi #**ka#** na #**ni#** ni wazi. Kutokana na utaratibu huu, mtafiti amegundua kuwa maneno mengi ya *Sheng'* huundwa kwa silabi wazi.

Hata maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiingereza, na yanaoishia kwa silabi ya konsonanti tu, hulazimika kuchukua irabu na kuwa silabi wazi. Utafiti umegundua kuwa baadhi ya vitenzi vya *Sheng'* huchukua kiambishi cha hali isiyodhihirika #***nga#***.

Imedhihirika kuwa, kiambishi #***nga#*** hutumika katika hali zote za nyakati na hali. Ikiwa kitenzi katika hali ya kutenda huishia kwa irabu ***/a/*** basi silabi #***nga#*** hupachikwa kwenye kitenzi. Hata hivyo, ikiwa kitenzi kina irabu ***/i/*** basi silabi #***ngi***# itatumika. Kigezo hiki kinafanya silabi hii kuzua tofauti kubwa kati ya KS na *Sheng'*. Katika ukanushi, kiambishi hiki hubadilika na kuwa #***ngi***#. Mtafiti amefanikiwa kuonyesha jinsi baadhi ya vitenzi vilivyo katika S.E.D vinavyoweza kuchukua silabi #***nga***# katika kuonyesha nyakati na hali tofauti katika sentensi. Ametoa mifano ya vitenzi kama; *amezea**nga*** na *amepenya**nga*** kudhihirisha hali hii**.** Katika ukanushi utafiti umeonyesha namna kiambishi #***nga#*** hubadilika na kuwa #***ngi#***. Kitenzi *amezea**nga*** kinakanushwa na kuwa *amezea**ngi*** nacho kitenzi *amepenya**nga*** kinakanushwa na kuwa *apenya**ngi***. Utafiti huu umefanikiwa kuonyesha kuwa matumizi haya ya kiambishi #***nga#*** na #***ngi***# ni tofauti na jinsi ilivyo katika KS ambapo vitenzi vya hali ya ukanushi huchukua kiambishi tamati #***ki***#.

Kadhalika, utafiti umeonyesha kuwa baadhi ya vivumishi vya *Sheng'* huundwa kutoka kwa vitenzi na nomino. Nomino hizi na vitenzi aghalabu huwa zimekopwa. Baada ya kukopwa, hupachikwa kipasuo ghuna cha mdomo ***/m/*** kinachotiwa kabla ya mzizi, na kubadilisha maneno hayo kuwa vivumishi. Maneno supu-**m**supu (mrembo sana), poa-**m**poa- (mzuri) na chafu-**m**chafu (mtaalamu /mwerevu) imetolewa kama mifano

kudhihirisha hali hii. Utafiti huu umedhihirisha kuwa, vielezi vingi vya *Sheng'* huundwa kutoka kwa nomino au vivumishi ambavyo hukopwa kutoka lugha zingine. Kiambishi #***ki***# au #***vi#*** kinapotiwa kwa baadhi ya nomino na vitenzi, hubadilika na kuwa vielezi. Mtafiti ametoa mfano wa kielezi *poa* ambacho kikichukua silabi #***vi***# kinabadilika na kuwa kielezi ***vi****poa*. Sifa za arudhi za *Sheng'* zimejadiliwa na kuonyesha jinsi zinavyozua tofauti kati ya *Sheng'* na KS. Utafiti umegundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* huwa na shadda mwishoni mwa neno. Maneno yenye sauti ya mvuto kama *amba**a*** hutiwa shadda kwa irabu ya mwisho /**a**/. Hali hii hufanya irabu ya mwisho kuwa silabi tofauti inayojisimamia. Kando na maneno yenye silabi za mvuto, mtafiti ametoa mfano wa neno *seti*. Katika KS, neno hili hutiwa shadda katika silabi ya pili kutoka mwisho na kuwa '***se***- *ti***.** Hata hivyo, katika *Sheng'* neno hili hutiwa shadda katika silabi tamati na kuwa *se*- *'**ti.*** Hili ni dhihirisho tosha kuwa matumizi ya shadda katika *Sheng'* huzua tofauti na KS. Utafiti huu umebainisha baadhi ya maneno katika S.E.D ambayo huwa na maana tofauti kwa sababu ya toni.

Utafiti umetoa mfano wa neno *zima* linalokuwa na maana mbili. Likitamkwa bila toni linamaanisha *tuliza*. Toni ikitiwa kwa irabu /**a**/ inabadilisha maana ya neno na kuwa *zima**a*** lenye maana ya mtaa wa Zimmerman mjini Nairobi. Hali hii inafanya *Sheng'* kuwa tofauti na KS kwa sababu kulingana na Kindija (2014), toni haipatikani katika KS. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa lengo la pili la utafiti huu limetimizwa. Lengo hili lilikuwa kubainisha tofauti za miundo ya kifonolojia kati ya *Sheng'* na KS.

### 5.3.3 Sababu za tofauti za kimuundo katika matumizi ya Sheng' na Kiswahili sanifu.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa: kueleza sababu za tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu. Lengo hili linaambatana na swali la tatu la utafiti. Swali hili ni: ni sababu zipi za kimuundo zinazoleta tofauti katika matumizi ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu? Utafiti huu umeeleza na kufafanua sababu kadhaa zinazofanya *Sheng'* kuwa na muundo tofauti wa kifonolojia na KS. Utafiti umeweza kubainisha sababu nane kuu. Nazo ni: kuficha siri katika *Sheng',* athari za Lugha changizi, ubunifu wa wazungumzaji, mienendo ya kisasa, hali ya maisha na uchumi, kurahisisha mawasiliano, *Sheng'* hutumika kama lugha tenganishi na sababu za tasfida. Katika kuficha siri, utafiti ulitoa mfano wa neno la KS *msichana*. Neno hili limetungiwa visawe vingi vinavyotumika katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano.

Baadhi ya visawe ambavyo mtafiti aligundua vinavyotumika katika *Sheng'* badala ya neno *msichana* ni kama: *babe, kifaranga, lebo, matunda, mwasi, shaba, shabu,* na *toti*. Kutokana na mifano hii, mtafiti ameweza kuonyesha kuwa lengo kuu la vijana kubuni aina nyingi ya maneno kurejelea neno *msichana* ni kuficha siri. Sababu ya pili iliyobainishwa na utafiti huu ya kuwepo kwa tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na KS ni athari za lugha changizi. Utafiti umebainisha kuwa *Sheng'* ina irabu saba ilhali KS kina irabu tano. Yamkinika kuwa irabu mbili za ziada zimekopwa kutoka lugha zingine za Kibantu kama vile Gikuyu na Ekegusii. Irabu zilizobainishwa ni; */a/, /e/*, **/ɛ/**, */i/, /o/, /ɔ / na /u/*. Utafiti huu umedhihirisha kuwa irabu */ɛ/ na /ɔ/* zimekopwa kutoka lugha za Kibantu ikiwemo Ekegusii. Hali hii inazua tofauti kati ya *Sheng'* na KS. Utafiti umeonyesha kuwa msimbo wa *Sheng'* umekopa muundo wa

uundaji wa baadhi ya maneno kutoka Dholuo. Nomino za pekee katika lugha ya Dholuo aghalabu hupachikwa irabu /**o**/ katika silabi tamati. Utafiti umebainisha kuwa, kuna baadhi ya maneno ambayo huundwa kwa kupachikwa irabu ***/o/*** au */ɔ/* katika silabi ya tamati.

Maneno kama *dago* (mtaa wa Dagoretti mjini Nairobi), *diro* (dirisha), *pango* (mtaa wa Pangani mjini Nairobi) na *bako* (mchezo wa vikapu) yameambishwa irabu ***/o/***.

Kando na lugha changizi, utafiti huu umeonyesha namna ubunifu wa wazungumzaji unavyozua tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na KS. Utafiti umedokeza maneno katika sekta ya uchukuzi ambayo dhamira yake ni kuvutia, na kujitambulisha kwa hadhira. Maneno kama *dondoka* (shuka kwa gari), *manyanga* (gari la matatu maridadi), *matwana* (matatu), *mbu* (basi kubwa), *mtambo* (gari) yamebuniwa na washikadau katika sekta ya matatu ili kujitambulisha na kuvutia abiria. Utafiti umedhihirisha kuwa neno *manyanga* au *mbu* limebuniwa kuvutia zaidi wateja. Abiria huenda wanavutiwa na umaridadi na umbo la kisasa la magari yanayotajwa kuwa *manyanga*. Utafiti huu umeonyesha jinsi mienendo ya kisasa inavyozua tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na KS. Mtafiti ametoa mfano wa neno *soksi* (mipira ya mapenzi) ambalo limezalika kutoka lugha ya Kiingereza *soksi*. Ameeleza kuwa neno *soksi* katika Kiingereza lina maana ya *vazi livaliwalo miguuni kabla ya viatu*.

Linapoingizwa katika *Sheng'* linapata maana mpya ya *condom*. *Condom* ni kifaa kilichotengenezwa na jamii ya kisasa kwa ajili ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya ukimwi. Hii ni ishara tosha kuwa mienendo ya kisasa huchangia kuzuka kwa leksimu

mpya katika msimbo wa *Sheng'*. Kadhalika, utafiti umegundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* yamebuniwa na kuingizwa katika *Sheng'* kwa sababu ya shughuli za kibiashara na hali ya uchumi. Hili limedhihirika kwa mifano ya maneno kama: *chota* (kutoa pesa), *chukulia* (nunua kitu), *genge* (kazi ya kuajiriwa), *gesi* (kosa pesa), *peremba* (chukuwa pesa), *waya* (kuishiwa na pesa) na *jahi* (tajiri). Isitoshe, utafiti umegundua maneno yaliyoundwa kurejelea mihadarati. Maneno kama; *boza, kiapo, kitete, shada, mzizi, tembe,* na *ganja* yanatumika kurejelea mihadarati. Nalo neno *bhangi* linawakilishwa na neno *choma*. Mifano hii inadhihirisha kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* huundwa ili kuafiki matakwa ya kibiashara na uchumi.

Utafiti huu umethibitisha namna baadhi ya maneno ya *Sheng'* yanavyotumika na wazungumzaji kurahisisha mawasiliano. Utafiti umegundua kuwa *Sheng'* ina aina mbili kuu za ngeli: maneno yanayorejelea binadamu kama ngeli ya kwanza, na yanayorejelea viumbe/vitu visivyo hai kuwa ngeli ya pili. Katika hali ya udogo maneno ya *Sheng'* huchukua viambishi vya ngeli ya 12/13 ambavyo ni KA/TU. *KA* hutumika katika umoja na *TU* katika wingi. Utafiti umeonyesha kuwa maumbo haya ya udogo hayajitokezi katika KS lakini huwa katika lugha za Kibantu kama vile Gikuyu. Utafiti umetoa mfano wa neno *mtambo*. Udogo wa neno hili katika *Sheng'* likiwa kwa umoja ni *kamtambo*, wingi wake ni *tumtambo*. Hata hivyo, udogo wa neno hili katika KS ni *kijitambo* na wingi ni *vijitambo*. Maumbo haya ya udogo husababisha tofauti kati ya *Sheng'* na KS. Utafiti huu umeonyesha kuwa *Sheng'* ni msimbo wa lugha tenganishi. Lugha tenganishi hukusudia kuwatenga wazungumzaji katika miktadha mahsusi ya jamii. Mtafiti ametoa mfano wa maneno: *chizika, ambaa, kata, kitoe, penya,* na *usuko* ambayo yote yanarejelea maana moja ya neno *ondoka*. Neno

*ondoka* tayari liko katika KS na linaeleweka vyema na jamii pana ya wazungumzaji wa KS.

Kwa mujibu wa utafiti huu, kuzuka kwa maneno haya mbadala, ni dhihirisho tosha kuwa leksimu nyingi za *Sheng'* hubuniwa kwa kusudi la vijana kujitenga na jamii pana kimawasiliano. Mwisho, utafiti huu umedhihirisha kuwa baadhi ya maneno yamebuniwa katika *Sheng'* kwa sababu ya tasfida. Utafiti umeonyesha baadhi ya maneno yanayotumika badala ya maneno asilia ambayo yaweza kuzua aibu, kuchafua roho au kushtua hadhira. Kwa mfano, mtafiti ameonyesha neno *katia* ambalo ni maarufu sana miongoni mwa vijana. Neno hili hutumika katika *Sheng'* badala ya neno *tongoza*. Matumizi ya neno *tongoza* huzua aibu na huonyesha upotovu wa maadili likitumika katika mawasiliano. Ikabidi vijana kubuni neno mbadala, *katia* ili kutumika mahali pake. Maelezo haya yanatosha kuthibitisha kuwa lengo la tatu la utafiti huu limetimizwa. Lengo hili lilikuwa: kueleza sababu za tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na Kiswahili sanifu. Maelezo haya ni ithibati tosha kuwa utafiti umeweza kutimiza lengo la tatu la utafiti huu ambalo ni kueleza tofauti za kimuundo katika matumizi ya *Sheng'* na KS.

**5.4 Changamoto za utafiti.**

Changamoto kuu katika utafiti huu ilikuwa data ya maneno yalioyotumiwa kama msingi wa utafiti mengi hayajadumu hadi sasa katika mawasiliano ya kisasa. Hali hii iliathiri uhalali na uchanganuzi wa data ya utafiti kwa sababu ilifaa kuchunguza baadhi ya maneno yalivyokua na kuyalinganisha na Kiswahili sanifu cha sasa. Kadhalika, baadhi ya maneno ya *Sheng'* hutupiliwa mbali baada ya matumizi ya kipindi fulani na

mengine hupata maana mpya iliyo tofauti mno na matumizi yake ya awali. Kuchunguza muundo wa kifonolojia wa maneno hayo kwa kuyalinganisha na maneno yaliyo katika kamusi za kisasa kunazua tatizo la kiuchanganuzi. Hata hivyo, mtafiti aliweza kusuluhisha tatizo hili kwa kuteua sampuli ya maneno ambayo hutumika katika *Sheng'* na Kiswahili Sanifu.  Madai ya Salome' (2020) kuwa maneno mengi ya *Sheng'* hukopwa kutoka lugha za kienyeji zaidi ya 40 yalionyesha ugumu wa kuelewa maana asilia ya baadhi ya maneno ya *Sheng'* ambayo yalikopwa kutoka lugha hizi.

## 5.5 Mapendekezo ya utafiti zaidi

Utafiti huu umedhihirisha kuwa kuna athari za kifonolojia za S.E.D kwa KS. Uchunguzi huu umejikita katika kutathmini namna *Sheng'* inavyoathiri KS kifonolojia. Hata hivyo, uchunguzi zaidi waweza kufanywa ili kuangazia namna *Sheng'* inavyoathiri KS kwa kuchunguza viwango vingine vya isimu kama vile mofolojia, semantiki na sintaksia. Kadhalika, uchunguzi huu umeegemea zaidi kamusi ya S.E.D kama msingi wa data. Tafiti zaidi zaweza kufanywa kwa kuchunguza kamusi zingine za *Sheng'* zilizochapishwa baada ya chapisho la S.E.D (2003).

**MAREJELEO**


Bosire, M. (2006). *Hybrid languages: The Case of Sheng.* State University of New York, Albany.

Bosire, M. (2014). *Sheng: The phonology, morphology and social profile of an urban vernacular*. Tasnifu ya uzamifu. University at Albany, State University of New York.

Bwenge, C. (1995). *Utafiti wa maana za maneno ya kamusi: Uzoefu wa kutafiti msamiati wa Kamusi ya Kiswahili sanifu.* Katika Kiango J. na Mdee, J. (Wahariri), *Utafiti na utungaji wa kamusi*. Dar es Salaam: TUKI.

Cheruiyot, E. (2022). *Sababu za Kudondoshwa kwa Fonimu za Likwidi katika Maneno Teule. Editon Cons. J. Kiswahili,* 4(1), 348-355. DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.299

Chimera, R. (2000). *Kiswahili past, present and future horizons*. Nairobi: Nairobi University press.

Echessa, R. (1990). *A Study of word structure and processes involved in Sheng' Word formation.* Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

East African Educational Publishers. (2013). *Kamusi Teule ya Kiswahili*. Nairobi. EAEP.

Ferrari, A. (2014). *Evolution of Sheng during the Last Decade.* Les Cahiers d'Afrique de l'Est / The East African Review, 49 | 2014, 29-54.

Githinji, P. (2006). *Bazes and their Shibboleths: Lexical variation and Sheng speaker's identity in Nairobi.* Ohio University, United State.Nordic Journal of African Studies 15(4): 443–472 (2006)

Githinji, P. (2022). *Strategies for Identifying Sheng: What counts as Sheng?* Kenyatta University. file:///C:/Users/ADMIN/Downloads/249-Article %20Text-381-1-10-20221108.pdf

Githiora, C. (2002). *Sheng: Peer language, Swahili dialect or emerging Creole?* https: //www.researchgate.net/publication/248968711 Sheng Peer language Swahili dialect or emerging Creole.

Githiora, C. (2018). *Sheng': Rise of a Kenyan swahili vernacular.* London: James Currey.

Jomo Kenyatta Foundation. (2016). *Kamusi Elezi ya Kiswahili.* Nairobi. JKF.

Kager, R (1999). *Optimality theory.* London: Cambridge.

Kang'ethe-Iraki, F. (2004). *Cognitive efficiency: The sheng phenomenon in Kenya.* Journal in International Pragmatics Association. http:// erepo.usiu.ac.ke.

Kihara, D. (2006). *Uchambuzi wa matini: matumizi ya lugha katika sajili ya matatu*. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Kihara, D. (2016). *Uundaji, udumishaji na mabadiliko ya leksimu katika Sheng' ya matatu.* http://erepository.mku.ac.ke/handle/123456789/5482

Kihara, P. na Schröder, H. (2012). *A Relevance-theoretical analysis of aspects of Mchongoano.* The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics, Vol. 2 (2012), 63-78.

Kindija, K. (2012). *Taaluma ya fonetiki na fonolojia*. Dar es Salaam. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Kombo, D na Tromp, D. (2006). *Proposal and thesis writing.* Nairobi: Paulins.

Konnor G. na Hinter M. (2021). *Impact of Sheng' language in Kenya.*Cairo. Chuo Kikuu cha Cairo.

Makini, N. (2015). *Udhihirikaji wa kanuni ya DAHL katika lugha ya Ekegusii.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Mbaabu, I. (1994). *Sarufi ya Kiswahili sanifu.* Nairobi: Longhorn.

Mbaabu, I.na Kipande, N. (2003). *Swahili- English Dictionary: deciphering East Africa's underworld language.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mbaabu, I. (1996). *Language policy in East Africa: A dependency theory perspective*. Nairobi: Educational Research and Publications.

Mekonge, L. (2016). *Athari za sheng katika ufundishaji wa Kiswahili mjini Kisii: Utafiti kifani wa shule za upili za Gusii Highlights na Daraja Mbili.* Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi.Haijachapishwa.

Mgullu, R. (1999). *Mtaala wa Isimu. Fonetiki na fonolojia*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Michieka, M. (2012). *Language maintenance and shift among Kenyan university students.* In Selected Proceedings of the 41st Annual Conference on African Linguistics, ed. Bruce Connell and Nicholas Rolle, 164-170. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. www. lingref. com, document #2746.

Mmbwanga, F. (2016). *The Sheng Identity, Cultural Background and Their Influence on Communication in Academic Endevours: The Case of Machakos University*. College. https://www. researchgate.net/ publication/352413988. The Sheng Identity Cultural Background and Their Influence on Communication in Academic Endevours. The Case of Machakos University College.

Muaka, L. (2011). *Language Perceptions and Identity among Kenyan Speakers.* In Selected Proceedings of the 40th Annual Conference on African Linguistics, ed. Eyamba G. Bokamba et al., 217-230. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. www.lingref.com, document #2577.

Mugambi, A. (2007). *Utohozi maana katika maneno ya Sheng'*. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mugenda, O. na Mugenda, A. (1999). *Research Methods*. Nairobi: Acts Press.

Mukhwana, A. (2015). *Sheng and Engsh: What they are and what they are not.* International Journal of Scientific Research and Innovative Technology Vol. 2 No. 1; January 2015

Munuku, A. (2005). *Code switching in the Kiswahili contemporary rap song.* Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.Haijachapishwa.

Mwangi, I. na Mukhwana, A (2011). *Isimu Jamii*. Nairobi. Focus.

Mwenesi, M. et al. (2022). *Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Upokezilugha wa Kiswahili Miongoni mwa Wanadaraja la Awali Katika Shule za Msingi Mjini Mbale, Kaunti ya Vihiga, Kenya.* https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.578

Mwihaki, A. (2007). *Viewing Sheng' as a Social Dialect: A Linguistic Approach*. Chemchemi International Journal of the School of Humanities and Social Sciences. Kenyatta University Vol.4 namba2.

Ogechi, O. (2005). *On Lexicalization in Sheng.* Nordic Journal of African Studies 14(3): 334–355

Owino, A. (2016). *Mifanyiko ya kimofofonolojia ya ukuzaji na udunishaji nomino za Kiwanga, Kakamega, Kenya.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Egerton. Haijachapishwa.

Prince, A. and Smolensky, P. (2003). *Optimality theory in phonology*. Oxford: Oxford University Press

Romaine, S. (1994). *Pidgins and Creole languages*, London: Longman.

Salome', G. (2020). *Shaping New Identities: Sheng, Youth, and Ethnicity in Kenya*. https://hir.harvard.edu/author/sgarnier/

*Taifa Leo.* (2021, Juni 22). Dondoo za Hapa na Pale. Gazeti la Taifa Leo. Uk. 12.

Wairungu, M. (2010). *"A language of many hats": The rise of sheng and other linguistic styles among urban youth in Kenya.* Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Virginia, Haijachapishwa.

Warambo, P. (2017). *Uchanganuzi wa maendeleo ya kisematiki katika Sheng: Mtazamo wa pragmatiki Leksika. Tasnifu ya Uzamili*. Haijachapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi.

Warambo, P. et al. (2017). *Neologism: A Narrowing or a Broadening Process, a Case of Sheng.* Journal of Literature, Languages and Linguistics. An International Peer-reviewed Journal. Vol.37, 2017.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho A: Data Iliyotumika Katika Utafiti Huu.

### Orodha ya maneno katika S.E.D yanayojitokeza katika Kiswahili sanifu

| Maneno katika S.E.D. | Aina | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. Ajuta | N | Vyatu | Asikitika |
| 2. Ambaa | T | Ondoka | Kaa mbali na mtu |
| 3. Andasi | N | Matawi ya miraa | Nishai ya ulevi |
| 4. Arifu | N | Rafiki | Enye maarifa mengi |
| 5. Auta | N | Barabara ya Outering, Nairobi. | Nyumba, makao, makaazi |
| 6. Avunja | N | Vyatu vizito | Gawa vipande vipande/asi |
| 7. Babe | N | Msichana mdogo | Tajiri |
| 8. Bachu | N | Miraa | Gololi iliyochakaa. |
| 9. Badili | N | Baba | Ondoa na weka kingine |
| 10. Bado | N | Baba | Wakati haujafika. |
| 11. Bako | N | Mpira wa vikapu | Kipimo cha kitanga cha mkono |
| 12. Bamba | T | Shika | Kuwa bapa, embamba |
| 13. Bango | N | Shilingi moja | Karatasi kubwa ya maandishi |
| 14. Baniani | N | Mtu bahili/mchoyo | Mhindi mfanyibiashara |
| 15. Bano | N | Aina fulani ya jiwe | Chombo cha kubania mbao/chuma |
| 16. Budi | N | Mzazi wa kiume | Jambo la lazima |
| 17. Beti | N | Chupa | Fungu moja la shairi |
| 18. Binda | T | Kuenda | Tunda linalopikwa kama mboga. |
| 19. Boboka | N | Ongea ujinga | Tamka maneno mengi yasiyo na maana. |
| 20. Bomani | N | Bahili, mchoyo | Kwenye boma |
| 21. Bomu | N | Kunya | Silaha ya mlipuko |
| 22. Bonga | T | Ongea | Toboa punji za nafaka |
| 23. Boza | N | Bangi/ dawa za kulevya | Debe kubwa |
| 24. Brandi | V | Mpya | Aina ya pombe kali |
| 25. Buda | N | Mzazi wa kiume/baba | Mwanamme aliyezeeka sana |

| **Maneno katika S.E.D.** | **Aina** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|---|
| 26. Buru | N | Mtaa wa Buruburu | Kibuyu cha kutengeneza siagi. |
| 27. Buu | N | Basi kubwa | Tulia/nyamaza |
| 28. Buyu | N | Baba | Tunda la mbuyu |
| 29. Chafu | N | Mtaalamu/ mwerevu | Enye matendo maovu |
| 30. Chai | N | Hongo | Kinywaji |
| 31. Chambele | N | Ng'ambo | Malipo ya mbeleni ya kuzuia kitu kisiuzwe. |
| 32. Chanuka | T | Kuwa katika mtindi/hali ya kisasa | Mmea kuota maua |
| 33. Chanja | T | Changia/kusanya | Kata vipande |
| 34. Chapa | T | Funga bao mchezoni | Piga ili kuumiza |
| 35. Chapati | N | Mapigo/ngumi | Mkate bapa |
| 36. Chati | T | Ongea uongo | Mchoro wa maelezo na takwimu |
| 37. Cheki | T | Angalia | Hundi ya pesa |
| 38. Chira | N | Ukimwi | Laana, kumtakia mtu mabaya |
| 39. Chizi | N | Wazimu | Mwenye akili punguani |
| 40. Chizika | T | Kuwa wazimu | Maji kudondoka kidogo kidogo |
| 41. Chokora | N | Watoto wa mitaani | Tafuta kwa kutawanya |
| 42. Choma | T | Vuta bhangi | Teketeza kwa moto |
| 43. Chongoa | T | Chochea | Fanya kitu kiwe na ncha kali |
| 44. Chora | T | Kuandika | Toa mfano wa mtu/kitu kwa kalamu |
| 45. Chorea | T | Andaa mpangilio | Chora kwa niaba ya mtu |
| 46. Chota | T | Kutoa pesa | Twaa au chukua sehemu ya kitu |
| 47. Chuja | N | Vyatu | Kamua kwa mikono |
| 48. Chukulia | T | Nunua kitu, fanya mtu aonekane mjinga | Kuwa na imani juu ya jambo |
| 49. Chuma | N | Shilingi moja | Fanya kazi/biashara/madini magumu |
| | | | |

| **Maneno katika S.E.D.** | **Aina** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|---|
| 50. Churo | N | Kahaba | Enye kisirani |
| 51. Chuo | N | Shule | Ndoa/taasisi ya mafundisho |
| 52. Daa | N | Mjinga kabisa | Funza wa kuvulia samaki |
| 53. Dafu | N | Shilingi mia moja | Nazi changa yenye maji matamu |
| 54. Dago | N | Mtaa wa Dagoretti | Kambi ya wavuvi. |
| 55. Dakia | N | Anayeongea matusi | Fanya haraka/pita juu |
| 56. Danda | N | Mjinga | Rukia chombo cha usafiri |
| 57. Dandia | T | Kukalia | Abiri chombo bila idhini |
| 58. Dara | T | Papasa | Papasa |
| 59. Deka | N | Kuona | Jivunia/ringia, tumainia msaada |
| 60. Dema | T | Kula chakula | Mtego wa kuvulia samaki |
| 61. Depo | N | Naibu wa mwalimu mkuu | Mahali pa kuhifadhi vitu |
| 62. Dimba | N | Mchuano wa kandanda | Mchezo wa kandanda |
| 63. Dinda | T | Kataa kwa kiburi | Kata/kuwa imara |
| 64. Diro | N | Dirisha | Mahali ambapo watu wengi hula |
| 65. Dishi | T | Kula chakula | Chombo cha kutilia chakula |
| 66. Dodosa | T | Tingiza kiuno | Sitasita ukisoma/ukiongea |
| 67. Dondoka | T | Shuka kwa gari | Anguka kutoka juu |
| 68. Doro | T | Lala | Siochangamka/liozubaa |
| 69. Doti | T | Kuongea visivyo | vipande vya kitambaa |
| 70. Duba | N | Matako | Kuwa nusu ya kipimo kamili |
| 71. Dufu | T | Kuongelea | Ngoma ndogo ya Waislamu. |
| 72. Dunda | V | Kataa, anguka kwa kishindo | Gonga kama mpira/pigisha kama |
| 73. Duru | T | Lala | Zamu/zunguka kila mahali |
| | | | |

| **Maneno katika S.E.D.** | **Aina** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|---|
| 74. Enga | V | Kujifanya huoni mtu | Kata kwa kisu/upanga |
| 75. Fala | N | Asiyejua kusoma au kuandika | Mpumbavu/bozi |
| 76. Feri | T | Anguka chini | Pantone |
| 77. Fifi | N | Miraa | Siokuwa na thamani |
| 78. Finyo | N | Ongeza uongo | Mbano wa ncha ya vidole |
| 79. Futa | N | Mchezo wa kandanda | Panguza kitu kilichoandikwa. |
| 80. Futi | N | Mchezo wa kandanda | Kipimo cha urefu wa inchi 12. |
| 81. Gamu | N | Gundi | Kitu majimaji cha kunata |
| 82. Gange | N | Kazi ya kuajiriwa | mawe ya chokaa/kazi |
| 83. Ganja | N | Mihadarati | Bangi/aina ya jahazi lenye mlingoti |
| 84. Gesi | T | Kosa pesa/ filisika | Hewa |
| 85. Gizani | E | Gerezani | Kutokuwa na mwangaza |
| 86. Gogi | N | Miwani ya jua | Maringo/majivuno. |
| 87. Gomba | N | Miraa | Zua rabsha/fujo, nyuzinyuzi za mgomba |
| 88. Gota | T | Piga mtu vikumbo. | Fikia kikomo. |
| 89. Guchi | T | Enda | Tembea kwa mchechemeo |
| 90. Gwanda | N | Vyatu vya kuchezea soka | Vazi fupi la kitambaa |
| 91. Gwara | T | Iba | Sarafu ya fedha au shaba |
| 92. Gwaya | N | Hali ya kuogopa | Tetemeka kwa baridi |
| 93. Haha | T | Kutulia | Babaika ukiongea |
| 94. Haja | N | Shilingi mia moja | Hitaji la mtu/ uchafu wa mwili |
| 95. Hamasa | N | Shilingi hamsini | Ari/uwezo wa kutenda jambo |
| 96. Hara | T | Kuelewa, kukosa pesa | Kubali kuwa mwenzako ana uwezo kubwa/enda choo |
| | | | |

| Maneno katika S.E.D. | Aina | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|
| 97. Heri | N | Uongo | Fanikiwa/ hali ya amani |
| 98. Honda | N | Pikipiki | Gari la gurudumu mbili |
| 99. Hori | T | Ogopa | Mkono wa bahari ghuba/ chombo cha bahari |
| 100. Inda | N | Sehemu ya viwandani | Wivu |
| 101. Inua | T | Piga mtu | Weka juu kutoka chini |
| 102. Ishia | T | Ondoka | malizikia |
| 103. Jaa | T | Kuwa kubwa, nona | Pahali pa taka/kuwa mkubwa |
| 104. Jahi | N | Tajiri | Ncha ya kaskazini mwa dunia |
| 105. Jaivu | T | Fanya mzaha | Mtindo wa densi ya zamani |
| 106. Jaka | N | Mtu wa jamii ya Wajaluo. | Kichaka kikubwa |
| 107. Jamu | T | Kasirika | Rojo ya kupaka kwa mkate. |
| 108. Jezi | N | Sare ya shule | Fulana ya wanamichezo |
| 109. Jiji | N | Nairobi | Mji mkubwa |
| 110. Jikamua | T | Kojoa | Jitahidi |
| 111. Jisikia | T | Penda | Jihisi/jione bora |
| 112. Jongo | N | Sarafu ya shilingi moja | Maradhi ya kuvimba miguu. |
| 113. Jumu | N | Viatu | Kapu kubwa mbovu |
| 114. Kaa | H | Fanana | Jinsi kinavyoonekana/aina ya mnyama, keti |
| 115. Kago | N | Vitu vya thamana | Hirisi |
| 116. Kalasi | T | Kufika mwisho | Chombo cha kusafiri baharini |
| 117. Kale | N | Mkalenjini | Zamani |
| 118. Kambambe | N | Mpira wa kandanda | Kubwa sana |
| 119. Kambi | N | Chuo kikuu cha Nairobi | Eneo la kupumzikia, makaazi ya jeshi |
| 120. Karo | N | Kipande cha karatasi | Mahali pa kuoshea vyombo. ada ya shule |

| Maneno katika S.E.D. | | Aina | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|---|
| 121. | Kasa | N | Mtaa wa kasarani | Mnyama aina ya kobe aishie baharini |
| 122. | Kata | T | Ondoka | Tenganisha kwa kisu |
| 123. | Katia | T | Tongoza | Kata kwa niaba ya mwingine |
| 124. | Kavu | N | Noti ya shilingi elfu moja | Siokuwa na maji |
| 125. | Kenge | N | Pesa | Mnyama mdogo katika jamii ya mamba |
| 126. | Kiapo | N | Dawa za kulevya | Yamini, zindiko la kuzuia wezi |
| 127. | Kibichi | N | Mtaa wa Kibira | Sioiva vizuri |
| 128. | Kibuda | N | Mzee mdogo | Mwanamume aliyezeeka |
| 129. | Kifaranga | N | Msichana mdogo | Mtoto wa kuku |
| 130. | Kijiko | T | Kimbia | Kifaa cha kuchukulia chakula |
| 131. | Kiki | T | Kufa | Pigo moja la mpira |
| 132. | Kinaa | N | Ujinga, shida | Hali ya kutosheka na kitu |
| 133. | Kinai | T | Kufa | Kosa hamu ya chakula |
| 134. | Kinda | T | Iba, saliti | Kijana. mtoto wa ndege. mti mdogo |
| 135. | Kiranja | N | Mwabudu shetani | Kijana aliyetahiriwa |
| 136. | Kisanga | N | Mada inayojadiliwa | Tukio la mkasa /balaa |
| 137. | Kishua | T | Kuwa ya ukweli | Mashua ndogo |
| 138. | Kiswa | N | Lugha ya Kiswahili | Vazi la heshima la dini |
| 139. | Kitete | N | Dawa ya kulevya /bangi | Kuwa wasiwasi /woga |
| 140. | Kitoe | T | Ondoka | Ondoa kitu |
| 141. | Koboa | T | Piga kofi | Vina hindi kwa kuvunja |
| 142. | Kobole | N | Sarafu ya ncha saba | Sarafu ya shilingi tano |
| 143. | Koki | N | Soda ya cocacola | Tayarisha bunduki kuifyatua |
| 144. | Kole | N | Chuo | Kikonyo cha kushikilia matunda kwa mti |
| 145. | Koma | N | Shilingi elfu moja | Alama ya uandishi. acha. |

| Maneno katika S.E.D. | | Aina | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|---|
| 146. | Komo | N | Mtaa katika wilaya ya Kiambu | Sehemu ya mbele kati ya uso na macho |
| 147. | Konda | N | Makanga | Kuwa mnyonge |
| 148. | Koni | N | Mlaghai | Mnyama mdogo kama komba |
| 149. | Kopa | N | Afisa wa polisi | Omba ili urudishe |
| 150. | Kosi | N | Mavazi ya ndani | Kamba ya kushikilia chombo cha bahari |
| 151. | Koya | N | Makaazi ya wafanyikazi katika boma | Furahi baada ya kukamilika kwa jambo |
| 152. | Krosi | N | Mbio ya nyikani | Piga mpira kutoka upande mmoja hadi mwingine |
| 153. | Kuli | N | Vyatu vya kuchezea | Mbebaji mizigo bandarini |
| 154. | Kujichoma | T | Kuanza mradi na kushindwa | Kufanya uungue mwenyewe |
| 155. | Kunja | T | Papasa | Pinda/beta |
| 156. | Kuro | N | Kahaba | Mnyama kama paa. |
| 157. | Kusanya | T | Iba | Weka pamoja |
| 158. | Laghai | N | Rafiki wa karibu sana | Mdanganyifu. shawishi kwa hila |
| 159. | Laiki | T | Penda | Tosha. lingana na mwingine |
| 160. | Lalia | T | Kudhibiti/tawala hali | Weka mwili kwa kitu kingine |
| 161. | Lapa | T | Puuza | Tamani. randa. aina ya kiatu. |
| 162. | Lebo | N | Msichana mrembo | Chapa inayoonyesha umilikaji. |
| 163. | Lenga | T | Jifanya huoni | Angaza ili kupata shabaha |
| 164. | Linga | N | Mpishi | Pima kwa makini |
| 165. | Lola | T | Kuona | Tazama /angalia |
| 166. | Mabao | N | Hisi njaa | Utabiri wa nyota. Jukwaa. Goli |
| 167. | Mada | T | Ua | Ujumbe wa habari |
| 168. | Madoido | V | Kiburi | Urembo unaoongezewa kitu |

| **Maneno katika S.E.D.** | | **Aina** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|---|---|
| 169. | Mambo | N | Hadithi | Wingi wa jambo. matukio. kigingi |
| 170. | Manamba | N | Utingo | Wafanyikazi wahamiaji shambani |
| 171. | Manda | T | Ua | Aina ya mkate umbo duara. |
| 172. | Manga | T | Kukula chakula | Bara la Arabu, Arubuni |
| 173. | Mango | N | Matiti | Jiwe ngumu la kusugulia vitu |
| 174. | Manya | T | Kula /kuelewa | Fahamu/ elewa |
| 175. | Manyanga | N | Kitu kipya kama gari | Ala ya muziki |
| 176. | Mashini | N | Kazi | Kinu/mtambo |
| 177. | Maskani | N | Chumba cha kujificha | Makaazi |
| 178. | Matunda | N | Msichana mrembo | Zao la mmea/chuma |
| 179. | Matwana | N | Matatu | Gari la kuchukua abiria na mizigo |
| 180. | Mbao | N | Shilingi ishirini | Mazao ya mmea yenye mbegu na majimaji |
| 181. | Mbochi | N | Kijakazi | Maji katika maua /nekta |
| 182. | Mbu | N | Gari kubwa /basi | Mdudu anayesambaza malaria |
| 183. | Mbuku | N | Vitabu | Mtu mchoyo |
| 184. | Mbuyu | N | Baba | Mti wenye shina kubwa |
| 185. | Mchuma | N | Bastola | Anayefanya shughuli ya kuvuna vitu |
| 186. | Mea | T | Enda/ondoka | Kua kutoka ardhi au mwili |
| 187. | Mei | N | Mahindi | Mwezi wa tano |
| 188. | Mezea | T | Elewa/ongea ukweli | Teremshia chakula hadi tumboni |
| 189. | Minya | T | Kukula chakula | Finya kiwe laini |
| 190. | Mkale | N | Jamii ya wakalenjini | Mtu aliyekomaa wa ujuzi wa zamani |
| 191. | Mng'aro | N | Nguo mpya | Kitu kinachotoa nuru |
| 192. | Mosi | T | Pole pole | Iliotangulia |
| 193. | Mrengo | T | Kuwa na mpango na mtu mwingine | Wafuasi tofauti wa kundi/dhehebu |

| **Maneno katika S.E.D.** | | **Aina** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|---|---|
| 194. | Mtaa | N | Town | Sehemu iliyojitenga na mji |
| 195. | Mtambo | N | Saa ya mkono/ gari | Mashinu/ kifaa cha kutoa nguvu |
| 196. | Mtumba | N | Nguo kuukuu | Nguo kuukuu |
| 197. | Msamba | V | Mtu mjinga | Sehemu ya mwili kati ya mapaja |
| 198. | Msusu | N | Mchumba wa kiume | Mti ambao matawi yake ni dawa ya maradhi ya zinaa |
| 199. | Muda | T | Kuwa kimya | Kipindi cha wakati |
| 200. | Muone | T | Mpige | Mwangalie |
| 201. | Mzubao | V | Changanyikiwa akili | Hali ya bumbuazi |
| 202. | Mwambo | N | Chungu cha chuma | Hali ya kukosa pesa |
| 203. | Mwango | N | Noti ya shilingi mia tano | Sehemu ya kuangikia taa |
| 204. | Mwasi | N | Msichana | Enda kinyume |
| 205. | Mzizi | N | Mmea wa kulevya | Sehemu ya mmea chini ya ardhi |
| 206. | Nai | N | Mji wa Nairobi | Ala ya muziki nyembamba |
| 207. | Nazi | T | Chochea/ fanya uchochezi | Tunda la mnazi |
| 208. | Ndusi | N | Mbwa | Kasha /sanduku la vitu vya thamana |
| 209. | Ng'ara | T | Fanya kitu kwa njia nzuri | Ng'aa/shabikia hali fulani |
| 210. | Ngiri | N | Noti ya shilingo mia moja | Mnyama wa pori/aina ya maradhi. |
| 211. | Ng'oa Jiwe | N | Mtu wa sura mbaya | Vuta na kutoa jiwe |
| 212. | Ngoi | N | Mlinzi | Stadi wa kuongoza nyimbo |
| 213. | Ng'oka | T | Kufa | Toka na mizizi |
| 214. | Ng'ota | T | Piga mtu | Toka baada ya kuvutwa |
| 215. | Ngoto | N | Kiingereza | Konzi / vidole vilivyokunjwa |
| 216. | Ngwa | N | Mstari uliolainika | Mali ya mtu |

| Maneno katika S.E.D. | | Aina | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|---|
| 217. | Ng'wea | T | Nuka | Konda |
| 218. | Niaje | V | Salamu za kujulia hali | Iko namna gani |
| 219. | Nira | V | Mpya | Kipande cha mti kinachofungiwa fahali/farasi |
| 220. | Njumu | N | Viatu | Misumari kwenye viatu vya kuchezea |
| 221. | Noma | N | Shida | Kadi ya kujitambulisha mahali pa kazi |
| 222. | Nyaka | N | Kiti | Ruka na kushika kitu |
| 223. | Nyege | N | Figo | Hamu ya mapenzi |
| 224. | Nyiga | T | Elewa | Sehemu inayoota nyasi na miti |
| 225. | Nyoa | T | Sema ukweli wa jambo | Ondoa nywele kwa kichwa |
| 226. | Nyonga | T | Vaa tai | Kiungo cha mwili/kaba kooni |
| 227. | Nyuki | N | Pombe kali ya chang'aa | Mdudu aumaye kwa mshale |
| 228. | Omoka | T | Kuwa tajiri / fanikiwa | Bomoka sehemu ya nyumba |
| 229. | Ona | T | Piga kofi | Tazama |
| 230. | Ondoa | T | Kukula chakula | Toa |
| 231. | Orodha | E | Kuwa karibu, zunguka karibu | Mpangilio wa majina/vitu |
| 232. | Ozoni | N | Kiwango cha juu | Utando uzungukao jua |
| 233. | Paka | N | Uvumi | Eneza rangi/mnyama wa nyumbani |
| 234. | Pale | N | Rafiki mkuu | Kionyeshi cha mahali |
| 235. | Pandisha | T | Sema uongo | Elekeza kitu juu/ bei iwe juu |
| 236. | Panja | N | Mwezi | Paji la uso |
| 237. | Papa | N | Mzazi wa kiume | Tamko la kusistiza mahali/ mnyama wa baharini |
| 238. | Pango | N | Mtaa wa Pangani jijini Nairobi | Nafasi kubwa katika miti/majabali |
| 239. | Penya | T | Ondoka ukikimbia | Jiingize kwa kitu |
| 240. | Pepea | T | Enda | Tikisatikisa |

| **Maneno katika S.E.D.** | | **Aina** | **Kamusi ya *Sheng'*** | **Kamusi Sanifu** |
|---|---|---|---|---|
| 241. | Pepeta | T | Kula | Tupatupa juu |
| 242. | Pepo | N | Adhabu | Mbinguni/shetani/mzuka |
| 243. | Peremba | T | Chukua pesa kutoka kwa mfuko wa mtu | Tembea kwa uangalifu |
| 244. | Pewa | T | Kunywa pombe | Kuwa kwa hali ya kupokea |
| 245. | Picha | N | Filamu | Mfano wa mtu/kitu |
| 246. | Pigilia | T | Vaa nguo | Gonga msumari |
| 247. | Pitisha | T | Leta | Penyeza kitu mahali fulani |
| 248. | Plani | N | Makubaliano | Mpangilio |
| 249. | Po | V | Nzuri | Neno linalotumiwa kwa ishara ya kutema mate |
| 250. | Poa | V | Kuwa sawa | Nyamaza/fifia |
| 251. | Pori | N | Polisi | Sehemu iliyojaa miti na nyasi |
| 252. | Pozi | T | Tazama | Tuliza mwili kabla ya kupigwa picha |
| 253. | Puru | N | Peremende | Ugonjwa wa bawasiri |
| 254. | Rada | N | Kuwa chonjo /mwangalifu | Adhabu ya Mungu/kifaa cha kuongoza ndege |
| 255. | Rusha | T | Umiza/ sababisha uchungu | Tupa juu/mbali |
| 256. | Safi | N | Mihadarati | Nadhifu, jema |
| 257. | Salala | N | Salamu | Nyama nyororo kwenye uti wa mgongo |
| 258. | Sanifu | T | Shahidi | Chora umbo/zingatia viwango |
| 259. | Sanya | T | Iba | Weka pamoja |
| 260. | Sanywa | V | Kulewa zaidi | Chukuliwa na kuwekwa pamoja |
| 261. | Sasa | V | Salamu | Wakati huu/uliopo |
| 262. | Sembe | N | Ugali | Sima/ugali |
| 263. | Semi | N | Seminari | Mchuano wa mpira kabla ya fainali |
| 264. | Seti | T | Anza | Fungu la idadi fulani ya vitu |

| Maneno katika S.E.D. | | Aina | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|---|
| 265. | Sato | N | Jumamosi | Samaki wa maji baridi mwenye magamba meusi |
| 266. | Shaba | N | Msichana, kitu cha thamana | Aina za madini za kuunda waya |
| 267. | Shabu | N | Msichana mrembo | Jiwe jeupe la kusafisha maji |
| 268. | Shada | N | Dawa za kulevya | Mkazo kwenye neno |
| 269. | Shafti | N | Mkoba | Chuma cha kuzungusha gurudumu kutoka kwa injini |
| 270. | Shari | H | Mtu | Jambo linalosababisha hasara |
| 271. | Shiriki | T | Kupooza kwa kulewa zaidi | Fanya mambo pamoja |
| 272. | Shombe | N | Mpenzi wa kiume | Mtoto wa wazazi wa rangi tofauti |
| 273. | Shona | N | Kinai/rithika | Shikanisha kwa uzi |
| 274. | Shonde | N | Kwenda haja/kujisaidia | Kusanyiko la kinyesi |
| 275. | Sinya | N | Polisi | Chukiza |
| 276. | Sista | N | Dada wa kike | Mtawa mwanamke |
| 277. | Soksi | N | Mipira ya mapenzi | Vaazi livaliwalo miguuni kabla ya viatu. |
| 278. | Sota | N | Misukosuko | Jikokota au songa kwa makalio |
| 279. | Stadi | N | Uga wa mpira | hodari/ mwenye ujuzi wa juu |
| 280. | Stori | N | Hadithi | Hadithi |
| 281. | Sugu | N | Kitu kigumu | kutosikia adhabu/ugumu katika mwili |
| 282. | Sukuma | N | Tai ya kuvaa shingoni | Lazimisha kwa nguvu |
| 283. | Surua | N | Sabuni | Homa kali ya watoto |
| 284. | Tai | T | Tahiri | Aina ya mwewe |
| 285. | Tao | N | Mji | Mkato wa kitambaa nusu duara |
| 286. | Tegea | T | Ngojea | Wekea mtego |
| 287. | Tele | N | Runinga | Mpaka juu/enye kujaa |

| Maneno katika S.E.D. | | Aina | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|---|
| 288. | Tema | T | Toa hongo | Toa kinywani/kata kitu kama vile kuni. |
| 289. | Tembe | N | Dawa ya kulevya | Kidonge cha dawa |
| 290. | Tia | T | Kunywa | Ingiza |
| 291. | Tilia | T | Sema | Pea mtu chakula |
| 292. | Tindi | T | Kuwa mlevi | Kifundo cha maungio katikati mwa viganja |
| 293. | Tinga | T | Funga bao/shinda | Funga bao/enda huku na huku |
| 294. | Tini | N | Kijana mdogo | Tunda kama pera lenye nyama nyingi |
| 295. | Tokea | T | Vaa nadhifu | Tukia, jiri |
| 296. | Toma | N | Nyanya /tomato | Ingia mahali kwa kasi |
| 297. | Tonga | T | Kula chakula | Toa sauti kali |
| 298. | Tota | N | Msichana | Ingia na kitu cha majimaji kwa wingi |
| 299. | Tuna | T | Lala | Fura/vimba nuna |
| 300. | Tupa | T | Nuka | Rusha |
| 301. | Ua | T | Kuwa yako | Ondoa uhai |
| 302. | Ubao | N | Hisi njaa | Sehemu ya gogo lililopasuliwa |
| 303. | Uganga | N | Ugali | Taaluma ya kutibu na kuponya |
| 304. | Ugoro | N | Dhahabu | Tumbaku iliyosagwa |
| 305. | Ukara | N | Kijikaratasi | Aina ya muundo wa shairi |
| 306. | Ukata | T | Kufa | Umaskini |
| 307. | Ukoo | V | Nzuri, muhimu | Uzawa wa jamii |
| 308. | Ulipo | N | Sapatu | Mahali mtu ako |
| 309. | Umbika | V | Rembeka, vutia | Kuwa na umbo/sura ya kupendeza |
| 310. | Umo | N | Mtaa wa Umoja | Kuwa ndani ya kitu. |
| 311. | Unda | T | Piga mtu | Jenga, tengeneza |
| 312. | Undu | V | Kitu kisicho na maana | Kishingi chekundu cha jogoo |
| 313. | Unyoya | T | Kimbia kwa kasi | Mabawa ya ndege |
| 314. | Ushoga | N | Soga | Usenge/urafiki kati ya waume |
| 315. | Usuko | H | Enda na ondoka | Namna ya kusuka |
| | | | | |

| Maneno katika S.E.D. | | Aina | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|---|
| 316. | Utambi | N | Tumbo kubwa | Uzi wa kuwashia taa ya mafuta |
| 317. | Vaa | T | Piga/chapa | Eneza kitu/nguo kwa mwili |
| 318. | Vunja | T | Piga mtu | Fanya kitu kiwe vipande |
| 319. | Waka | T | Lewa zaidi | Toa mwangaza |
| 320. | Wanga | N | Mpenzi wa kike | uma, umia/ unga wa kunyoshea nguo |
| 321. | Wango | N | Pombe kali ya kienyeji | Jinsi ya kuhesabu |
| 322. | Waria | N | Mtu wa jamii ya Wasomali | Mtaalam wa kazi za mikono |
| 323. | Wati | N | Maji | Kipimo cha nguvu za umeme |
| 324. | Watisha | N | Fulana/ aina ya shati | Wazua hofu |
| 325. | Waya | T | Kosa pesa/filisika | Uzi mwembamba wa chuma |
| 326. | Wazee | N | Wazazi | Wenye umri mkubwa |
| 327. | Wazi | N | Ahsante | Enye kuonekana |
| 328. | Wembe | H | Enda kwa kasi sana | Kifaa bapa bati cha kukatia |
| 329. | Zama | T | Jificha | Tumbukia majini/kale |
| 330. | Ziara | H | Kuwa mviringo | Safari ya kuzuru mahali |
| 331. | Zii | T | Tulia | Tamko la kuonyesha dharau |
| 332. | Ziki | N | Muziki | Aina ya mshono unaozunguka shingo |
| 333. | Zima | T | Mtaa wa Zimerman | Fanya kisiendelee kuwaka |
| 334. | Zusha | T | Anzisha mgogoro/kasirika | Anzisha kuenea |
| 335. | Zuzu | N | Mpumbavu | Mjinga |

## Kiambatisho B: Kibali cha Utafiti cha Chuo Kikuu cha Kenyatta.

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

**P.O. Box 43844, 00100**
**NAIROBI, KENYA**
**Tel. 8710901 Ext. 57530**

---

**Our Ref:** C50/CE/26142/2014

**DATE:** 1st February, 2022

Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR JOTHAM MUYUMBA – REG. NO. C50/CE/26142/2014.**

I write to introduce **Jotham Muyumba** who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the **Department of Kiswahili.**

**Jotham** intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, **"Athari Za Sheng' Kwa Kiswahili Sanifu: Uchunguzi Wa Kamusi Ya Sheng"."**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

PROF. ELISHIBA KIMANI
AG. DEAN, GRADUATE SCHOOL

EM/nn

## Kiambatisho C : Leseni ya Utafiti ya Nacosti.

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 301365

Date of Issue: 25/February/2022

### RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Mr.. JOTHAM MUYUMBA of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Kakamega on the topic: ATHARI ZA SHENG' KWA KISWAHILI SANIFU: UCHUNGUZI WA KAMUSI YA SHENG'. for the period ending : 25/February/2023.**

License No: **NACOSTI/P/22/15990**

**301365**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commision for Science, Technology and Innovation -

**Kiambatisho D : Kibali cha Utafiti cha Kaunti Ndogo ya Kakamega Kaskazini.**

MINISTRY OF EDUCATION

Telegram:
Telephone: 0710697611
When replying please quote
E-mail kakameganorth@yahoo.com

SUB-COUNTY EDUCATION CE
KAKAMEGA NORTH SUB-COUNTY
P. O. BOX 34- 50103
MALAVA

STATE DEPARTMENT OF EARLY LEARNING AND BASIC EDUCATION

Date 1ST MARCH, 2022

TO.
PRINCIPALS
KAKAMEGA NORTH SUBCOUNTY

RE: MR. JOTHAM MUYUMBA REG NO:C50/CE/26142/2014

The above has been granted permission by National Council for Science &Technology vide their letter Ref. NACOSTI/P/21/15990 dated 25th February 2022 to carry out research on "ATHARI ZA SHENG KWA KISWAHILI SANIFU: UCHUNGUZI WA KAMUSI YA SHENG, "for the period ending 25th Feb 2023.

Kindly accord him the necessary assistance when he visits your institution

For SUB-COUNTY
DIRECTOR OF EDUCATION
KAKAMEGA NORTH
P. O. Box 34-50103. MALAVA
Date:............... Sign:...............

PP

**ROSELYNE CHISUMI**
**SUB COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION**
**KAKAMEGA NORTH**

## Kiambatisho E : Kibali cha Utafiti cha Kaunti ya Kakamega.

REPUBLIC OF KENYA

MINISTRY OF EDUCATION

STATE DEPARTMENT OF EARLY LEA3RING AND BASIC EDUCA4TION

Telephone: 056 -30411
Fax: 056 – 31307
E-mail: rceducation2016@gmail.com
When replying please quote our Ref

County Director of Education
Kakamega County
P. O. BOX 137 - 50100
KAKAMEGA

**REF: KAKA/C/GA/29/17/VOL.VI/40**

**4th May, 2022**

Mr.Jotham Muyumba,
KENYATTA UNIVERSITY
**P.O. Box 43844,**
**NAIROBI**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Reference is made to a letter from the Ref.No. *NACOSTI/P/22/15990 dated 25th* February, 2022 concerning subject matter,

This is to inform you that you have been authorized to carry out research on **'Athari za sheng' kwa Kiswahili sanifu : Uchunguzi wa Kamusi ya sheng'** for the period ending 25th February,2023.

Please accord him/her any necessary assistance he/she may require.

FOR
COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KAKAMEGA COUNTY

DICKSON O. OGONYA
COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KAKAMEGA COUNTY

*Copy to*:
The Regional Director of Education
WESTERN REGION

## Kiambatisho F: Ripoti ya Uzuiaji Wizi wa Kiakademia

ATHARI ZA SHENG' KWA KISWAHILI SANIFU: UCHUNGUZI WA KAMUSI YA SHENG'.

ORIGINALITY REPORT

| 6% | 5% | 1% | 3% |
|---|---|---|---|
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
|---|---|---|
| 1 | ir-library.ku.ac.ke<br>Internet Source | 1% |
| 2 | erepository.uonbi.ac.ke:8080<br>Internet Source | 1% |
| 3 | Submitted to Kenyatta University<br>Student Paper | 1% |
| 4 | Submitted to University Der Es Salaam<br>Student Paper | <1% |
| 5 | erepository.uonbi.ac.ke<br>Internet Source | <1% |
| 6 | repository.out.ac.tz<br>Internet Source | <1% |
| 7 | masshele.blogspot.com<br>Internet Source | <1% |
| 8 | edocs.maseno.ac.ke<br>Internet Source | <1% |
| 9 | journals.openedition.org<br>Internet Source | <1% |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | 1library.net<br>Internet Source | <1% |
| 11 | mwalimuwakiswahili.co.tz<br>Internet Source | <1% |
| 12 | ejournal.stp-bandung.ac.id<br>Internet Source | <1% |
| 13 | repository.suza.ac.tz:8080<br>Internet Source | <1% |
| 14 | pseudepigraphas.blogspot.com<br>Internet Source | <1% |
| 15 | sinyati.blogspot.com<br>Internet Source | <1% |
| 16 | Submitted to University of South Africa<br>Student Paper | <1% |
| 17 | Submitted to Eiffel Corporation<br>Student Paper | <1% |
| 18 | library.kisiiuniversity.ac.ke:8080<br>Internet Source | <1% |
| 19 | ohq.evinceitnc.space<br>Internet Source | <1% |
| 20 | profiles.uonbi.ac.ke<br>Internet Source | <1% |
| 21 | Submitted to Laureate Higher Education Group | <1% |

Student Paper

| | | |
|---|---|---|
| 22 | journals.udsm.ac.tz<br>Internet Source | <1% |
| 23 | Submitted to Middle East Technical University<br>Student Paper | <1% |
| 24 | Submitted to Mount Kenya University<br>Student Paper | <1% |
| 25 | sw.wikipedia.org<br>Internet Source | <1% |
| 26 | Submitted to University of Oxford<br>Student Paper | <1% |
| 27 | ebin.pub<br>Internet Source | <1% |
| 28 | ir-library.mmust.ac.ke<br>Internet Source | <1% |
| 29 | www.coursehero.com<br>Internet Source | <1% |
| 30 | Naomi van Stapele. "'When the Numbers Stop Adding': Imagining Futures in Perilous Presents Among Youth in Nairobi Ghettos", The European Journal of Development Research, 2020<br>Publication | <1% |
| 31 | erepository.mku.ac.ke<br>Internet Source | <1% |

| | | |
|---|---|---|
| 32 | halshs.archives-ouvertes.fr<br>Internet Source | <1% |
| 33 | repository.rongovarsity.ac.ke<br>Internet Source | <1% |
| 34 | www.njas.helsinki.fi<br>Internet Source | <1% |
| 35 | David B. Wandera. "Resisting Epistemic Blackout: Illustrating Afrocentric Methodology in a Kenyan Classroom", Reading Research Quarterly, 2019<br>Publication | <1% |
| 36 | manyama1.blogspot.com<br>Internet Source | <1% |
| 37 | manyamacharles.blogspot.com<br>Internet Source | <1% |
| 38 | salsa.ling.utexas.edu<br>Internet Source | <1% |
| 39 | kiswahiliashirafu.com<br>Internet Source | <1% |
| 40 | teses.usp.br<br>Internet Source | <1% |
| 41 | Submitted to Chuka University<br>Student Paper | <1% |
| 42 | doczz.net<br>Internet Source | <1% |

| | | |
|---|---|---|
| 43 | theblackboard.co.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 44 | kiswahilisolutioncenter.wordpress.com<br>Internet Source | <1 % |
| 45 | repository.up.ac.za<br>Internet Source | <1 % |
| 46 | www.royalliteglobal.com<br>Internet Source | <1 % |
| 47 | easpublisher.com<br>Internet Source | <1 % |
| 48 | japhetmasatu.blogspot.com<br>Internet Source | <1 % |
| 49 | mambo.hypotheses.org<br>Internet Source | <1 % |
| 50 | mauthamani.blogspot.com<br>Internet Source | <1 % |
| 51 | repository.maseno.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 52 | serialpublishers.org<br>Internet Source | <1 % |
| 53 | sw.m.wikipedia.org<br>Internet Source | <1 % |
| 54 | tunuzakiswahili.blogspot.com<br>Internet Source | <1 % |

| | | |
|---|---|---|
| 55 | www.rsisinternational.org<br>Internet Source | <1% |

Exclude quotes Off

Exclude bibliography On

Exclude matches < 8 words